Nipashe
Ijumaa Novemba 8, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580070
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US


Vanilla inapoongezeka zao la matumaini kwa wakulima Ukurasa 19
'Mkaa Endelevu' unavyowaibua kimaendeleo wakazi wa Kilosa Ukurasa 14
BUFE
Ijumaa Novemba 8, 2019
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Mwanamitindo Odemba kumtua mama ndoo Ukurasa 15
Jaji Mihayo: Niliikuta TTB hoi, madeni na akaunti, sasa walau inatazamika
Na Beatrice Philemon
TANZANIA imo katika orodha ya nchi zilizobarikiwa kuwa na vivutio vingi vya utalii na vinailetea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Hivi sasa, imejikita zaidi kuboresha miundombinu yake ifikike kirahisi kwa Watanzania kwa ujumla.
Hapo kunatajwa mambo kama ununuzi wa ndege, kurahisisha usafiri wa watalii kwenda kuona vivutio vya utalii.
Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji, Devota Mdachi, bodi imefanya mapitio ya sheria, na imeongezwa majukumu ya msingi ya taasisi kutoka matano hadi 11, yanayojumuisha ukuzaji sekta ya Mikutano na Matukio (MICE).
Maeneo mengine yaliyoongezwa katika sheria hiyo ni jukumu la kutangaza utalii wa ndani, kuendeleza ushirikiano kati ya mashirika na wadau wa sekta na kuanzisha zao la Utalii wa Mikutano na Matukio.
INAENDELEA UK.16
UCHUMI
Habari katika picha Ukurasa 17
Ewura yabuni mbadala vijijini kukabili 'maduka' ya madumu Ukurasa 18

UKURASA 13



## Raia 32 wa China wanusurika kifungo kwa kulipa mil. 591/-

UKURASA 3



# Chadema yajitoa uchaguzi mitaa

• **Yatoa** tamko zito, ACT - Wazalendo yaanika vioja wagombea wake kukatwa... *Endelea ukurasa 2*



Distributed via ippmedia

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akiagana na Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Dk. Stergomena Tax, baada ya kufungua Mkutano wa siku tano wa Mawaziri wa Sekta ya Afya na Ukimwi wa Nchi 16 Wanachama wa jumuiya hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu. **Habari uk.2. PICHA: OMR.**

## Hukumu kesi kina Malinzi yakwama

UKURASA 3



Scan Hapa
Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store


## Musukuma atao tahadhari kuhusu mapato Jiji Dodoma

UK.2

MICHEZO YANGA, NDANDA HAPATOSHI BARA UK.32
MAONI, KATUNI UK.6

# SADC yawataka wanachama wajitegemee huduma za afya

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), imezitaka nchi wanachama kuanza kujitegemea katika utoaji wa huduma za afya kwa kutumia vyanzo vya mapato vya ndani.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mtendaji wa SADC, Dk. Stegomena Tax, wakati wa ufunguzi wa mkutano wa mawaziri wanaoshughulikia sekta ya afya na Ukimwi.

Kutolewa kwa kauli hiyo kumefanyika ikiwa ni miaka michache tangu yafanyike makubaliano ya Umoja wa Mataifa (UN) kuwa kila nchi inatakiwa kutenga asilimia 15 ya bajeti yake kwa ajili ya sekta ya afya.

Dk. Tax alisema kwa kipindi kirefu, nchi za SADC zimekuwa zikitegemea wafadhili katika kuendesha miradi hiyo hasa katika sekta ya afya.

"Ili kuondoa vikwazo vilivyopo kwenye kushughulikia sekta ya afya na Ukimwi katika nchi za SADC, tunatakiwa kujiondoa kutegemea zaidi fedha za wafadhili kwa maana wakati mwingine zinakuwa kidogo na muda wa ufadhili ukiisha zinakoma, badala yake tutenge fedha za ndani kushughulikia sekta hii," Dk. Tax alisema.

Kiongozi huyo wa SADC pia alizitaka nchi wanachama kuwekeza nguvu zaidi katika ugunduzi wa mapema, hasa kwa magonjwa ya malaria na Ukimwi.

Akifungua mkutano huo, Makamu wa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, alizitaka nchi wanachama wa SADC kuboresha mifumo ya afya ili kufikia makubaliano ya kimataifa kuhusiana sekta ya afya.

# Chadema yajitoa uchaguzi wa mitaa

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimetangaza rasmi kujitoa katika uchaguzi wa serikali za mitaa, uliopangwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu kwa madai kuwa wagombea wake wengi wameenguliwa kiuonevu katika kinyang'anyiro hicho.

Kauli hiyo ya chama hicho kikuu cha upinzani nchini ilitolewa jana jijini Dodoma na Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, akieleza kuwa Chadema sasa haitasimamisha mgombea katika maeneo yote nchini kutokana na kile alichodai mizengwe inayofanywa na maofisa watendaji dhidi ya vyama vya upinzani.

Alisema wamekubaliana kutoshiriki katika uchaguzi huo baada ya kukaa na halmashauri kuu na kamati kuu ya chama hicho na kujiridhisha kuwa wagombea wa chama chao wanaundiwa mizengwe.

Alisema wagombea wachache wa chama hicho ambao fomu zao zilipokewa na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi huo na kuteuliwa kugombea, wajitoe katika kinyang'anyiro hicho.

"Kutokana na kutangaza msimamo huu, hata wale ambao fomu zao zilikataliwa kwa mizengwe, hawatakata rufaa yoyote tena," alisema.

Mbowe ambaye pia ni Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, alisema chama chake hakitawapa ushirikiano wenyeviti wote watakaochaguliwa kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika uchaguzi huo kwa kuwa chama kinaona watapatikana kupitia uchaguzi uliojawa na mizengwe.

Alisema Chadema kama chama kikuu cha upinzani nchini, kilitambua uchaguzi huo haupaswi kubezwa ndiyo maana kikajipanga na kuhakikisha kinaweka wagombea katika nafasi zote.

"Tuliwaandaa wagombea wetu na tulitimiza taratibu zote za uchaguzi ndani ya chama na tulifanikiwa kwa asilimia 85, lakini walifanyiwa mizengwe hadi kufikia asilimia 60, lakini cha kushangaza, hadi jana wagombea wetu wameenguliwa hadi kufikia asilimia tisa," alidai.

"Kutokana na hali hiyo kamati kuu na halimashauri kuu pamoja na wabunge walikaa ili kubadilishana mawazo na kuona nini kinaweza kufanyika, kwa pamoja tumeona hatuwezi kubariki masuala haya kwa kushiriki katika uchaguzi ambao demokrasia imebakwa.

"Hatuwezi kuwalaumu watendaji kwa kuwafanyia mizengwe wagombea wetu, hatuamini kama watendaji wanaweza kufanya figisu hizo viongozi wa serikali wasijue, Waziri Mkuu asijue, wala Jafo asijue!

"Hii ni hujuma na ni unafiki na sasa hii ijulikane kuwa CCM na serikali kwa ujumla wake ni waoga, haiwezekani wakawa wanajigamba kununua ndege, ujenzi wa barabara na miradi mbalimbali ya maji wakati huo wanaogopa uchaguzi," Mbowe alidai.

Kiongozi huyo wa Chadema alisema chama chake kinaona kuna haja kuwa na tume huru ambayo itakuwa inasimamia uchaguzi huo ili uwe huru na wa haki.

INAENDELEA UK. 8




Aliyekuwa Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Jamali Malinzi, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya hukumu ya kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kutakatisha fedha inayomkabili na wenzake watatu, kuahirisha hadi Novemba 21 mwaka huu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mbunge aonya mapato Jiji la Dodoma

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

MBUNGE wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Kasheku 'Musukuma', ametoa tahadhari kuhusu ongezeko la mapato katika Jiji la Dodoma huku akiishauri serikali inapaswa kubuni vyanzo vya mapato vya kudumu badala ya kuridhika na vilivyopo sasa ambavyo amesema ni vya muda.

Amesema jiji hilo kwa sasa linakuwa na mapato mengi kwa sababu linauza viwanja na majengo, hivyo linapaswa kutafuta vyanzo vya kudumu ikiwamo ujenzi wa bandari kavu itakayokuwa inapokea mizigo ya Rwanda, Burundi.

Musukuma aliyasema hayo jana bungeni mjini hapa wakati akichangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21.

"Sasa hivi tunaona mapato ni makubwa jijini Dodoma kwa sababu ya uuzaji wa viwanja na majengo. Lakini tunapaswa tubuni vitu ambavyo vitaliingizia mapato kwa miaka yote," alisema.

"Kwa mfano, tungeweza kutengeneza bandari kavu hapa Dodoma tukawa na sehemu ya kuhifadhi makontena. Mizigo yote inayokwenda Rwanda na Burundi inachukuliwa Dodoma badala ya maroli kwenda Dar es Salaam. tutakuwa tumetengeneza chanzo kikubwa cha mapato na hata reli yetu ya SGR itakuwa inashusha makontena hapa," aliongeza.

Kuhusu viwanda, Musukuma alisema inatakiwa kukutana na wamiliki walioshindwa kuviendeleza, lengo kuu likiwa ni kubaini sababu ya viwanda vingi nchini kufa.

Alisema kwa kufanya hivyo, itawezesha kupata 'dawa' ya kusaidia viwanda kuendelea na kufikia Tanzania ya viwanda inayohitajika.


Musukuma alisema mawazo ya Rais John Magufuli ya kuwanyang'anya wafanyabiashara viwanda walioshindwa kuviendeleza yalikuwa mazuri, lakini wasaidizi wake (mawaziri) wangeenda mbali zaidi kwa kuwanyang'anya wamiliki hao mawazo yao.

"Mngewaita na kuwasikiliza wawaeleze kwa nini walishindwa kuviendeleza viwanda hivyo. Nakueleza Waziri (wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango hakuna mfanyabiashara anayeweza kukopa fedha benki halafu akafungua kiwanda akakitelekeza. Huyo hayupo. lazima kutakuwa na sababu iliyomsukuma kushindwa kuendeleza kiwanda," alisema na kuongeza:

"Nikuombe tu, walioshindwa waiteni waulizeni kama

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akifanya mazungumzo na mgeni wake, Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Jaji Sylvain Ore (wa pili kulia), akiwa na Ujumbe wake wa Majaji, walipofika Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Masauni aihakikishia UNHCR kuwalinda wakimbizi

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, amefanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Shirika la Kimataifa la Wakimbizi (UNHCR), Kanda ya Mashariki, Pembe ya Afrika na Maziwa Makuu, Clementine Nkweta-Salami, na kumhakikishia ushirikiano zaidi kati ya wizara yake na shirika hilo.

Mazungumzo hayo yaliyofanyika ofisini kwa Mhandisi Masauni, jijini Dodoma jana yalijadili masuala mbalimbali ikiwamo uimarishaji wa ushirikiano hasa katika kuhakikisha wakimbizi wanalindwa na kuhudumiwa ipasavyo.

Naibu Waziri Masauni alimhakikishia Mkurugenzi huyo kuwa Tanzania itaendelea kulinda haki za wakimbizi kama ilivyokuwa ikifanya kwa miaka mingi, na pia inasimamia zoezi la kuwarejesha kwa hiari nchini kwao wakimbizi kutoka Burundi.

"Nikuhakikishie tu, Serikali ya Tanzania inawajali wakimbizi, ndio maana kwa miaka mingi inaendelea kuwahifadhi, hivyo katika kipindi hiki cha kuwarejesha nchini kwao tunahakikisha wanarudishwa wakimbizi wote kwa hiari," alisema Masauni.

Alisema mazungumzo zaidi kuhusu wakimbizi waliopo nchini yatajadiliwa zaidi na kukubaliana katika mkutano wa pande tatu unaotarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Naibu Waziri alimshukuru Mkurugenzi huyo ambaye aliambatana na Mwakilishi Mkazi wa Shirika hilo hapa nchini, Chansa Kapaya.

# Wachina 32 walipa faini mil. 591/- kukwepa jela

Distributed via ippmedia

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mkoa wa Geita imewahukumu raia wa kigeni kutoka China 32 akiwamo Mkurugenzi wa Mgodi wa Eagle Brand Limited kwenda jela miaka miwili au kulipa faini ya Sh. milioni 591.22 kwa makosa manne.

Hata hivyo, washtakiwa hao walilipa faini na kuachiwa huru.

Washitakiwa hao (32) akiwemo Mkurugenzi wa Mgodi huo walifikishwa jana Mahakamani hapo majira ya saa nne na dakika 45 asubuhi wakikabiliwa na mashtaka manne likiwamo la kuwapo nchini kinyume cha sheria, kufanya kazi na kujipatia kipato bila kuwa na kibali, kukwepa kulipa kodi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Kampuni kuajiri raia wakigeni wasio na kibali. Mkuu wa mashtaka wa serikali Mkoani Geita, Bibiaba Kileo, aliambia Mahakama hiyo kuwa washtakiwa hao walikamatwa kwenye operesheni iliyofanyika Oktoba 22, mwaka huu katika Mgodi wa Eagle Brand Limited uliopo katika kijiji cha Nyamahuna wakifanya kazi.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakma hiyo Bwegoge Obadia, akisoma hukumu hiyo alisema katika kosa la kwanza washtakiwa wa 31 wamehukumiwa kwenda jela miaka miwili au kulipa faini ya Sh. milioni 31 kila mmoja Sh. milioni moja, kosa la pili kulipa faini ya Sh. milioni 310 ambapo kila mmoja anatakiwa kulipa milioni kumi .

Katika kosa la tatu ni kulipa Sh.milioni 240 kwa kukwepa kodi ya TRA wakati katika kosa la nne Mkurugenzi wa Kampuni ya Eagle Brand Limited amehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni 10 kwa kuwaajiri wageni wasio na kibali .

Mahakama hiyo ililazimika kusimama kwa muda wa dakika kadhaa kutafuta mkalimani wa lugha ya Kichina baada ya wakili wa raia hao wa kigeni, Miyasi Samson Mashauri akisaidiana na Wakili Francis Beatus Kiganga kuiomba Mahakama kuwa na mkalimani wa lugha hiyo kutokana na raia hao kutokuwa na uwezo wa kuzungumza lugha ya Kiswahili, hivyo Mahakama hiyo kutumia Kiingereza na Kichina .

Kabla ya hukumu hiyo kutolewa, Wakili Mashauri aliambia Mahakama hiyo kuwa wateja wake wamekiri makosa hayo bila kuisumbua Mahakama na wako tayari kulipa faini hiyo. Walilipa na kuachiwa huru.

# Uhamisho hakimu wakwamisha hukumu ya Malinzi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imepiga kalenda kutoa hukumu ya kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kutakatisha fedha inayomkabili aliyekuwa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Jamal Malinzi na wenzake watatu mpaka Novemba 21, mwaka huu.

Hukumu hiyo ilipangwa kusomwa jana, lakini kwa kuwa Hakimu Mkazi, Maira Kasonde, aliyesikiliza kesi hiyo kuhamishiwa kituo kingine cha kazi.

Kesi hiyo iliahirishwa na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Kevini Mhina.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Pendo Temu, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kusikilizwa mbele ya Hakimu Kasonde, lakini upande wa Jamhuri umepata taarifa kwamba amehamishiwa kituo kingine cha kazi.

"Mheshimiwa upande wa Jamhuri tumepata taarifa kwamba Hakimu Kasonde amehamishiwa kituo kingine cha kazi tunaomba mwongozo wa mahakama," alidai Temu. Hakimu Mhina alisema ni kweli Hakimu Kasonde amepata uhamisho na taratibu za kumwezesha kuandika hukumu hiyo zimekamilika na itasomwa Novemba 21, mwaka huu.

Mapema mahakamani hapo upande wa Jamhuri uliita mashahidi 15 na vielelezo tisa kuthibitisha kesi hiyo na utetezi wanne kupangua tuhuma hizo.

Mbali na Malinzi, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni aliyekuwa Katibu wa TFF, Selestine Mwesigwa, Mhasibu wa TFF, Nsiande Mwanga na Karani Flora Rauya.

Katika kesi hiyo mashahidi 15 wa upande wa mashtaka walitoa ushahidi na tayari aliyekuwa Rais wa TFF Jamal Malinzi ameanza kujitetea mahakamani hapo.

Katika kesi hiyo ya jinai namba 213 ya mwaka 2017 washtakiwa Malinzi, Mwesigwa na Nsiande wapo rumande kwa kukabiliwa na mashtaka ya utakatishaji wa fedha kuwa miongoni mwa mashtaka ambayo kwa mujibu wa sheria hayana dhamana huku Flora akiwa nje kwa dhamana.


## TAARIFA KWA UMMA



Kampuni ya NAS-DAR AIRCO inautaarifu umma kwamba ndugu **Mikidadi Yasini** ambaye alikuwa mfanyakazi wa NAS-DAR AIRCO kitengo cha GSE (Muendesha mitambo) kwa sasa sio mfanyakazi wa Kampuni yetu na mkataba wake wa kufanya kazi ulisitishwa kuanzia Oktoba 16, 2019.

Kampuni haitohusika na utoaji wake wa taarifa kwa niaba ya Kampuni, kufanya malipo au huduma kwa niaba ya Kampuni kwani mhusika sio mfanyakazi wa NAS-DAR AIRCO.

Vyombo vya habari pamoja na umma mnataarifiwa kwamba kwa taarifa zozote zinazohusiana na kampuni ya NAS-DAR AIRCO mnakaribishwa katika ofisi zetu zilizopo Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), jengo la kuhifadhia mizigo, geti namba 6 **au** kwa mawasiliano zaidi wasiliana na:

**Idara ya Masuala ya Kampuni,**
**Kampuni ya NAS-DAR AIRCO,**
**Kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Julius Nyerere,**
**Jengo la kuhifadhia mizigo, Geti Na. 06,**
**S.L.P 18112,**
**Dar es salaam, Tanzania.**
**Simu: +255 222842218.**

nas airco

215505702

# Matokeo ya utafiti kujikinga malaria kwa 'sandoz' mbioni

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Afya Ifakara (IHI), ipo katika hatua ya mwisho ya kutoa utafiti wa namna ya kujikinga na ugonjwa wa malaria kwa kutumia viatu vya wazi 'sandoz' ambavyo mtu akivivaa hatang'atwa na mbu.

Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Dk. Honorati Masanja, aliyasema hayo jana katika mafunzo waliyoyaandaa kwa ajili ya waandishi na wahariri kuhusu utafiti wanazofanya katika sekta ya afya Tanzania, Afrika na duniani.

Pia taasisi hiyo ilielezea kuhusu programu ya Umahiri kutoka Chuo cha Mafunzo cha IHI Bagamoyo yenye lengo la kupata wataalamu watakaofanya utafiti kwa vitendo zaidi Tanzania.

Dk. Masanja alisema wameamua kufanya utafiti huo kwa sababu wamebaini mbu hupenda kuuma mtu sehemu za miguuni kutokana na harufu zinazosababishwa na uvaaji wa viatu.

"Tabia ya mbu tulivyowasoma hupenda kuuma mtu sehemu za miguu kwa sababu ya harufu zinazotoka miguuni zinazosababishwa na viatu. Taasisi yetu imeamua kufanya utafiti huu ambao umeanza miaka mitatu iliyopita na kwa sasa unakwenda ukingoni, tunatarajia hadi mwakani tutakuwa na majibu mazuri ya utafiti na nini kitafuata baada ya hapo," alisema.

Alisema utafiti huo wa kuweka dawa kwenye viatu haulengi mbu anayeambukiza malaria pekee, hata wale wanaosababisha ugonjwa wa zika na dengue kwa sababu wote wanang'ata mchana kwa kuwa usiku mtu hujifungia kwenye chandarua.

Alisema katika utafiti huo wanaangalia waweke dawa kiasi gani, urembo gani utumike ili iwe bidhaa inayovutia.

"Huu ni utafiti unaondelea na ukitupa matokeo mazuri tutaipeleka bidhaa hii sokoni."

Dk. Masanja alisema utafiti mwingine wanaoufanya ni kutengeneza mbinu za kupambana na mbu kupitia mabegi ya kawaida ambayo yatakuwa na malighafi yenye dawa.

"Kama ni mwanafunzi amekaa nje anajisomea mbu watakuwa hawamsumbui. Utafiti

INAENDELEA UK. 8

# Ufaransa kusaidia TZ kupambana na magonjwa

**Na Beatrice Shayo**

BALOZI wa Ufaransa nchini Tanzania, Frederic Clavier, amesema serikali yake imetoa kipaumbele kupambana na magonjwa makubwa nchini Tanzania ili kupunguza idadi ya vifo.

Alisema hayo katika uzinduzi wa Siku ya Afya ya Kifaransa juzi na kuungwa mkono na kampuni za Ufaransa zinazoshughulika na masuala ya afya, Sanofi na Biomerieux.

"Ningependa kuweka msisitizo katika majukwaa ya kimataifa, masuala yanayohusu afya tunayapa kipaumbele kwa Ufaransa na nchi nyingine zote za Umoja wa Ulaya," alisema Clavier.

Alisema wataangalia mikakati tofauti katika nchi jinsi asasi za kiraia zilivyojikita kwenye sekta ya afya kwa ajili ya kupunguza vifo na magonjwa makubwa, kusambaza vifaa na kutoa elimu kuhusu afya kutokana na kupewa kipaumbele cha kwanza kwa magonjwa ya milipuko duniani.

Alisema suala la kudhibiti vifo vya wajawazito wamelipa kipaumbele kutokana na kinamama kufariki wakati wa kujifungua. Alisema moja ya sababu ya vifo hivyo ni maambukizi ya magonjwa kwa wajawazito na kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukiza.

Pia, asilimia 80 ya wagonjwa kuchelewa kugundua ugonjwa na wataalamu wa afya kuwa changamoto.

Clavier alisema Serikali ya Ufaransa kwa kushirikiana na wawakilishi kutoka Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan (AKDN), wameweka kipaumbele suala la afya nchini.

Alisema mkakati wao ni kuimarisha vifaa vya kutoa huduma na mafunzo kwa wataalamu wa afya ili kusaidia jamii kuwa na uelewa wa kujua dalili za mwanzo za ugonjwa wa saratani na utafiti katika magonjwa hayo.

Katika maendeleo ya sera ya afya, alisema dhumuni lao ni kuendeleza upatikanaji wa dawa.

Meneja wa kampuni ya BioMerieux inayojihusisha na afya, Jacqueline Karachi, alisema ni muhimu kuwa na takwimu sahihi za magonjwa ili yaweze kutolewa tiba sahihi.

Alisema kuna baadhi ya wagonjwa huanza kunywa dawa kabla ya kugundua anasumbuliwa na ugonjwa gani.

"Wananchi wanajikuta wanaingia gharama kubwa kujitibu ugonjwa ambao haupo ni muhimu kufanyiwa uchunguzi na wataalamu kwa kuwa unapoendelea kunywa dawa hazifanyi kazi mwilini," alisisitiza.

Mwakilishi kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (Muhas), Dk. Siana Nkya, alisema kwa sasa wanafanya utafiti wa kupata tiba ya ugonjwa wa selimundo.

Alisema jamii nyingi hazina uelewa wa matibabu kwa mtoto ambaye anazaliwa na selimundo ingawa maisha yao hayazidi umri wa miaka mitano na kufariki.

Dk. Nkya alishauri kuanzishwa programu maalum ya kuwapima watoto wanapozaliwa ili kujua kama wamezaliwa na ugonjwa huo waanze kupatiwa tiba mapema ili iwasaidie kuongeza umri wa kuishi.



Msimamizi wa Mauzo na Masoko wa Maji ya Kilimanjaro, yanayozalishwa na kampuni ya Bonite Bottlers, Joseph Semali, akisoma jina la mmoja wa washindi wa droo ya kwanza ya maji ya Kilimanjaro, kwa wateja wakubwa na wadogo, iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana, ambapo washindi walijishindia televisheni, pikipiki na katoni 50 za maji. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Bonite yazawadia pikipiki washindi 45

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Bonite Bottlers Ltd (BBL) ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, jana imewazawadia washindi wake 45 waliojishindia pikipiki, televisheni na katoni za maji ya Kilimanjaro.

Kampuni hiyo inayozalisha vinywaji baridi yakiwamo maji ya Kilimanjaro ilichezesha droo kwanza kwa wateja wake wa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

Katika droo hiyo iliyochezeshwa jijini Dar es Salaam, jumla ya wateja 15 walishinda pikipiki kila mmoja, 15 televisheni kila mmoja na 15 wengine walishinda kila mmoja katoni 50 za maji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, muda mfupi kabla ya kuchezeshwa kwa droo hiyo, Meneja Mauzo na Masoko wa Bonite Bottlers Ltd (BBL), Christopher Loiruk, alisema, shindano hilo lilizinduliwa Oktoba 7, mwaka huu na lengo ni kuwashukuru wateja wao kwa kuendelea kutumia maji ya Kilimanjaro.

Aliema droo hiyo ya kwanza kufanyika, imehusisha kanda tano katika mikoa hiyo mitatu kulingana na mgawanyo walioweka ili shindano hilo liwanufaishe wakazi wote wa mikoa hiyo.

Alisema Kanda A inahusisha maeneo ya katikati ya Jiji la Dar es Salaam, Kariakoo, Upanga na Kigamboni; Kanda B inahusisha maeneo ya Tabata, Ilala, Mbagala, Kurasini na Mkuranga wilayani Kisarawe.

Loiruk alisema Kanda C inahusisha maeneo ya Sinza, Mwenge, Kinondoni na Tegeta, Kanda D ni maeneo ya Mbezi Beach, Mikocheni, Masaki na Kibaha na Kanda E inahusisha maeneo ya Manzese, Kimara, Makumbusho, Bagamoyo na mkoa wa Morogoro.

"Lengo la kugawa kwa kanda ni ili wateja wetu wote wanaonunua maji ya Kilimanjaro wanufaike na droo hii na kujishindia pikipiki mpya, televisheni mpya za nchi 32 na maji katoni 50 kila mmoja," alisema Loiruk.

Alieleza zaidi kuwa, lengo ni kuwapata washindi 90 wakiwamo wa watakaoshinda pikipiki 30, televisheni 30 na katoni za maji 150 kwa washindi 30.

Alisema vigezo vya kushiriki shindano hilo ni kwa kila mteja anayenunua maji kuanzia katoni 10 anapatiwa tiketi ya kushiriki droo hiyo na zinashindanishwa kwa kanda ili kuwanufaisha wateja wa maeneo yote.

Loiruk aliwataja washindi 15 wa pikipiki na maeneo wanakotoka katika mabano kuwa ni Isdory Asenga (Kibaha), Manford (Kariakoo), Zubeda Mpili (Mbagala), Ayoub Moukiwa (Uwanja wa Taifa), Gasper Urassa (Palestina), Omega Bupamba (Boko), Mary Goodluck (Dar es Salaam), Debora Njau (Kunduchi), Michael Tesha (Kinyerezi), Godlizen Sam (Masaki), Mary Shokole (Bagamoyo), Alex Mrina (Manzese), Misriya Asnee (Juwata), Sophia Omary na Juma Mbanga (Morogoro).

Washindi wengine 15 wa televisheni kuwa ni Flora Shirima (Agrey), Gabriel Kavina (Banana), Johari Mussa (Tabata), Mary Kimaro (Ilala), Geofrey (Mwananyamala), Erasmos Mwacha (Tegeta), Innocent Adelin (Sinza), Nabel Abdallah (Sinza), Yona Mwanja (Kibaha), Tarimo (Mikocheni), Suzani (Manzese), Mary Joseph (Manzese), Mary Munishi (Morogoro), Antony Chami (Soko), Varelian Mallya (Morogoro).

Washindi wengi 15 walioshinda katoni 15 za maji ni Kenan (Ungindoni), Agnes Massawe (Tabata), Erick Mroso (Kariakoo), Stellah Sanga (Tabata), Godfrey Sebastian (Sinza), Agnes Pascal (Tegeta), Praxeda Paschael (Kinyerezi), Tedi Jeimwami (Kawe), Francis Marandu (Msasani), Jason (Shekilango), Mussa omiro (Kijitonyama), Neema Roita (Mzumbe), Sera Mkasholika (Kingo), Haridy Naganga (Kihonda) na Cornelus (Msasani).

Alisema baadhi ya washindi walipigiwa simu wakati wa kuchezesha droo na wote watapigiwa na kupangiwa siku ya kukabidhiwa zawadi zao zote.

# HABARI KITAIFA



Mchuuzi wa chapati akihatarisha afya za walaji kwa kufanyia biashara jirani na rundo la takataka, katika eneo la Tandale, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **MIRAJI MSALA**

## Ujenzi barabara lami kilomita 92 waanza

**Na Sabato Kasika**

UJENZI wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Musoma Mjini hadi Busekera mkoani Mara, yenye urefu wa kilometa 92, umeanza huku ukitarajiwa kukamilika mwaka 2021.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vicent Anney, alipokuwa akizungumza jana na gazeti hili kwa njia ya simu na kufafanua kuwa hatua ya kwanza ya ujenzi ni kilometa tano.

Mkuu huyo wa wilaya alisema kilometa hizo tano zimeanzia kijiji cha Kusenyi hadi Suguti na kisha ujenzi utaendelea kuelekea Busekera na hatimaye kukamilisha kilometa zote 92.

"Tumeamua kuanza na hizo kilometa tano kwa kuzingatia kwamba kule Suguti tunajenga hospitali ya wilaya, hivyo ni muhimu barabara iwe na lami na kisha maeneo mengine yatafuatia," alisema Dk. Anney.

Alisema ujenzi wa kilometa hizo tano ulianza miezi miwili iliyopita na utaendelea kwa miezi sita na mkandarasi akikamilisha, ataanzia Suguti kwenda Busekera.

"Akishakamilisha huko, atarudi hadi Kusenyi na kuendelea kujenga kwa kiwango cha lami hadi mjini Musoma. Hapo tutakuwa tumekamilisha barabara nzima na ujenzi huo unatarajiwa kukamilika mwaka 2021," alisema.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo unafanywa na Kampuni ya Gemen Engineering na kwamba kwa taratibu za serikali umepata msamaha wa kodi kwenye mradi wa serikali.

"Ujenzi wa barabara hii ulikuwa kwenye ahadi ya Rais John Magufuli kwa wakazi wa Musoma na sasa imeanza kutekelezwa," alisema.

DK. Anney alifafanua kuwa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, akiwa kijijini Kabegi, Rais aliahidi kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Alisema upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hiyo vilifanyika na hatimaye sasa kinachoendelea ni ujenzi kwa kiwango cha lami.

Distributed via ippmedia

# Wapewa siri kufanya biashara bila vikwazo

**Na Felix Andrew**

WAZALISHAJI, wasindikaji wa bidhaa na wafanyabiashara wametakiwa kutumia fursa zinazotolewa na serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) za kuwapatia elimu ili waweze kufanya biashara bila kukukumbana na vikwazo.

Wito huo ulitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Kibondo mkoani Kigoma, Luis Bura aliyewakilishwa na Tatibu Tawala wa wilaya hiyo, Ayoub Sebabili wakati wa ufunguzi wa semina ya wazalishaji wafanyabiashara wa wilayani humo.

Bura alisema mafunzo hayo yatawawezesha kutengeneza na kuuza bidhaa zinazokidhi matakwa ya viwango na kuziongezea thamani zile zinazozalishwa kupitia mfumo wa uthibitishaji ubora.

Alisema uzalishaji wa bidhaa ni muhimu katika sekta binafsi kwani kwa kiasi kikubwa unachangia pato la taifa, kuongeza ajira na kuondoa umaskini.

"Azma ya Serikali ni kufikia malengo ya taifa kwamba ifikapo 2025 tuwe tumejenga uchumi wenye nguvu imara na wenye ushindani," alifafanua.

Alisema uongozi wa wilaya unaamini kuwa mafunzo hayo kwa wajasiriamali ni njia muafaka ya kuleta tija zaidi katika juhudi za kuliletea taifa maendeleo ya haraka kulingana na fursa hasa kwenye sekta ya viwanda. Naye Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Simon Anange, akifungua semina wilayani humo mapema wiki hii, alisema wajasiriamali wengi wilayani humo wanachangamoto ya kuanzisha vikundi bila ya kuwa na malengo yenye tija hivyo wengi hawanufaiki na vikundi hivyo.

Alisema mafunzo ambayo yameshirikisha pia maafisa kutoka afya, maendeleo ya jamii, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na maofisa biashara, imekuja wakati mwafaka ambapo Serikali imeazimia kwa dhati kuendeleza viwanda.

Anange aliwataka wajasiriamali wengi wanaochakata bidhaa mbalimbali waliopo kwenye vikundi wawekeze kwenye ardhi kwa ajili ya kufanya uchakataji huo na kuzingatia viwango.

Alisema uboreshwaji wa miundombinu kwenye barababara, reli na usafiri wa anga utaleta wageni wengi hivyo kuwataka wana Kasulu kuchangamkia fursa hizo.

Alisisitiza pia umuhimu wa wajasiriamali kuwa wabunifu kwani wengi wao wanajikita kwenye utengenezaji wa bidhaa za aina moja. Alisema uzalishaji wa bidhaa bora na salama kutoka viwandani ni muhimu ilikuwezesha zile zinazozalishwa kushindana katika masoko ya ndani, kikanda na kimataifa, hivyo semina hii ni uthibitisho wa azma ya serikali kupitia taasisi zake katika kufanikisha malengo ya Tanzania yaViwanda.

Awali Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora, Gervas Kaisi, akiwakaribisha katika semina kwa wakati tofauti wilayani Kasulu na Kibondo, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. AthumanNgenya, alisema Shirika linatambua kwamba soko la Tanzania bado lina bidhaa nyingi ambazo viwango vyake ni vya lazima lakini bado hazijathibitishwa ubora wake hivyo kuleta ushindani wa kibiashara usiosawia kwenye soko.

Alisema bidhaa zote zilizo kwenye kundi la viwango vya lazima zinapaswa kuthibitishwa ubora wake na TBS kabla ya kuzipeleka kwenye soko na kufanya kinyume na utaratibu huo ni kukiuka Sheria yaViwango Na.2 ya mwaka 2009.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni aibu kuruhusu uhalifu huu wa kilimo cha bangi

**WAKATI** zikitolewa taarifa za kupungua kwa matukio ya utumiaji, usafirishaji na uuzaji wa dawa mbalimbali za kulevya nchini, bado kuna changamoto kutokana na kasi kubwa ya ulimaji wa zao la bangi.

Taarifa za sasa zinaonyesha kuwa baadhi ya mikoa inaongoza kilimo hicho, hivyo kuashiria kuwa mapambano dhidi ya dawa za kulevya hayanabudi kujielekeza katika kudhibiti kilimo cha bangi ambacho kinachochea biashara na matumizi yake katika jamii yetu.

Serikali imesema kwamba matumizi ya dawa za kulevya aina ya bangi, bado ni tatizo nchini, huku mkoa wa Mara ukitajwa kuwa ni kinara katika kulima zao hilo ukifuatiwa na Tanga.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ndiye aliyebainisha hayo bungeni juzi, wakati akiwasilisha taarifa ya hali ya dawa za kulevya kwa mwaka 2018.

Mhagama alisema pamoja na jitihada zilizofanywa na serikali katika kupambana na dawa za kulevya nchini, bangi imeendelea kuwa tatizo kubwa nchini na kuitaja mikoa mingine inayolima kwa wingi zao hilo ni Morogoro, Arusha, Kagera na Ruvuma.

Katika kuonyesha ukubwa wa jambo hilo, Mhagama alisema kwamba kwa kipindi cha mwaka 2018 juhudi za vyombo vya dola kwa kushirikiana na wananchi zilifanikisha ukamataji wa tani 24.3 za bangi zikiwahusisha watuhumiwa 10,061.

Alisema dawa za kulevya aina ya mirungi nayo imeendelea kutumiwa na watu wa rika mbalimbali, kwamba kwa mwaka 2018 vyombo vya dola vilikamata tani 8.97 za mirungi zikiwahusisha watuhumiwa 1,186.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2018, kesi 7,592 zikiwa na watuhumiwa 10,979, zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali, kesi 7,174 zilizowahusisha watuhumiwa 11,045 ziliendelea kusikilizwa.

Sisi tunafikiri kuwa kilimo cha bangi kinaweza kukomeshwa kabisa ikiwa jamii nzima itaamua kushirikiana badala ya kuliachia Jeshi la Polisi pekee jukumu hilo.

Tunasema hivyo kwa kuwa wahusika ni wananchi wenyewe na bangi hiyo inalimwa katika mashamba ambayo yako kwenye maeneo yao, hivyo wanazo taarifa zote kuhusiana na wamiliki wa mashamba hayo pamoja na wanaoilima pamoja na kufahamu wanaivuna wakati gani na wanaipeleka wapi kuiuza.

Wananchi hawapaswi kujivua lawama hizo kwa kuwa huko nyuma tumekuwa tukishuhudia Jeshi la Polisi likienda katika maeneo mbalimbali kufyeka mashamba ya bangi na kuiharibu baada ya kupata taarifa kutoka kwa raia wema.

Mbali na ushirikiano wa jamii nzima na vyombo vya dola wa kupeana taarifa kuhusu wanaojihusisha na kilimo cha bangi, njia nyingine ni ya kukaza sheria kuhusiana na bangi.

Hapa tunamaanisha kuwa serikali inaweza kutunga sheria kali ya kudhibiti kilimo hicho kwa kuwabana kwa adhabu kali wamiliki wa mashamba ambayo yatalimwa bangi.

Pia viongozi wa serikali ngazi za vijiji, vitongoji na mitaa wapewe jukumu la ukaguzi wa mara kwa mara kwenye mashamba yanayotiliwa shaka kutumika kwa kilimo cha bangi.

Tukibaki kulalamika kuwa uzalishaji wa bangi unaongezeka na kutaja tu mikoa inayoongoza, tutakuwa hatulisaidii taifa, bali tutakuwa tunaviacha hatarini vizazi vijavyo kwa kuwa athari za bangi na dawa nyingine za kulevya tunazifahamu.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Machinga wasaidiwe kuepuka janga hili

**WAFANYABIASHARA** wadogo, maarufu kwa jina la Machinga wanafanya shughuli zao katika maeneo mbalimbali, huku mamlaka husika zikiwatafutia sehemu rasmi za biashara.

Ni sehemu wanazotakiwa kufanyia biashara zao katika masoko yaliyotengwa na manispaa au halmashauri, lakini zikiwa na huduma zote za msingi kuanzia maji, vyoo, usafiri na nyingine.

Ingawa agizo la kuboresha masoko yao ni la muda mrefu, inawezekana halijafanyika na ndiyo maana wameendelea kuwapo kando ya barabara wakiuza bidhaa zao kama kawaida.

Pamoja na kuruhusiwa kufanya biashara za katika maeneo mbalimbali na hasa kando ya barabara kama nilivyosema, angalizo kubwa ni kuhakikisha hawachafui mazingira ya maeneo yanayofanyia biashara.

Hata hivyo, angalizo linaonekana kuwa gumu kwa baadhi yao, kutokana na jinsi wanavyoendelea kuchafua mazingira kana kwamba ni jambo la kawaida kwao kukaa katika uchafu.

Mfano mmojawapo, ni wamchinga walioko eneo la Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam, ambako hivi sasa wameamua kupanga vitu vyao hadi katika mitaro na wengine kuweka mbao juu ya mitaro hiyo na kupanga biashara.

Kimsingi ni kwamba, serikali kwa kiasi kikubwa inaboresha miundombinu ya barabara jijini, ikiwamo mitaro ya kupitisha maji ya mvua, ili yasisambae mitaani na kuleta usumbufu kwa watu.

Pamoja na juhudi hizo, huenda miundombinu hiyo ikaharibika kutokana na baadhi ya wafanyabiashara kugeuza sehemu hizo za kupanga bidhaa wakisubiri wateja.

Mtindo huo nimeushuhudia eneo la Mbezi Mwisho kwa wachuuzi, wakiwamo wanaouza matunda, mboga na bidhaa nyinginezo. Wanazipanga ndani ya mitaro na muda wa kufanya biashara unapoisha, huacha taka zao mitaroni.

Kwa hali kama hiyo, ni wazi kwamba huenda ikasababisha mitaro ikaziba na kusababisha uchafuzi wa mazingira na hivyo kuwa kero kwa wengine.

Maendeleo ni muhimu kwa binadamu yoyote, lakini maisha bora hayawezi kufikiwa iwapo watu hawatakuwa na utamaduni wa kukitunza kilichopo kama, ambavyo wafanyabiashara hao wadogo wamekuwa wakifanya.

Serikali inapanua Barabara ya Morogoro, ili kupunguza foleni za magari, lakini sasa mitaro ya barabara hiyo imegeuzwa sehemu ya kupanga biashara, ambayo si salama kabisa.

Nitamke, wamachinga hawabaguliwi na ndiyo maana serikali ikaandaa vitambulisho na kuwagawia, kwa sababu inatambua shughuli zao kwenye jamii. Lakini, niwasahauri kwamba, nao wanapaswa kufika mahali wanazingatia maelekezo kwa kutochafua mazingira.

Jambo wanalotakiwa kulishika sana, ni kwamba wakati wakijengewa mazingira bora ya kufanya biashara, ni muhimu wakazingatia usafi wa mazingira, kuliko kuendelea na hali ya sasa.

Binafsi, siamini kwamba maeneo ya biashara yameisha hadi waamue kupanga bidhaa zao ndani ya mitaro, au waweke mtaroni na kupanga bidhaa.

Nadhani kuna tatizo mahali fulani, waelekezwe ili waache mtindo huo. Wapo wanaopanga bidhaa hadi kwenye hifadhi ya barabara, hali ambayo ni hatari kwa usalama na vyema wakaacha kufanya hivyo, ili kuepuka ajali za barabarani.

Ni muhimu kwa mikoa na halmashauri zote, nikiamini kila mahali waendelee kutimiza malengo ya kuweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara wadogo, kwa kutenga maeneo rasmi ya biashara.

Pia wasichague mazingira na wakati huohuo ni faida kwao ya kupuke ajali dhidi yao.

Kimsingi, Machinga hawapaswi kubughudhiwa bali kutengewa maeneo na suala hilo lilikwisha kuagizwa na Rais John Magufuli, kwamba halmashauri zote zifanye hivyo, ili wapate maeneo ya uhakika kufanyia biashara.

Wakati wakisubiri hilo, basi ni muhimu wazingatie usalama wao, pamoja na usafi wa mazingira kwa kutopanga bidhaa zao kando ya barabara na ndani ya mitaro.

Wengine huziba hata njia za waendao kwa miguu na kusababisha usumbufu, na kama nilivyosema, siamini kwamba wanakosa sehemu hadi wafanye hivyo.

Sababu inayoelezwa na baadhi yao hadi kufikia hatua hiyo, ni kutaka kupanga bidhaa mbele ya wengine, hadi wanaangukia kuiweka mitaroni, ili wawahi kupata wateja wengi na kwa haraka zaidi.

Imani ya aina hiyo ni kwamba, wakipanga biashara mbele kwa kuweka hadi mitaroni, ni namna ya kuwapata wateja wengi. Hilo halifai kabisa. Wanatakiwa kutambua kuwa hata wakiwa nyuma ya wateja, bado watawafuata huko huko waliko.

## BARUA & MJADALA

# Mtihani huu somo kwetu

**Mhariri,**

*NAJUA vijana wetu katika shule mbalimbali za kutwa, bweni, binafsi na serikali wako katika pilika za kukabili mitihani ya kuhitimu elimu ya kidato cha nne.*

*Pia kama inavyojulikana kwamba elimu ni ufunguo wa maisha na wanaokutana na mitihani ikiwamo hiyo ya kidato cha nne mingine na mingine chini ya utaratibu wa Baraza la Mitihani la Taifa (Necta), si vijana peke yao, hata wazee wenzangu nao wamo.*

*Ndio sababu tunasikia kuwapo watahiniwa wa kujitegemea na wanaofanya mitihani, katika utaratibu wa darasa la miaka miwili na kadhalika.*

*Lakini, kwa hilo ninalopenda kulizungumzia hapa ni mahsusi kwa wale vijana walioko shuleni. Wakati wa mitihani wote inajulikana kisaikolojia ni jambo la kuhofiwa, inashangaza kusikia baadhi ya wafanya mitihani wanafikia hatua mbaya ya kudhihaki kwa vitendo.*

*Huko nyuma kuna ushuhuda wa wanaokwepa kufanya mitihani na wengine wanaoandika kejeli katika karatasi ya mtihani. Ni mbaya sana na kama kusingekuwapo uthibitisho kutoka taarifa rasmi za wasimamizi, wakati mwingine ni vigumu sana kuamini.*


*Umma unapotambua na kuamini 'elimu ndiyo ufunguo wa maisha' na upande wa pili wa shilingi inakuwa, suala gumu kuamini kinachotokea. Lakini ukweli unabaki, ndiyo hali halisi.*

*Sasa walioko katika mitihani hadi sasa, ukimya huu unatupa salamu nzuri kwamba huenda kuna hatua na marekebisho ya kinidhamu yamechukua nafasi yake.*

*Na kwa maana hiyo, namna utakavyofanyika mtihani basi utakuwa mwongozo bora wa kusimamia mitihani kama kwa ufanisi au kuwapo kasoro zozote.*

**Masingeni Juma,**
**Kiparang'anda, Mkuranga.**

# Miaka minne ya Magufuli, TPA kazi yenu inaonekana




**Na Mary Geofrey**

TUKIWA tunaadhimisha miaka minne tangu Rais Dk.John Magufuli, achaguliwe na kuapishwa kuongoza serikali, yapo mambo mengi ya kujivunia.

Mbali na kuboresha huduma na uzalishaji katika sekta kama afya, elimu, barabara, kilimo na madini nchini, pia sekta ya usafirishaji kwa njia ya maji ni moja ya maeneo aliyotilia mkazo katika awamu yake ya uongozi, katika kipande hiki cha miaka mitano.

Kazi kubwa inayofanyika katika bandari zote nchini, inajumuisha kujenga magati ya kisasa kwa ajili ya meli kubwa za mizigo zitie nanga pasipo shaka, kupanua kina cha maji, kujenga ofisi na maghala ya kuhifadhi mizigo.

Serikali pia imewekeza kujenga barabara za kuingia katika maeneo yote ya bandari nchini, lengo ni kuondoa vikwazo vyote vilivyowafanya wananchi washindwe kutumia usafiri wa maji.

Mbali na miundombinu, Mamlaka ya Bandari (TPA), inayosimamia shughuli zote za bandari kwa mujibu wa sheria Namba Saba ya mwaka 2004 na kuanza kutumika mwaka 2006, ina wajibu pia wa kujenga na kununua vyombo vya usafiri majini, kama meli za kisasa na boti.

Nikiwa sehemu ya wanahabari waliopata fursa ya kutembelea miradi kadhaa ya bandari za maziwa makuu na baharini, yapo makubwa yanayofanyika usiku na mchana.

Kazi kubwa zinafanywa na Watanzania wenyewe chini ya usimamizi wa TPA, lengo ni kuinua uchumi wa watu wanaoishi pembezoni mwa maeneo yanayozunguka maziwa na bahari, pia kuwafungua fursa za kiuchumi wafanyabiashara wanaosafirisha bidhaa kwenda katika nchi mbalimbali duniani.

Kupitia shughuli zinazofanywa na bandari, mbali na kuwanufaisha walengwa wakuu Watanzania, pia miradi kuna iliyomalizika imewezesha kuipa TPA mapato ya kuendelea kupaa kila mwaka.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Deusdedit Kakoko, sasa imeshaongeza makusanyo yake kutoka Sh. bilioni 818 mwaka 2017/18 hasdi kufikia zaidi ya Sh. bilioni 900 mwaka wa fedha uliopita.

Ongezeko hilo ni zaidi ya Sh. bilioni 90 kwa kipindi cha mwaka mmoja na katika mapato hayo ya mwaka 2018/19, walitoa mrabaha serikalini zaidi ya Sh. bilioni 200.

Kakoko anasema ni mapato yanayotokana na maboresho makubwa yanayoendelea kufanywa katika bandari zote nchini, ambazo zinahudumia meli za shehena ya mizigo na abiria.

Kati ya miradi wanayotekeleza ni ile ya mikakati ya taifa ya miaka 10 na ya ndani ya TPA, ambayo inasaidia kuboresha utendaji kazi wa bandari na kuiongeza mapato.

Katika bandari ya Dar es Salaam, wanatekeleza miradi mikakati ambayo mmoja unagharimu Sh. bilioni 377 na ikikamilika itawezesha meli kubwa duniani kutia nanga na kufungua milango ya kibiashara kwa nchi jirani, kuvutiwa kupitisha shehena zao katika bandari hiyo.

Kwa mujibu Mhandisi Kakoko, gharama za miradi yote inafika Dola za Marekani bilioni 431 na kwamba bajeti ya TPA inatumia Sh. trilioni moja ya kuendeleza mradi katika bandari hiyo.

Miongoni mwa miradi mikakati inayotekelezwa na Serikali ni pamoja na ile ya ununuzi wa skana au midaki uliofanywa kwa agizo la Rais John Magufuli mwaka 2016 kwa lengo la kuimarisha usalama.

Kadhalika, daraja za juu katika makutano ya barabara, maarufu 'flyover' ujenzi wake unaendelea kwa kasi.

Pia ujenzi wa kuongeza kina katika bandari zote kubwa za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara inaendelea kuhakikisha bandari hizo zinakuwa na kina kirefu cha kupokea meli kubwa, yote ikichangia kuongeza mapato maradufu.

Katika miradi hiyo , imebahatika kuishuhudia ujenzi wake unaendelea kwa kasi isiyo ya kawaida Tanga kwa kupanua kina cha mita 17, inayogharimu Sh. bilioni 170 ambazo ni fedha za ndani ya nchi.

Miradi inayotekelezwa naTPA; ujenzi wa gati za kisasa, upanuzi wa bandari zote nchini, kujenga ofisi na maghala ya kuhifadhi mizigo, ili kufungua milango ya kibiashara na nchi jirani.

Gharama za miradi hiyo inakadiriwa kuwa zaidi ya Sh. bilioni 500 ya fedha za ndani na hufika Sh. bilioni 600 kama wakipata na fedha za nje na kwamba na asilimia 30 ya fedha hizo wanalipa mrahaba serikalini.

Haya yote yanatekelezwa na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo Mhandisi Kakoko, ambaye wakati wote amekuwa akifanya kazi usiku na mchana kuhakikisha miradi hiyo inakamilika.

Licha ya kuwa usimamizi wa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, umekuwa ukichochea mafanikio hayo lakini pia watendaji ambao ni mameneja wa bandari zote zilizobahatika kutembelea wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati.

Juhudi za watendaji wote ni ngazi ya kufanikisha juhudi kubwa zinazofanywa na serikali katika kuhakikisha uchumi wa taifa unapaa na kulinda thamani ya fedha ya mlipa kodi ambaye ni mimi na wewe, hongera TPA kazi nzuri.

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Mbunge atoa tuhuma nzito uchaguzi S/Mitaa

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

MBUNGE wa Tarime Vijijini (Chadema), John Heche, amesema Wakurugenzi wa Halmashauri na wakuu wa wilaya wamekuwa wakikutana na wasimamizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa na kuwafundisha namna ya kughushi matokeo ya uchaguzi huo. Alisema Wilaya ya Tarime mkoani Mara Mkurugenzi wa Halmashauri aliwaita wasimamizi wa uchaguzi na kukutana nao Chuo cha Ualimu baada ya kazi ya kupokea fomu kumalizika, kuanza kuwafundisha namna ya kughushi matokeo.

Aliyasema hayo jana bungeni wakati akichangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Heche alidai viongozi hao wa serikali wamekuwa wakiwafundisha watendaji ambao ndiyo wasimamizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa, namna ya kughushi matokeo ya uchaguzi huo.

"Wilaya nzima ya Maswa, siku saba, mjimbo mawili hawakuingia kazini, Tarime Mkurugenzi ameita watendaji baada ya kupokea fomu, wakakaa chuo cha ualimu," alisema Heche.

Hata hivyo, kauli hiyo ilimlazimu Mnadhimu Mkuu wa Shughuli za Serikali bungeni, Jenista Mhagama, kuomba utaratibu.

Mhagama alisema: "Nimeshindwa kuvumilia, mbunge anayechangia anataka kututhibitishia bunge hili kwamba, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wameitisha vikao na kuwafundisha watu kufanya fojari" "Tuhuma hizi ni nzito hatuwezi kukaa hapa halafu unatoa tuhuma nzito kwa viongozi wenye madaraka na serikali wanaowahudumia wananchi, kwa manufaa yako binafsi, Waziri wa Tamisemi alishatoa maelezo mazuri, kila mtu ana haki ya kupeleka tuhuma hizo katika sehemu husika, Namuomba Heche ama atoe uthibitisho wa hao wakuu wa wilaya, mikoa na wakurugenzi waliokuwa wamewafungia watu na kuwafundisha fojari, au afute kauli yake." Mhagama alisema viongozi waliotajwa na Heche wanatambulika kisheria kuhusika katika uchaguzi wa serikali za mitaa. Alisema msimamizi mkuu wa uchaguzi lazima akutane na wasimamizi wake na kuwafundisha.

Baada ya Mhagama kutoa maelezo hayo, Mwenyekiti wa Bunge, NajmaMurtaza Giga, alisimama na kusema:

"Heche nilitegemea baada ya kuzungumza hayo utatuletea uthibitisho wa kutuonesha ulichokisema, au ufute kauli yako na usiendelee kuzungumza hayo maneno, vinginevyo nitakuzuia kuzungumza." Hata hivyo, Heche alikataa kufuta kauli hiyo na kusisitiza kuwa vitendo hivyo vimetokea kweli na anao uthibitisho. "Mwenyekiti nilitegemea ungenipa muda wa kukuletea uthibitisho, lakini siyo kuniambia nitoe sasa hivi," alisema Heche.

Heche alieleza kuwa masuala ya kughushi yanayofanywa na wasimamizi wa uchaguzi wakiwafundisha na watendaji, wakianza kughushi kwenye mambo ya serikali kuanzia ngazi ya chini ikiwamo kuiba pesa za wananchi hatotegemea kuona serikali kuu ikilalamika.

Distributed via ippmedia

# Matokeo ya utafiti kujikinga malaria

INATOKA UK. 4

mwingine ni wa viti vya kukalia. Utafiti hizi zote zikikamilika na kutupa majibu chanja, zitatatua changamoto ya malaria iliyopo," alisema.

Alisema baada ya utafiti zote kukamilika na taasisi inaweza kumpa mtu ili kutengeneza vitu hivyo ili kutoa ajira kwa Watanzania.

Pia alisema wanachokingalia kwenye utafiti huo ni pamoja na madhara kama yapo ni ya muda mfupi au mrefu.

Alisema utafiti mwingine ni kutengeneza vitambaa vyenye dawa ambavyo vitawekwa kwenye eneo la nyumba linalotenganisha paa na ukuta ili kuzuia mbu kuingia ndani.

Dk. Masanja alipoulizwa utafiti huo unaoendelea kama umeshafanyika nchi nyingine duniani, alisema hafahamu lakini kwa taasisi ya Ifakara inazifanya kwa ushirikiano na nchi ya Brazil.

Kuhusu baadhi ya watu kudai dawa zinazowekwa kwenye neti zina madhara alisema hiyo ni imani tu na kuitaka jamii iondokane na dhana hiyo kwa sababu siyo kweli.

"Ili dawa iingie sokoni hufanyiwa utafiti na Shirika la Afya Duniani haliwezi kukubali dawa itumike kama hawajajiridhisha," alisema.

Aliwakumbusha Watanzania kuwa dawa zote wanazokunywa ni sumu endapo zitatumika bila kufuata utaratibu. Naye Mratibu wa Programu ya Umahiri, Dk. Dickson Lwetoijera, kutoka katika Kituo cha Mafunzo cha IHI, Bagamoyo, alisema programu hiyo ya umahiri ilianza kutolewa kuanzia mwaka 2017.

# Chadema yajitoa uchaguzi wa mitaa

INATOKA UK. 2

**ACT-WAZALENDO YAANIKA VIOJA WAGOMBEA KUKATWA**

Chama cha ACT-Wazalendo kimeeleza kufadhaishwa na kile kilichokiita hujuma dhidi ya vyama vya upinzani katika uteuzi wa wagombea wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Katibu Mkuu wa chama hicho, Dorothy Semu, alidai kuenguliwa kwa wagombea wao, kulipangwa mapema ili wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wapite bila kupingwa.

"Wagombea wetu 110,040 nchi nzima wameenguliwa, wakiwamo 2,000 ambao hata sababu za kuenguliwa kwao hazijaelezwa.

"Kuenguliwa kwa wagombea hawa na wengine kutoka vyama vya upinzani kumelenga kuhakikisha wagombea wa CCM wanapita bila kupingwa," alisema Semu.

Akifafanua zaidi kuhusu kuenguliwa kwa wagombea wa chama chake, kiongozi huyo wa ACT alidai baadhi ya wagombea wao wameambiwa hawana shughuli halali licha ya kuwa miongoni mwa walipakodi wakubwa nchini.

Alidai miongoni mwa walioenguliwa kwa kigezo hicho ni mgombea wao katika Mtaa wa Masaki jijini, ambaye jina lake limekatwa licha ya kuwa ni mfanyabiashara anayetambuliwa na Mamlaka ya Mapato (TRA) na hulipa kodi ya zaidi ya Sh. milioni 30 kwa mwaka.

Alidai kuna wagombea wao wameenguliwa kwa kuelezwa kuwa chama hicho hakipo katika orodha ya vyama vilivyosajiliwa na msajili wa vyama nchini.

Semu pia alisema kuna walioenguliwa kwa madai kuwa si wakazi wa maeneo wanayogombea licha ya kuwa na kuzaliwa katika maeneo hayo na kuwa na makazi ya kudumu na familia zao kuishi katika maeneo husika.

"Kuna hujuma pia ilifanyika kwa fomu za wagombea wetu kughushiwa na kuongezwa herufi za majina ya mgombea na hivyo mgombea kuenguliwa kwa maelezo kuwa majina yaliyotumika siyo sahihi licha ya kuwa fomu hizo zilijazwa majina sahihi," alidai.

Alisema tayari chama hicho kimeanza kuchukua hatua dhidi ya suala hilo kwa kufanya mawasiliano na vyama vingine, vikiwamo Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), National League for Democracy (NLD) na Chama cha NCCR-Mageuzi ili kuunganisha nguvu na kuchukua hatua za pamoja.

Aliongeza kuwa kamati ya chama imeitishwa kwa dharura na itakuwa na kikao leo ili kutafakari hatua za kuchukua kukabiliana na kile alichoita hujuma dhidi ya vyama vya siasa nchini.

**Imeandikwa na Paul Mabeja, DODOMA Enock Charles , Dar**

# Mbunge aonya mapato Jiji la Dodoma

INATOKA UK. 2

mlivyofanya kwa wachimbaji wa dhahabu wakawaeleza matatizo yao na leo mnaingiza mabilioni. Wafanyabiashara mkakutana nao wakaeleza upungufu wa TRA na sasa bandarini mizigo inajaa. Nikuombe waiteni hao watu walionyang'anywa viwanda, wasikilize watakueleza wapi walipokwama."

Mbunge wa Tarime Vijijini (Chadema), John Heche, alisema licha ya serikali kuleta mpango huo, kuna baadhi ya miradi ambayo ilikuwa katika mpango huo haijatekelezwa.

Alisema mradi wa Mchuchuma na Liganga tangu mwaka 2009 umeshindwa kuendelezwa.

"Mwaka 2009 serikali iliingia mkataba na kampuni moja ya China kwa ajili ya kuendeleza mradi wa Mchuchuma na Liganga. Serikali ilitakiwa kumiliki asilimia 20 na hiyo kampuni asilimia 80 na mwaka 2010 mradi ulipaswa kuanza na thamani ya mradi ni Dola za Mradi ni milioni tatu," alisema. "Mradi huo ungetoa ajira za moja kwa moja 5,000 na za muda mfupi 30,000, lakini tangu mwaka huo hadi sasa hakuna cha mradi," aliongeza.

Mbunge wa Mafinga Mjini (CCM), Cosato Chumi, alisema ili serikali ifikie uchumi wa kati ifikapo 2025 inapaswa kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vidogo ambavyo mitaji yake si mikubwa.


NGOME HOLDING GROUP

**NGOME HOLDING GROUP LIMITED**
P. O. Box 35923 Dar es salaam Tanzania
Tel: +255 739999798 Fax: +255 739999798
Email: ngomeholdinggroupltd@gmail.com

**TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA TATU WA WANAHISA WA NGOME HOLDING GROUP LIMITED IJUMAA TAREHE 29/11/2019**

Mwenyekiti wa bodi ya **NGOME HOLDING GROUP LIMITED** anatangaza Mkutano Mkuu wa tatu wa wanahisa wa NGOME HOLDING GROUP LIMITED utakaofanyika ukumbi wa mikutano uliopo jengo la Ngome Holding House, Sinza Afrikasana tarehe 29 Novemba 2019 kuanzia saa 4.00 asubuhi

**AGENDA**

1. Kufungua Mkutano
2. Elimu ya usimamizi bora wa kampuni tanzu
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa mkutano mkuu wa mwaka 2018
4. Kujadili yatokanayo na muhtasari wa mkutano mkuu wa mwaka 2018
5. Kupokea na kujadili taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi
6. Kupokea hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2018
7. Kuwasilisha mapendekezo ya mapato na matumizi kwa mwaka 2020
8. Pendekezo la gawio kwa wanahisa kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Desemba, 2018
9. Kuteua mkaguzi wa hesabu za kampuni kwa mwaka 2019
10. Kujadili pendekezo la Ngome Holding Group Limited kumilikiwa na kuendeshwa kwa asilimia 100 na Ngome SACCOS Limited
11. Kupanga tarehe ya mkutano ujao
12. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
13. Kufunga kikao

**NB:**

1. Wanahisa watakaohudhuria mkutano huo watajitegemea.
2. Wanahisa watakaohudhuria mkutano huo wanatakiwa kuja na vyeti vyao vya hisa na kitambulisho. Kwa wale ambao watawakilishwa, waje na barua ya utambulisho na cheti cha hisa cha anayewakilishwa.
3. Wanahisa wanaombwa kuthibitisha ushiriki wao kwa barua pepe; ngomeholdinggroupltd@gmail.com au kwa simu namba 0686191875, 0765006055 na 0713332780
4. Kwa wale watakaokuwa na mengineyo wawasilishe kwa katibu wa bodi kupitia barua pepe; ngomeholdinggroupltd@gmail.com au kwa simu namba **0686191875, 0765006055 na 0713332780**

Imetolewa kwa niaba ya

Bodi ya Wakurugenzi wa NGOME HOLDING GROUP LIMITED

CR Yateri, Ndc
Brigadier General (rtd)
Chairman

215508102

# Mgogoro ardhi wananchi, mwekezaji waibuka upya

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MGOGORO wa mpaka kati ya mwekezaji wa shamba la Mpunga la Kapunga na wananchi wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, umeibuka upya, baada ya kuwekwa kwa mpaka mpya wa shamba hilo ambao umezingira nyumba zaidi ya 150 za wananchi pamoja na Shule ya Msingi Iyalla B ambazo zinatakiwa kuvunjwa ili eneo hilo liwe sehemu ya shamba.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi kijijini hapo, wananchi hao walisema hatua hiyo ya uwekwaji wa mpaka mpya wa shamba la Kapunga, unafufua mgogoro ambao serikali ya awamu ya tano ilikuwa ilishautatua tangu mwaka 2016.

Mmoja wa wananchi hao, Emily Edward alisema kuwa mpaka mpya wa shamba hilo umeingia kwenye makazi ya wananchi pamoja na kumega baadhi ya majengo ya Shule ya Msingi Iyalla B, ambayo ilijengwa kwa nguvu za wananchi, jambo ambalo linaonyesha kuwa mwekezaji huyo hajali maendeleo ya wananchi.

"Tumeona mpaka mpya umewekwa kwa kutumia magreda, mahali ulipopita mpaka huo umezingira nyumba zaidi ya 150 za makazi ya wananchi, lakini hata shule yetu ya Iyalla B nayo imemegwa, hivyo tunashindwa kuelewa dhamira ya mwekezaji kama kweli anajali maendeleo yetu," alisema Edward.

Naye Manyanya Matabhe, alisema kuwa mpaka huo umewekwa kinyemela bila kushirikisha wakazi wa eneo hilo kwa lengo la kudhulumu ardhi ya wananchi wanyonge wanaitumia kwa kilimo na makazi.

"Mpaka huu uliwekwa kinyemela, wananchi waliamka asubuhi wakakuta tayari mpaka umewekwa bila ya wao kushirikishwa, hii inaonyesha kuwa dhamira yao ni kuwadhulumu wananchi wanyonge ardhi yao," alisema Matabhe.

Mwenyekiti mstaafu wa Kijiji cha Kapunga, Ramadhan Nyoni, alisema Serikali ya sasa ilipoingia madarakani ilishughulikia mgogoro huo ambapo Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, aliamuru hekta 1,800 zimegwe kutoka kwenye shamba la mwekezaji na kurejeshwa kwa wananchi.

Alisema serikali ilitoa uamuzi huo baada ya kubaini kuwa mwekezaji huyo alipatiwa kimakosa baada ya hati yake kukosewa kwa kuongezewa maeneo ambayo alikuwa hastahili kuyamiliki.

Alisema tangu shamba hilo linakabidhiwa kwa mwekezaji, lilikuwa na ukubwa wa hekta 5,500, lakini mwekezaji alivyoandikiwa mkataba wake ilikuwa ni hekta 7,370, jambo ambalo lilisababisha wananchi wa kijiji cha Kapunga kunyanyaswa kwa kuondolewa kwenye maeneo yao.

Nyoni alisema Serikali Kuu iliamua imfidie mwekezaji huyo ardhi yake katika eneo la Kihansi, lakini baadhi ya viongozi wa Wilaya ya Mbarali wakataka wamfidie mwekezaji ardhi hiyo

INAENDELEA UK. 24


Distributed via ippmedia

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe (kushoto), na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi wa Malawi, Ralph Jooma, wakibadilishana makubaliano ya ushirikiano waliosaini, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuimarisha biashara na uhusiano wa kijamii kati ya nchi hizo mbili, kwa kutumia miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam, barabara pamoja na safari za ndege za ATCL. **PICHA: WUUM**

# Mtumishi matatani kwa tuhuma kughushi cheti

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

TASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(TAKUKURU) mkoa wa Katavi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Mkoa, wanatarajia kumfikisha mahakamani mtumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda kwa makosa ya kughushi na kutoa nyaraka za uongo.

Kwa mujibu wa Takukuru, kosa hilo ni kinyume cha vifungu namba 333, 335, 337, na 342 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu sura ya 16 ya mwaka 2002.

Mkuu wa Takukuru wa Mkoa wa Katavi, Christopher Nakua, alimtaja mtumishi huyo ni Deodatus Jabily (46), mkazi wa mtaa wa Nsemulwa Manispaa ya Mpanda, ambaye ni dereva wa halmashauri hiyo.

Alisema mtuhumiwa atafikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Katavi kwa tuhuma ya kughushi cheti cha udereva kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kilichoko jijini Dares Salaam na kukiwasilisha kwa mwajiri wake, huku akijua sio cheti halisi na akiwa anajua hakusoma katika chuo hicho.

Alisema Jabily aliwasilisha cheti hicho kwa mwajiri wake ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, na kuwa mwaka 2009 mtuhumiwa alifanikiwa kupata ajira kwa kutumia nyaraka hiyo iliyoghushiwa kinyume cha sheria.

Aliwaonya watumishi wa umma na jamii kwa ujumla kutojihusisha na vitendo vya jinai ikiwamo kama kuwasilisha nyaraka za uongo ili kujipatia ajira au manufaa yoyote ambayo ni kinyume cha sheria.

# Neema ya umeme sasa yaifikia shule

**Na Mwandishi Wetu,** KISARAWE

SIKU chache baada ya Tanesco kusambaza nguzo katika eneo la Gumba liliko karibu na Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Christon, Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, jana aliwataka wakazi wa eneo hilo kushirikiana kikamilifu na wafanyakazi wa Tanesco wanaotekeleza mradi wa kusambaza umeme katika eneo lao.

Katika ziara ya kutembelea eneo hilo na shule kujionea tatizo la umeme lilivyo, Jokate, alipewa maelezo na wataalamu wa Tanesco ambao waliahidi kutatua tatizo la umeme katika eneo hilo ili kutekeleza azma ya serikali ya kusambaza umeme vijijini kwa kadri inavyowezekana. "Umeme ni nyenzo muhimu katika kuinua taaluma na pia huongeza fursa za kiuwekezaji. Umeme wa uhakika utaifanya wilaya yetu kuwa katika nafasi nzuri kitaaluma na kiuchumi. Nawashukuru sana wataalamu wa Tanesco kwa namna ambavyo mmejipanga kutekeleza mradi huu utakaosukuma maendeleo eneo hili kwa haraka," alisema Jokate na kuongeza kwamba itakuwa vizuri mradi huo ukiisha kabla ya mwaka huu.

Jokate aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano wakati wa zoezi hilo linalotarajiwa kuanza Jumatatu ili kuharakisha upatikanaji wa umeme wa uhakika na kwa gharama nafuu.

"Nawaomba wananchi kushirikiana na wataalamu wa Tanesco ili kuharakisha upatikanaji wa umeme ambao ni muhimu sana katika kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi ikiwamo ujenzi wa viwanda vya kati na vikubwa," alisema.

Mkuu wa Shule, August Minja, aliishukuru serikali na Tanesco kwa kuupa mradi huo msukumo na kueleza kwamba utaiondolea shule yao tatizo la ukosefu wa umeme wa uhakika na wa gharama nafuu.

"Kukamilika kwa mradi huu kutaleta nafuu kubwa kwa shule kwa kuwa tumekuwa tukitumia gharama kubwa katika kuendesha majenereta kama chanzo cha nishati ya umeme," alisema Minja.

Juma Maulidi, mwanafunzi wa kidato cha tatu, alisema umeme wa gridi utawaongezea wanafunzi ari ya kujifunza kwa bidii.

"Umeme wa uhakika utakuwa ni motisha katika masomo yetu. Sasa hivi tunapata wakati mgumu sana hususani nyakati za usiku kwani umeme wa generta hauaminiki. Umeme wa gridi utazidi kuiweka wilaya yetu katika nafasi nzuri kitaaluma," alisema.

# Sheria kubana wapangishaji wa nyumba yanukia kutua bungeni

SERIKALI imesema itapeleka kanuni bungeni kwa ajili ya kuwabana wamiliki wa nyumba wanaowalazimisha wapangaji wao kulipa kodi kwa kipindi cha miezi sita hadi mwaka mmoja.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, aliyasema hayo jana wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mtama (CCM), Nape Nnauye, aliyekuwa anataka majibu ya serikali kuhusu wapangaji kulazimishwa kulipa kodi kuanzia miezi sita.

Nape alisema: "Waajiriwa wapya haswa wale wa kipato cha chini wanashindwa kumudu makazi bora katika mazingira kuwa wamiliki wengi wa nyumba wanataka kodi ya miezi sita hadi mwaka mzima, jambo ambalo watumishi hawa hawawezi kumudu, hivyo kujihusisha na vitendo vya rushwa ili wapate pesa za kulipia kodi."

"Sasa serikali haioni imefika wakati wa kuleta sheria bungeni itakayowalazimisha wamiliki wa nyumba kudai kodi ya zaidi ya mwezi mmoja?" Alihoji Nnauye.

Akijibu, Lukuvu alisema ni kweli jambo hilo linaleta kero sana na wizara imeshatoa ufafanuzi kadhaa.

Alisema kwa mujibu wa sera, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi anaweza kutoa maelekezo fulani au kuweka kanuni kuweza kutawala masuala ya makazi.

Alisema alishawahi kutangaza na kupiga marufuku utaratibu huo kwa sababu siyo wa kiungwana wala kisheria.

"Ni kweli watu wanalazimisha wapangaji kulipa miezi 12, si vijana wanaoanza kazi tu, hata wanafunzi wanaokaa katika hosteli wanalazimishwa kulipa miezi 12.

Hili jambo halikubaliki hata kidogo, serikali haitaingilia gharama ya upangishaji kwa sababu upangishaji ni makubaliano.

Ingawa ipo katika utaratibu wa kuweka Regulatory Authority (mamlaka ya uthibiti) ambayo itaangalia viwango vyenyewe vya upangishaji ili kulinda haki za wenye nyumba na wapangaji," alisema Lukuvi.

Alisema katika suala la kuwalazimisha wapangaji kulipa kodi ya miezi12 au sita halikubaliki.

Awali Mbunge wa Viti Maalum, Mary Muro (CCM), alihoji ni kwa nini nyumba zilizojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) , zimekosa wanunuaji, je, serikali itapunguza bei ili ziweze kupata wanunuaji?

Kwa kujenga nyumba nyingi vile serikali haioni inapoteza fedha za wavuja jasho?" Aliuliza.

Akijibu, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, alisema hakuna nyumba ya shirika hilo ambayo imekosa wateja, na kwamba nyumba ambazo hazijapangishwa hazizidi asilimia mbili.



Distributed via ippmedia

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, akieleza kuongezeka kwa wigo na fursa za upatikanaji wa huduma za fedha kwa wananchi unaotokana na Mpango Mkuu wa Taifa wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2019/2020 hadi 2029/2030, katika kikao kilichofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: WFM**

## 'Pilipili manga ni kipaumbele'

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema pilipili manga ni miongoni mwa mazao ya bustani yanayoendelea kupewa umuhimu wa kuzalishwa nchini kutokana na mahitaji yake kama kiungo na dawa za binadamu.

Bashe aliyasema hayo wakati alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Muheza (CCM), Balozi, Adadi Rajabu, ambaye alitaka kujua mpango wa serikali wa kutuma wataalamu kubaini ni kwa nini zao hilo limeshuka thamani.

Pia alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima hao ili waweze kulima kilimo cha kisasa.

"Wananchi wa Tarafa ya Amani wamelima zao la pilipili manga kwa wingi, hivi karibuni bei ya zao hilo imeanguka sana kutoka Sh.12,000 hadi Sh. 4,000, jambo linalowaumiza sana wakulima," alisema Rajabu.

Bashe alisema pilipili manga ni miongoni mwa mazao ya bustani yanayoendelea kupewa umuhimu wa kuzalishwa nchini

kutokana na mahitaji yake kama kiungo na dawa za binadamu.

Alisema, kutokana na umuhimu huo, Machi 2019, serikali ilituma wataalamu kufanya tathmini ya hali ya uzalishaji wa mazao ya viungo ikiwamo pilipili manga kwenye Halmashauri za Wilaya ya Muheza na Morogoro.

"Tathmini ilibaini kwamba bei ya pilipili manga imeshuka kutoka Sh. 13,000 kwa kilo mwaka 2017 hadi Sh. 4,500 kwa kilo katika mwaka 2019 sawa na asilimia 20 kutokana na ongezeko la uzalishaji kwa zao hili nchini pamoja na nchi wazalishaji wakubwa ambao ni Vietnam, Indonesia, Srilanka, Brazili na India," alisema Bashe. Alisema uzalishaji wa ndani wa zao hilo uliongezeka kutoka tani 7,836.40 mwaka 2014/2015 hadi tani 12,318.3 mwaka 2017/2018.

Alisema uzalishaji duniani kwa mwaka 2017 ulifikia tani 725,000 ikilinganishwa na mahitaji yanayokadiriwa kuwa tani 400,000 kwa mwaka.

## Waliochangia ujenzi wa Taifa kuenziwa

SERIKALI imesema moja ya vipaumbele vyake ni kuhakikisha inawaenzi watu wote ambao wamechangia kwa namna moja au nyingine katika ukombozi wa Tanzania na ujenzi wa Taifa.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Musa Sima, aliyasema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum CCM, Fakharia Shomar Khamis.

Katika swali lake, Fakharia alisema kwa kuwa Muungano ni tunu na tunahitaji kuwatunza wazee wanne walioshiriki kuchanganya mchanga wa Muungano baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

"Je, serikali inawaangalia vipi wazee wetu hao wanne kwa kuwapa asante baada ya utu uzima kuwafikia. Wakati wa sherehe za Muungano, wazee hao hufikishwa kwenye sherehe, Je, huko ndiko kuonyesha serikali inawatunza?" Alihoji Fakharia.


Akijibu, Sima alisema serikali inatambua michango ya watu mbalimbali walioshiriki katika ukombozi wa Tanzania na ujenzi wa Taifa ikiwa ni pamoja wazee walioshiriki katika tukio la kuchanganya udongo Aprili 26, 1964.

"Kundi hili ni moja kati ya makundi mengi yaliyotoa mchango wa hali na mali katika kulijenga Taifa hili ikiwamo wastaafu na walioshiriki katika vita vya Kagera," alisema Sima.

Alisema kwa sasa hakuna sheria mahsusi ya asante au malipo kwa watu waliofanya mambo makubwa yanayojenga historia ya nchi.

"Kuwashirikisha wazee hawa katika maadhimisho ya sherehe za Muungano ni sehemu ya kutambua mchango wao na kukumbuka tukio muhimu la uchanganyaji wa udongo wa Tanganyika na Zanzibar. Ushiriki wao huwezeshwa na Ofisi ya Makamu wa Rais," alisema Sima.

Alisema pamoja na wazee hao, yapo makundi mengine ya wazee ambao kwa namna moja au nyingine walitoa mchango wao katika ujenzi wa Taifa ambao pia hualikwa kushiriki katika maadhimisho hayo mfano viongozi wastaafu na wanasiasa wakongwe.




**Habari zote na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

# CCM yapita bila kupingwa vijiji 54 kati ya 56 Simanjiro

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WAGOMBEA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wamepita bila kupingwa kwenye vijiji 54 kati ya 56 na vitongoji 254 kati ya 278 wilayani Simanjiro mkoani Manyara.

Msimamizi wa Uchaguzi wa wilaya hiyo, Dk. Salehe Masaza, alisema jana kuwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimeweka wagombea kwenye vijiji viwili na vitongoji 24.

Dk. Masaza alisema nafasi 1,430, zikiwamo za wajumbe wa serikali za vijiji 648 na wajumbe wa viti maalum wanawake 448, zinagombewa na vyama vya siasa. "Bado tupo kwenye mchakato wa kupitia majina ili kubaini wagombea walioteuliwa au ambao hawakuteuliwa, baadaye nitakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kukupa taarifa juu ya hilo," alisema. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Kata ya Orkesumet, Edmund Tibiita, alisema wagombea wa CCM wamepita bila kupingwa kwenye eneo hilo. Katibu wa Chadema mkoani Manyara, Gervas Sulle, alisema wako kwenye wakati mgumu wa kufanya uchaguzi kwa kuwa wagombea wao wengi wamekatwa. "Nadhani kwenye eneo la Mbulu ni sawa na kwamba hakuna uchaguzi, kama ni wagombea sijui wapo watano au sita, wengine hawakuteuliwa," Sulle alisema.



Mamalishe maarufu mama Neema, akifanya maandalizi ya kuwapikia chakula wateja wake katika eneo la stendi ndogo ya jijini Arusha jana.
**PICHA: WOINDE SHIZZA**

# CRDB yapongezwa kuwajali wazawa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, ameipongeza Benki ya CRDB kwa kuwapa nafasi ya uongozi wa juu katika benki hiyo Watanzania, tofauti na benki zingine.

Aliyasema hayo jana jijini alipofungua kongamano la 'Pamoja Nawe Kukuza Uchumi', lililokutanisha wadau wa benki hiyo Kanda ya Kaskazini.

Alisema benki hiyo imekuwa mstari wa mbele kuonyesha Watanzania wanaweza katika masuala ya uongozi.

"Benki hii imeonyesha njia benki zingine zinazotoa nafasi hizo kwa raia wa kigeni kwa kuwapa nafasi wazawa katika nafasi kubwa na wameonyesha wanaweza sababu benki imepiga hatua kila nyanja na inazidi kukua," alisifu.

Gambo alisema CRDB wametambua umuhimu wa kutumia vipaji vya wazawa katika kutekeleza miradi ya maendeleo na kuiendesha benki hiyo.

Alisema wanachofanya CRDB ni kuendeleza falsafa ya Rais John Magufuli ya kusaidia wananchi wanyonge kwa kuanza kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo bila masharti magumu na kutoa kipaumbele kwa wazawa.

Mkurugenzi wa Wateja wa Kati na Wadogo wa benki hiyo, Boma Raballa, alisema wameamua kutoa semina kwa wateja wao toka Kanda ya Kaskazini ili wafahamu fursa zilizopo benki na kuzitumia kuboresha biashara zao.

Alisema benki hiyo kwa sasa imejipanga kuinua Watanzania kwa kutoa mikopo yenye riba nafuu na isiyo na riba kwa wajasiriamali wenye vitambulisho vya Rais Magufuli.

"Sisi CRDB tumeona tuwezeshe wateja wetu katika kuwainua kwenye mitaji yao ya biashara kutokana na kutufanikisha kupata maendeleo katika benki yetu," alisema.

Alitaja baadhi ya mafanikio waliyonayo kuwa ni kufungua mashine za kielektroniki za ATM 550 na kufungua matawi 266 Tanzania nzima.

## 12,000 wanufaika na mradi wa maji

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

ZAIDI ya wakazi 12,000 wa Kata ya Ayalagaya, Halmashauri ya Babati mkoani Manyara, wamenufaika na mradi wa maji uliojengwa na Shirika la Kalimu International kwa Sh. milioni 600.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ayalagaya, Onesmo Lohay, akitoa taarifa ya mradi huo kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, alisema mradi huo utakuwa mkombozi kwa vijiji vya kata hiyo na kusaidia kutatua kero ya maji iliyokuwapo kwa muda mrefu.

Lohay alisema mradi huo umegharimu zaidi ya Sh. milioni 600, wananchi wakichangia Sh. milioni 60 kufanikisha ujenzi wake.


Akihutubia wananchi, Mnyeti aliwapongeza wafadhili wa mradi huo kwa niaba ya serikali na kuwataka viongozi wa halmashauri kuhakikisha wahisani hao wanafika ofisini kwake ili kuwapa pongezi rasmi.

Mnyeti aliwataka wananchi wanaonufaika na mradi huo kuutunza na kutunza vyanzo vya maji vinavyouzunguka ili mradi uendelee kuwanufaisha.

"Msiharibu miundombinu ya mradi huu kwa kuwa tumesaidiwa na wafadhili na wafadhili wanakuja na kuondoka, hivyo tunzeni mradi, hata ambao hawajapata waje wapate," aliagiza.

Mhandisi wa Wakala wa Maji wa Halmashauri ya Babati, Welansari Mnisi, alisema mradi huo unatoa maji lita 360,000 kwa saa na chanzo cha maji kiko karibu nao.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Asha Juma, akizungumza na Nipashe, alisema mradi huo umewasaidia kuondokana na kero ya maji iliyokuwapo kwa muda mrefu.



# Wakerwa watoto kulala mabarazani

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

KUONGEZEKA kwa watoto wanaozurura mitaani na kulala barazani nyakati za usiku katika mji mdogo wa Sanya Juu, Wilaya ya Siha kumeanza kuibua maswali, huku baadhi ya viongozi wa dini wakitaka watendaji ngazi za kata na vijiji kuendesha msako wa kuwakamata wazazi ambao watoto wao hawalali nyumbani.

Katibu wa Msikiti wa Khalid Al Araimi wilayani Siha, Iddi Hamisi, alisema jana kuwa mji huo umejaa watoto wenye umri wa kwenda shuleni, ambao huonekana wakizurura mchana na usiku kwenye baa, kukaa kwenye vibanda vya kuonyesha sinema na kulala nje ya maduka ya watu.

Hamisi alisema hayo wakati wa ufunguzi wa msikiti wa kisasa wa Khalid Al Araimi uliojengwa na waumini wa Kiislamu kwa zaidi ya Sh. milioni 100. "Niiombe serikali kwa sababu najua iko makini, ni vyema ikawasukuma watendaji wa kata na vijiji kuwafuatilia watoto wote wenye umri wa kwenda shuleni wanaozurura mitaani ili wawapeleke kwa wazazi wao na ikiwezekana wachukuliwe hatua kwa uzembe," alisema.

Akieleza wanavyochukizwa na hali hiyo, Hamisi alisema haiwezekani serikali ikatumia fedha nyingi kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bure, kuanzia shule ya msingi hadi sekondari halafu baadhi ya wazazi wanashindwa kutimiza wajibu wao kwa kuwaandikisha watoto shule.

Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Sanya Juu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutherti Tanzania (KKKT), Dk. Deameny Lyamuya, alishauri wazazi kuwalea watoto wao katika maadili mema.

Alisema hata Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, imeeleza wazi juu ya wajibu wa mzazi na adhabu itakayotolewa na mahakama inapojiridhisha kuhusu kosa.

"Kwa muda mrefu limekuwa kama jambo la kawaida kuona watoto wadogo wa kuanzia umri ya kwenda shuleni wakiwa kandokando ya barabara wakiomba msaada wa fedha kwa watu mbalimbali wakiwamo madereva wa magari na wapita njia," alisema.

Mchungaji Lyamuya alisema serikali ina jukumu la msingi la kuhakikisha ulinzi na usalama kwa watoto hao unapatikana pamoja na kushirikisha jamii kuwasaidia na kuwaokoa vijana wanaoishi katika mazingira hatarishi wakiwamo watoto wa mtaani.



Wafanyakazi wa Kiwanda cha African Please, kilichopo Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, wakiandaa maharage mabichi maarufu kama 'Green Beans', kiwandani hapo, juzi, tayari kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi na mengine kutumika hapa nchini. **PICHA: DIXON BUSAGAGA**

# Sababu kuengua wapinzani zatajwa

**Na Paul William,** MOSHI

WAKATI vyama vya upinzani nchini, vikilia kuhusu rafu kwa wagombea wao kuenguliwa katika uchukuaji na urejeshaji wa fomu kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa, Msimamizi wa Uchaguzi wa Manispaa ya Moshi, Selina Masenga, amezitaja sababu zilizotumika kuwaondoa.

Masenga alitoa ufafanuzi huo jana, baada ya kuulizwa na Nipashe kuhusu taarifa za kuwapo kwa wagombea 42 wa uenyekiti wa Serikali za Mitaa katika Jimbo la Moshi Mjini ambao wamewekewa pingamizi.

Alizitaja sababu hizo kuwa pamoja na baadhi ya wagombea kutojua kusoma na kuandika, kushindwa kuzingatia masharti wakati wa ujazaji wa fomu, kukosea kujaza majina yao na kutojazwa kwa usahihi tarehe ya kukabidhiwa kadi ya uanachama.

"Jamani kuna makosa ya wazi ambayo baadhi ya wagombea wameyafanya wakati wa ujazaji wa fomu zao. Kwa mfano zipo kanuni mbalimbali za uchaguzi ambazo wagombea waliopitishwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), walishindwa kuzizingatia wakati wa ujazaji wa fomu za kugombea na kusababisha kuwekewa pingamizi," alisema.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, makosa yote hayo ni kinyume na kanuni za uchaguzi, kanuni ya 16 kifungu kidogo cha 1 (d), yaliyoainishwa katika ukurasa wa 50.

"Kanuni hii imeeleza wazi kuwa mgombea yeyote ili akikidhi kigezo hiki, jina lake alilojaza katika fomu ya kuomba kugombea linatakiwa kuonekana katika daftari la kupigia kura. Wako baadhi ya wagombea, hawakutimiza sifa hiyo," alisema.

Ofisa huyo alisema baadhi ya wagombea majina yaliyoandikwa kwenye fomu yametofautiana na yale yaliyoandikwa katika daftari la kupigia kura.

Pia alisema baadhi ya wagombea waliopoteza sifa kutokana na kutojua kusoma na kuandika, wameenguliwa kwa mujibu wa kanuni ya 15, kifungu kidogo (c), ukurasa wa 49 wa kanuni za uchaguzi.

Sababu zingine zilizosababisha wagombea hao kupoteza sifa ni wagombea kujaza fomu wakati fomu hizo zimejieleza kuwa mgombea anapaswa kujaza fomu mwenyewe.

"Wagombea walio wengi wameshindwa kujaza kwa usahihi, nafasi wanazoomba kama ambavyo mwongozo wa uchaguzi wa serikali za mitaa, kifungu cha 11 (e) kinataka. Wengine wamekosea tarehe ya kuzaliwa, kwa mfano yuko mgombea ameandika amezaliwa mwaka 2019, hivyo hajakidhi kanuni za umri wa kugombea," alisema.

Pia alisema baadhi ya wagombea walijidhamini, hivyo kukiuka masharti ya kifungu cha 14, kifungu kidogo cha 2 (a), ambacho kinaelekeza mgombea kuidhinishwa na chama chake na si kujiidhinisha.

"Hata saini za baadhi ya wagombea zilizomo kwenye fomu zinatofautiana na zilizomo kwenye daftari la kupigia kura pamoja na ile ya mgombea kutokuwa na maslahi katika taasisi iliyo na ubia na serikali," alisema.

# Taasisi yalaani wanaume kutelekeza watoto

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TAASISI ya Miembeni Action and Passion for People with Disability, imelaani utamaduni unaoendelea kutukuzwa na baadhi ya wanaume katika Manispaa ya Moshi wa kutelekeza familia baada ya kuzaliwa mtoto mwenye ulemavu.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Hussein Msacky, alisema jana kuwa kwa mujibu wa utafiti walioufanya, umebaini asilimia 95 ya wanaume katika eneo hilo, huzitelekeza familia zao pindi wanapozaa mtoto mwenye ulemavu, hivyo kubaki wakilelewa na mama peke yake.

Alikuwa akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum kuhusu ushiriki wa watu wenye ulemavu katika uchaguzi wa masuala ya kijamii kama uchaguzi ujao wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu, nchini kote.

"Imani potofu na vitendo vya baadhi ya wanaume katika Manispaa ya Moshi, kuzitelekeza familia zao kwa sababu ya kuzaa mtoto mwenye ulemavu, limekuwa tatizo kubwa.

"Katika utafiti wetu tumebaini kuwa mama anapojifungua mtoto mwenye ulemavu, mwanaume huikimbia familia na wengine huwapa majukumu ya kuwalea watoto wenye ulemavu bibi zao ambao wana umri mkubwa," alisema.

Alisema tatizo hilo bado linaendelea kukwamisha ustawi wa jamii, hasa kundi la watu wenye ulemavu, ambao kama watapatiwa elimu kama ilivyo kwa watoto wengine, wana nafasi kubwa ya kushiriki shughuli za maendeleo.

Kuhusu vikwazo vya kielimu ambavyo watoto wenye ulemavu katika shule za Tanzania wanakumbana navyo na kushindwa kuendelea na masomo yao, Msacky alivitaja kuwa ni mpango mbovu wa ujenzi wa majengo ya shule, ambayo hayawapi fursa watoto wenye ulemavu kuyatumia hasa wale wenye ulemavu wa macho na viungo.

Jambo la pili ni uelewa mdogo na kutothamini mambo yanayowahusu watu wenye ulemavu miongoni mwa walimu, viongozi wa shule na jamii kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Msacky, mambo yote hayo yana madhara pindi linapokuja suala la kutambua na kuthamini mahitaji ya kielimu kwa watoto wenye ulemavu.

Aidha, alitaja tatizo la wazazi wengi kutokuwa tayari kuwaandikisha watoto wenye ulemavu katika shule, jambo ambalo alisema linasababisha kiwango cha uandikishaji kwa watoto wenye ulemavu kubaki kikiwa chini.

Kikwazo kingine ni ukosefu wa mafunzo kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu na elimu jumuishi.

Mkurugenzi huyo alisema hali hiyo inachangiwa na kutotekelezwa kwa vitendo, sera ya serikali inayohusu elimu jumuishi ambayo ingetoa fursa zaidi za kielimu kwa watoto wenye ulemavu.

Alisema limo pia tatizo kwa shule nyingi hazina sifa za kufundisha watoto wenye ulemavu kutokana na ukosefu wa vifaa muhimu na matini yanayofaa kufanikisha tendo la ujifunzaji kwa watoto wenye ulemavu.



Ukurasa 19

Vanilla inapoongezeka zao la matumaini kwa wakulima



Ukurasa 14

'Mkaa Endelevu' unavyowaibua kimaendeleo wakazi wa Kilosa


# BUFE

Ijumaa Novemba 8, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 15

## Mwanamitindo Odemba kumtua mama ndoo

Distributed via ippmedia



# Jaji Mihayo: Niliikuta TTB hoi, madeni na akaunti, sasa walau inatazamika

**Na Beatrice Philemon**

TANZANIA imo katika orodha ya nchi zilizobarikiwa kuwa na vivutio vingi vya utalii na vinailetea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Hivi sasa, imejikita zaidi kuboresha miundombinu yake ifikike kirahisi kwa Watanzania kwa ujumla.

Hapo kunatajwa mambo kama ununuzi wa ndege, kurahisisha usafiri wa watalii kwenda kuona vivutio vya utalii.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji, Devota Mdachi, bodi imefanya mapitio ya sheria, na imeongezwa majukumu ya msingi ya taasisi kutoka matano hadi 11, yanayojumuisha ukuzaji sekta ya Mikutano na Matukio (MICE).

Maeneo mengine yaliyoongezwa katika sheria hiyo ni jukumu la kutangaza utalii wa ndani, kuendeleza ushirikiano kati ya mashirika na wadau wa sekta na kuanzisha zao la Utalii wa Mikutano na Matukio.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Ewura yabuni mbadala vijijini kukabili 'maduka' ya madumu

Ukurasa 18

BIASHARA

UCHUMI NDANI YA MAZINGIRA

# ‘Mkaa Endelevu’ unavyow kimaendeleo wakazi wa K

Na Christina Haule, Morogoro

USIMAMIZI Shirikishi wa Misitu (USM) ya asili katika kijiji cha Nyali kata ya Zombo wilayani Kilosa, Mkoa Morogoro, umeweka historia kuwasaidia wavunaji mkaa kupitia Mradi wa Kuleta Mageuzi Katika Sekta ya Mkaa Tanzania (TTCS); wengi wameshajenga nyumba boram, wakiondokana na makazi duni.

Mnufaikana na mvunaji mkaa wa njia ya TTCS maarufu ‘mkaa endelevu’ Yoram Maliwa, anasema amefanikiwa kujenga nyumba ya tofali za kuchoma yenye vyumba viwili na imeezekwa yenye thamani ya Sh. mil 2.5.

Anasema awali aliishi kwenye nyumba ya udongo iliyoezekwa kwa makuti, hadi mwaka 2015 ndipo alianza kukata ‘mkaa endelevu.’ Hapo mara moja aliona faida, akimsomesha mtoto aliyehitimu elimu ya sekondari na mwengine anafanya mitihani ya kumaliza kidato cha nne.

Maliwa anasema, anaendelea kutengeneza mkaa endelevu akiwa na matarajio ya uhakika kuvuna magunia 100, itakayompa pesa za kununua bati 30 na kujenga nyumba nyingine ya kisasa.

Mzalishaji mkaa huyo mwenye mke na watoto watano, pia anasema ameshafungua akaunti benki, inayomsaidia kujikimu kimaisha na familia, huku akiendelea kutunzaji mazingira.

Aidha, anasema mradi umewasaidia kuondoa adha ya kuchangishwa katika shughuli za maendeleo kijijini, ikiwamo kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya nyongeza shuleni, ofisi ya kijiji na hata dawati.

Kwa vipi? Inaelezwa kutokana na pesa zinazoingia kwenye mfuko wa kijiji unagharamia mahitaji hayo.

Maliwa anasema, wakiyazingatia mafunzo waliyopewa na TTCS, yatawasaidia sana, akilitaja suala la kuweka hisa, kutunza mazingira sambamba na msitu, kilimo kwanza na kupata faida.

Inaelezwa, mpaka sasa wameshajenga ofisi ya kijiji na zahanati, kutokana na faida inayopatikana kwenye mazao ya msitu.

Agnes Mathius, ni mkazi wa Nyali, anasema tangu aanze kuvuna mkaa kwa njia endelevu mwaka 2013 hadi sasa amefanikiwa kukarabati nyumba yake ya vyumba vitano kuwa ya kisasa sambamba na kununua king’amuzil.

Mama huyo anasema, manufaa hayo ni kupitia uhifadhi hisa kwenye kikundi cha kikoba mpango, ambao wamefundishwa kupitia



Distributed via ippmedia

> **“Mradi umewasaidia kuondoa adha ya kuchangishwa katika shughuli za maendeleo kijijini, ikiwamo kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya nyongeza shuleni, ofisi ya kijiji na hata dawati.**

Shule ya msingi wilayani Kilosa iliyokarabatiwa kupitia Mradi wa Mkaa Endelevu. Picha nyingine; Mdau m **MTANDAO.**



# aibua
# ilosa



radi huo akiwa kazini. **PICHA ZOTE:**



mradi wa mkaa endelevu.

Anataja pia mafanikio ya kumsomesha mwanawe hadi kufikia kidato cha nne, ambaye hivi sasa anafanya mitihani.

Mwanaharusi Athumani, ni mkazi wa kijiji cha Nyali, anaushukuru mradi wa Mkaa Endelevu, kwa elimu waliyowapa kuvuna mkaa kitaalamu na kupata faida iliyomuwezesha kukarabati nyumba yake na kumsomesha mwanawe hadi chuo cha ualimu.

Athumani anasema, awali alijenga nyumba ya kawaida, lakini baada ya kuingia mradi wa mkaa endelevu unaosimamia masuala ya uhifadhi shirikishi wa misitu, amepata fedha za kujikimu na kufanya mambo mawili kwa wakati mmoja.

Pia, anasema tayari ameshanunua kiwanja kingine kwa ajili ya kujenga nyumba ya matumizi mengine.

Anasema, awali wanawake hawakujihusisha kuvuna mkaa, wakiambiwa hilo ni la wanaume, lakini baada ya kuelimishwa kupitia Mkaa Endelevu, wamehamasika kujiunga kwenye Chama na Uvunaji Mkaa kuanza na sasa wanaona faida yake.

## MNUFAIKA ASEMA

Betina Mganga, mwanamke kijana aliyesomeshwa kwa fedha za Mkaa Endelevu, anaelekeza shukrani kwa mradi kumpa fursa mama yake kupata fedha za kumsomesha na kutimiza mahitaji yao mengine.

Anasema, ameshasoma katika Chuo cha Ualimu Mtwara hadi ngazi ya Diploma alikohitimu mwaka huu na kwamba, kwa sasa anafundisha kwa kujitolea kwenye Shule ya Msingi Zombo, iliyopo kata ya Zombo, Kilosa, anakoishi na mama yake akisubiri kupangiwa ajira.

## MWENYEKITI MTANDAO

Mwenyekiti wa Mtandao wa Wazalishaji Mkaa Endelevu wilayani Kilosa, Rashidi Kazeuka, anasema kuanzishwa hifadhi misitu kwa njia endelevu, umeleta heshima ya msitu kuinufaisha jamii kwa kila namna, kufanya wanakijiji wawe mbali na uharibifu wa misitu kama zamani.

Hivyo, ombi lake ni taasisi zinazohusika kuwapa kipaumbele tena watakapoanza awamu nyingine ya mradi, kwani iliyopo ya pili imefika mwisho, kukiwapo vijiji 17 kati ya 20 vinavyohusika na Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM), vinaendelea kunufaika na misitu tofauti.

Anasema, awali waliishia mtazamo kwamba misitu yote ni mali ya serikali na hawakuwa na nafasi kuitumia na walishia kuvuna mkaa kwa njia tofauti, lakini sasa wametambua uwezekano kumiliki msitu na kuendesha maisha yao.

Pia, Kazeuka anasema makusanyo mengine kwenda halmashauri na inayobaki inakuwa ya vijiji kwa maendeleo yao.

## MENEJA MRADI

Meneja Mradi wa Mradi wa Kuleta Mageuzi Katika Sekta ya Mkaa Tanzania (TTCS), Charles Leonard, anasema uanzishwaji misitu ya ardhi za vijiji katika wilaya tatu za mradi; Kilosa, Mvomero na Morogoro, umeweza kusaidia uvunaji endelevu wa rasilimali za misitu.

Pia, anasema kuna suala la kuvipatia vijiji 30 vilivyopo na kupata kiasi cha Sh. bilioni 2.8, kutokana na mapato ya ushuru wa mkaa na mbao, kutokana na uvunaji tani 10,000 za mbao na mkaa.

Anaeleza kwamba, fedha hizo zimeshaingia katika mgawanyo, serikali za vijiji zimepata zaidi ya Sh. bilioni 1.5 kutoka ushuru wa vijiji na mapato, inayotumika kuboresha maendeleo vijijini, ikiwamo ujenzi wa madarasa, zahanati, kusajili wanavijiji kwenye huduma za bima afya zilizoboreshwa.

Pia, pesa inatumika kuchimba visima virefu vya maji na kulipaa walimu na wahudumu wa afya wanajitolea kwenye zahanati zao.

Leonard anasema, fedha hizo zinasaidia serikali kupunguza kupeleka fedha za maendeleo kwenye maeneo hayo na kupeleka kwenye maeneo mengine na wazalishaji mkaa zaidi ya 2000 hupatiwa Sh. bilioni 1.3 inayotumiwa na wazalishaji mkaa kuboresha maisha yao.

Anasema, misitu hiyo ya hifadhi iliyopo kwenye vijiji 30 ni zaidi ya hekta 141, zimesaidia kupunguza uharibifu wa misitu na kupunguza kasi ya ufyekaji msitu katika maeneo ya mradi, ikilinganishwa na maeneo yasiyo na mradi, ndio maana wanalenga ufike mbali zaidi.

Meneja Mradi anasema, katika awamu ya kwanza na ya pili, walikutana na changamoto mbalimbali, ikiwamo mkaa endelevu unaozalishwa ni kiwango kidogo kulingana na mkaa uliopo sokoni, kama vile kwenye soko kubwa la Dar es salaam.

Anafafanua, mkaa uliozalishwa kwa njia zisizo endelevu nje ya maeneo ya mradi, imeuzwa kwa bei ya chini waklikwepa ushuru na kukosesha mapato ya serikali, huku ukileta changamoto ya ushindani soko.

Kwa mujibu wa Leonard, mpango wa mradi ni kuweka mfumo utakaochangiwa na vijiji kwa asilimia saba, ambazo zitatumika kutoa mafunzo kwa wanavijiji, kuwasaidia sokoni, sambamba na kuhimiza uwekezaji kwenye maeneo yao, ikiwamo kuanzisha vijiji vingine katika mradi kwa sasa.

Anasema wanatarajia kuwa na awamu ya tatu, utakaoanza Desemba mwaka huu, hadi mwezi Novemba mwaka 2022, wanaongeza maeneo ya mradi katika wilaya nne nchini, katika mikoa ya Mtwara, Tanga na Lindi, Ruangwa na Nachingwea.

# Mwanamitindo Odemba kumtua mama ndoo



Miriam Odemba akiwa na watoto katika moja ya matukio ya kijamii. **PICHA: MTANDAO**

**Na Tatu Tambile**

SERIKALI ilizindua kampeni iitwayo 'Kumtua Mama Ndoo Kichwani."Hapo lengo kuu ni kuhakikisha kila maeneo kunapatikana huduma ya maji safi na salama.

Hiyo inafanyika mbali na kupata huduma ya maji bomba, pia kunachimbwa visima virefu na vifupi, kutumia maji ya maziwa na mito kuyapeleka katika maeneo mbalimbali nchini. Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alionekana kuunga mkono kampeni hiyo mwishoni mwaka jana alipozungumza na waandishi wa habari na wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika uwanja wa Shule Sekondari Bugando, wilayani Geita.

Aliwaagiza wakuu wa wilaya kusimamia uhifadhi wa maeneo vyanzo vya maji, ili kuyafanya yaendelee kuwa chepechepe na kuhakikisha vijiji vyote vinapata maji ya uhakika na kuainisha maeneo ya misitu na vyanzo vya maji, yatunzwe vizuri.

Katika hatua nyingine za juhudi za kuunga mkono kampeni ya "Kumtua Mama Ndoo Kichwani" mwaka huu Naibu Waziri wa Maji Jumaa Aweso, alizindua na kukagua miradi ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, katika Kata ya Ibwera, eneo la Rugaze yenye uwezo wa kuhudumia zaidi ya wananchi 500, ambako juhudi za serikali zikiendelea kufanyika kuwafikia wengine kuhakikisha wanapata huduma bora ya maji safi na salama.

Vijijini ndiko wahanga wakuu wa upatikanaji na maji safi na salama. Sasa taasisi nyingine zisizo ya kiserikali, zimekuwa zikiunga mkono kampeni hiyo ya kiatifa, chini ya msimamizi mkuu, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Hapo ni asasi ya African Reflection Foundation, chini ya mwanamitindo ya zamani, Miriam Odemba. Alipozungumza na waandishi wa habari Jijini Dar es Salaam, anasema ameamua kutoka nchini Ufaransa alipokuwa akiishi, kuja nchini Tanzania ili kuunga mkono jitihada za serikali.

Odemba anasema kwa kutambua changamoto hizo ameamua kuunga mkono jitihada za serikali kufanya kazi kwa kushirikiana wadau, ili ama kuondoa au kupunguza tatizo la upatikanaji maji safi na salama.

"Wote tuna malengo ya kuisaidia jamii katika nyanja tofauti, ikiwamo kutafuta wafadhili kwa ajili ya kuendelea na kufanya utafiti wa miradi tunayoilenga hapa nchini.

"Basi, tumeona vyema tufanye kazi kwa kushirikiana huku taasisi ya ARF imebobea katika misaada ya kuchimba visima na wameshafanya hizo kazi sehemu nyingi nchini," anasema.

Odemba anasema, Oktoba mwaka huu walitembelea Wilaya ya Mkuranga kutimiza ahadi ya kuchimba visima katika lijiji cha Kiwambo, katika Shule ya Msingi Kiwambo, yenye wanafunzi 366, ili wapate maji safi na salama, kuokoa kinamama watoto walio katika changamoto nyingi wanapofuata maji mtoni.

Wito wake ni jukumu la kila Mtanzania mwenye hofu ya Mungu kuguswa kwa namna moja au nyingine kuchangia wahitaji wanaoishi katika mazingira ambayo si rafiki kusaidia kukabiliana na changamoto zinazowazunguka ya huduma ya kijamii ikiwamo ya maji safi, elimu, afya na malazi kwa ujumla kuhakikisha watoto, wamama, wazee na vijana wanapata huduma bora ya kijamii.

UCHUMI

BODI UTALII NA MIAKA 4 YA JPM

# Jaji Mihayo: Niliikuta TTB hoi, madeni na akaunti, sasa walau inatazamika

• Mkurugenzi achambua kutambaa hadi kutembea • Majukumu, sheria upya; ATCL, mabalozi hongera

INATOKA UK.13

Pia, kuna wajibu wa TTB kutoa msaada wa kitaalamu na masoko, kukuza uwekezaji katika utalii wa mikutano na matukio, kutangaza na kuendeleza utalii wa utamaduni na bidhaa nyingine, ili kuvutia mahitaji makubwa zaidi katika soko.

**JAJI MIHAYO**

Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Jaji Thomas Mihayo, anasema alipoteuliwa kuongoza wa mwenyekiti wa bodi hiyo, mwaka 2016 alikuta asasi hiyo akitamka 'iko hoi sana.'

"Kwenye akaunti ya kwanza kulikuwapo Dola (za Marekani) 6000 (Sh. milioni 13.4) na akaunti nyingine ya pili kulikuwapo Sh. milioni 12 na deni la shilingi bilioni saba, lakini deni hilo hivi sasa limeshuka hadi kufikia Sh. bilioni moja," anasema.

Anataja chanzo la deni la Sh.bilioni saba, lilichangiwa na mkataba anaoutafsiri 'haukuwa na tija, wala faida' na haukuanzia ndani ya bodi.

Jaji Mihayo anataja kwamba TTB ilikuwa na madeni mengi ya huduma kama vile umeme na malipo ya watumishi, ambayo baadhi yake yalibeba maswali.

Anaeleza mikakati yake kwa kuishirikiana na uongozi, waliamua kwenda kuiona serikali, wakakutana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na walimueleza hali ilivyokuwa kifedha.

Mwenyekiti huyo anasema ombi lao lilikubalika na walipewa fedha Sh.bilioni 2.4 na ndizo zilizobadilisha sura ya TTB.

"Wakati naingia kwenye uongozi wa Bodi, Waziri (Profesa Jumanne) Maghembe alikuwa anasema TTB hatuutangazi utalii, lakini tungetangazaje utalii wakati hatuna fedha?" anasema na kufafanua:"Lakini, baada ya kupata fedha hizi, tulizitumia vizuri na TTB ikaanza kujulikana na kazi zake,"

Anajisifu hivi sasa mashirika mengi yanataka kujiunga na bodi hiyo kuutangaza utalii, pia kuna vijana wengi wa Kitanzania wenye maono ya utalii wakiomba ushauri, kuwa wadau wa kuutangaza utalii kwa njia mbalimbali.

Jaji Mihayo anawasifu mabalozi wa nchi katika awamu ya uongozi uliopo, hivi sasa wanashirikiana na TTB kufungua soko la utalii, akitaja baadhi ya mafanikio yako katika nchini za Israeli, Italia, China, Korea Kusini, Malaysia na Singapore

"Mwanzoni tulikuwa hatuna hela na tulikuwa hatuwezi kwenda kwenye masoko hayo kutangaza vivutio vya utalii vinavyopatikana Tanzania, ikiwamo fursa za biashara na uwekezaji," anasema

Jaji Mihayo anasema, Rais Dk. John Magufuli, aliwaambia mabalozi wote wafanye diplomasia ya uchumi, ili Tanzania ifaidike na uwapo wao katika kukuza uchumi, wakiwaleta watalii, jambo analosifu na mabalozi wote wameitikia kwa vitendo.

"Hivi sasa, masoko haya yamefunguliwa na balozi zetu na watalii wanaokuja kutoka kwenye nchi hizo, ni nguvu zilizowekwa na mabalozi wetu na Bodi ya Utalii," anasema.

Pia, anasema katika kipindi hiki cha miaka minne ya uongozo wa Rais Dk.Magufuli, mazao ya utalii yameongezeka, akifafanua awali walijikita zaidi katika utalii wa wanyama na Mlima Kilimanjaro.

Jaji Mihayo ,anasema hivi sasa utalii umepanuka ukihusu pamoja na Mambo ya kale, unaopendwa zaidi na watalii kutoka nchi ya Israel na China.

"Naamini sasa hivi mambo ya kale utalii unashika namba moja katika kuchangia pato la Taifa kwa asilimia 17.5 ukiondoa sekta ya kilimo halafu katika ajira ni sekta ya kwanza," anasema nyinginezo ni misitu, fukwe, nyuki, utalii wa mikutano na meli (cruise ship).

Anataja vitu vilivyochangia utalii kuchangia kwa wingi katika Pato la Taifa, ni kuongezeka watalii hasa katika makundi kuweka rekodi ya watalii ya kuwasili watalii 1000 kwa siku moja.

Pia anasema hoteli zimeongezeka kujengwa, vitanda vimeongezeka, zingine zinakarabatiwa kusaka hadhi bora, vikundi vya utalii wa mila vimeongezeka na hivi sasa kuna matamasha mengi yanayolenga kutangaza utalii.



Mandhari na vivutio vya kitalii ndani ya hifadhi ya Serengeti iliyopata tuzo ya Afrika.

> **Hivi sasa, masoko haya yamefunguliwa na balozi zetu na watalii wanaokuja kutoka kwenye nchi hizo, ni nguvu zilizowekwa na mabalozi wetu na Bodi ya Utalii.**



Mwenyekiti wa TTB, Jaji Thomas Mihayo.



Mkurugenzi Mtendaji wa TTB, Devota Mdachi. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

**VIKWAZO**

Penye uzuri, hapakosi vikwazo Pamoja na uwekeza katika sekta ya utalii, Jaji Mihayo anasema bado TTB hajajitosheleza kifedha za kuutangaza utalii, akitaja mfano wa nchi kutoka jumuia ya nchi za Scandinavia: Finland, Sweden, Norway na masoko mengine kama vile Vietnum, Russia na nchi zingine.

Anasema bodi ya TTB inatarajia kwenda nchi ya Vietnam mwezi Februari mwaka ujao kutangaza vivutio vya utalii wa Tanzania na tayari tumeongea na balozi wa Tanzania nchini Vietnum na alituhakikishia kuwa soko la Vietnam ni zuri.

**MKURGENZI TTB**

Mkurugenzi Mtendaji wa TTB, Devota Mdachi, anasema katika kipindi cha Rais Dk. Magufuli, wamefanikiwa, ikiwamo ya kuongezeka kwa idadi ya watalii kimataifa mwaka jana, walishafikia 1,505,702 kutoka watalii 1,137,182 wa mwaka 2015.

Hesabu hiyo ya mwaka jana, iliingizia serikali jumla ya Sh. bilioni 5,441,666.34.

Pia mapato ya nchi kutoka Kodi ya Mapato yameongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 1,901.95 mwaka 2015 hadi Dola za Marekani milioni 2,412.30 za mwaka jana.

Mkurugenzi anataja masoko mapya yamefunguliwa katika nchi za China, Korea Kusini na Israel, kuungana na yaliyozoeleka ; Marekani, Uingereza, Ujerumani, ambako kuna makakati maalum ya kutangaza masoko yake. Masoko mengine makongwe ni Ufaransa na Italia.

"Kwa kushirikiana na wadau tumeweza kuandaa kauli ya utambulisho mpya wa nchi kimataifa ambayo ni Tanzania Unforgettable" anasema na kuna studio ya utangazaji kwa njia ya kielekroniki.

Devota anataja miradi ya utalii wa utamaduni chini ya Programu ya Utalii wa Utamaduni unaosimamiwa na TTB na imeendelea kuongezeka kutoka miradi 50 mwaka 2016 mpaka 72 sasa.

**WATALII VIKUNDI**

Devotha anataja aina mpya ya watalii wanaokuja nchini kwa vikundi kutoka nchi za China na Israel wakitumia ndege za kukodi, akitoa mfano hai ya watalii 1000 waliokuja nchini mwaka huu mwezi April kutoka Israel.

Pia, anataja kundi jingine la watalii 150 walifika nchini mwezi Agosti, wakitokea Israel na zaidi ya watalii 300 kutoka China.

**"TUZO KIMATAIFA"**

Tanzania inaendelea kupata tuzo mbalimbali za kimataifa kama eneo bora kwa utalii duniani. Anafafanua : "Tuzo hizi hutolewa na majarida na mitandao mbalimbali ya utalii kila mwaka kama vile New York Times, Lonely Planet, Safaribookings.com, CondéNastTraveler.com, Buzzfeed.com, Travel and Leisure magazine, fox news.com na National Geographic."

Anasema, vivutio vya utalii vimeendelea kupata tuzo za World Travel Africa (WTA) ngazi ya Afrika, Mlima Kilimanjaro ukipata tuzo ya kuwa kivutio cha utalii kinachoongoza barani Afrika 2018 na Serengeti inaongoza barani Afrika mwaka huu.

**MAONYESHO, FILAMU & SAFARI**

Lingine, ni kuendelea kukua na kuimarika onyesho liitwalo Swahili International Tourism Expo (S!TE) kila mwaka jijini Dar es Salaam na wanawaalika wakala wakubwa wa utalii na waandishi wa habari za utalii kutoka katika masoko makuu duniani.

Anasema mwaka 2017 idadi ya waonyeshaji ilikuwa 145, mawakala kutoka nje walikuwa 224, mwaka 2019 idadi ya waonyeshaji ilikuwa 152, wakala kutoka nje walikuwa 280 wakati mwaka 2019, idadi ya waonyeshaji ilikuwa 210 na wakala wa nje walikuwa 333.

Pia katika awamu iliyopo ya serikali, Devota anasema, TTB imefanikiwa kutengeneza filamu ya kuhamasisha utalii wa ndani na kuiweka katika mabasi yaendayo mikoani. Filamu ilitengenezwa mwaka 2017 na kuzinduliwa rasmi katika kituo cha mabasi ya mikoani cha Ubungo jijini Dar es Salaam.

Vilevile kuna safari za kwenda katika maeneo mbalimbali ya vivutio vya utalii hapa nchini kutokana kufufuliwa kwa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL).

Anataja baadhi ya maeneo hayo mikoa ya Katavi, Kigoma, Tabora na Mtwara, akifurahia kuanza kwa safari za ATCL kwenda nchi kama Zimbabwe, India na Afrika Kusini, kwamba kumerahisisha safari za watalii kufika nchini na kunaongezeko idadi ya watalii.

# Biashara katika picha



Mkuu wa Bidhaa na Bei wa Zantel, Aneth Muga, akionyesha simu janja ya Smart kwa waandishi wa habari, baada ya kuizindua mjini Zanzibar mapema wiki hii. Simu hiyo, inanunuliwa ikiwa na GB 12 intaneti kwa matumizi ya mwaka mzima. **NA MPIGA PICHA WETU**



Kijana akiwa amebeba stuli, akisaka wateja ili ajipatie kipato, kando ya Barabara ya Kawawa, eneo la Msimbazi Centre, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**



Wachuuzi wa maparachichi wakisaka wateja katika Barabara ya Gymkhana, Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

BIASHARA

# Ewura yabuni mbadala vijijini kukabili 'maduka' ya madumu



Wenye madumu katika foleni ya kununua mafuta. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Distributed via ippmedia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NISHATI ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya binadamu. Ni msemo unaotokana na ukweli kwamba bila ya nishati mambo mengi hayawezi kufanyika, kama vile uendeshaji viwanda vya ngazi tofauti, kwa sababu ni kichocheo kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Nishati ya mafuta za taa, petroli na dizeli, zinatajwa kuwa kichocheo kikubwa kwa shughuli za kila siku hasa katika kuendesha mitambo mbalimbali yakiwamo magari.

Kutokana na umuhimu huo, serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura) imekuwa ikifanya jitihada kuhakikisha nishati hiyo inapatikana kwa wingi, ili kupunguza ulanguzi na wananchi wasipate shida katika shughuli zao za kila siku.

**KULIVYO VIJIJINI**

Pamoja na mafuta kuuzwa katika vituo vinavyojengwa kupitia vibali vya Ewura, hali ya upatikanaji nishati hiyo vijijini imekuwa ngumu, kutokana na hali halisi ya miundombinu.

Hadi sasa kubwa ya Watanzania wanaishi vijijini na kutokana na umuhimu wa huduma, hiyo baadhi ya wafanyabiashara wadogo wanalazimika kununua mafuta kwenye vituo mijini na kuuza reja reja kienyeji kwenye madumu na chupa za maji, kwa ujazo tofauti vijijini.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Joseph Mahindoni, anasema wauzaji wamekuwa wakiuza mafuta kwa ujazo tofauti kwenye maduka ya bidhaa zingine, pia vibanda vya barabarani, ili kurahisisha upatikanaji wake vijijini.

> **"Nishati ya mafuta inatakiwa kuuzwa kwa utaratibu unaokubalika na kwa kuwa kujenga visima vikubwa ni gharama, njia hiyo ni bora na itakuwa ni rahisi kuwafikia wateja walio wengi.**

Anasema, kutokana na hali hiyo ya kimiundombinu, wafanyabiashara wa mafuta wamekuwa wakisita kujenga vituo vya mafuta maeneo ya vijijini na matokeo yake kujikita katika miji mikubwa, barabara kuu na miji midogo inayokuwa kibiashara.

Mkazi wa Mwitikira, katika Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Manzije Mazengo, anasema hali ya upatikanaji mafuta ni changamoto kwao na wanategemea wafanyabiashara wenye maduka ya vijijini hapo kusafirisha bidhaa hiyo, kutoka jijini Dodoma.

"Hapa unaweza kuishiwa mafuta ya taa, ukasubiri hadi jioni ndio upate, maana wanaouza wanafuata Dodoma mjini na hadi kufika huku ni jioni kabisa giza limeshaingia kwa kuwa magari yanayofanya safari za huku, yanaondoka Dodoma mjini saa nane mchana. Kwa kweli ni changamoto,"anaeleza.

Pia, anasema mafuta yanayotunzwa kwenye madumu kwenye makazi au sehemu za kawaida za biashara na pindi inapotokea moto yanachangia mazingira ya madhara kwa maisha ya watu na mali zao.

**VITUO TEMBEZI**

Kutokana na kuwapo mazingira hatarishi kwa sababu ya utunzaji na uhifadhi wa mafuta usiozingatia vigezo na masharti, Ewura, imekuwa ikibuni mbinu mbalimbali kuhakikisha nishati hiyo inapatikana vijijini kwa usalama.

Kwa sasa, Ewura inaanzisha utaratibu wa vituo tembezi ili kurahisisha upatikanaji huduma, kutokana na mahitaji yake kuongezeka kwa kushamiri kwa usafiri wa pikipiki maarufu kama bodaboda ambao ndio usafiri wa haraka kwa maeneo mengi.



Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Ewura, Titus Kaguo.

Akizungumza kwenye semina ya waandishi wa habari mjini Dodoma hivi karibuni, Mkuu wa Kitengo ya Mawasiliano na Uhusiano, Titus Kaguo, anasema Ewura imeibua mkakati mpya wa kuanzisha vituo vya mafuta vinavyotembea, (mobile fuel system) kwa kutumia magari maalumu, yaliyotengenezwa ajili ya kazi hiyo.

Kaguo anasema ni mpango unaolenga kurahisisha upatikanaji mafuta katika maeneo mbalimbali nchini, yakiwamo ya vijijini.

"Nishati ya mafuta inatakiwa kuuzwa kwa utaratibu unaokubalika na kwa kuwa kujenga visima vikubwa ni gharama, njia hiyo ni bora na itakuwa ni rahisi kuwafikia wateja walio wengi," anasema Kaguo.

Anasema, katika maeneo mengi nchini wafanyabiashara wadogo wamekuwa wakisafirisha na kuuza mafuta kwa njia ambazo si sahihi na zinazohatarisha usalama wa vyombo vya watumiaji na maisha yao wenyewe.

Kaguo anafafanua kwamba, watu hivi sasa wanatakiwa kufahamu kuwa kusafirisha kuuza mafuta kwa njia zisizo rasmi kwa kutumia madumu, ni kosa kisheria na hatari kubwa inayoweza kusababisha majanga kama milipiko ya moto.

"Kutokana na ongezeko la vyombo vya usafiri kama pikipiki, tumeamua kupunguza gharama za kuanzisha vituo vya uuzaji mafuta ili viweze kujengwa katika maeneo mbalimbali hasa vijijini ili kuepuka uuzaji mafuta katika vidumu," anasema.

Anaongeza: "Kwa sasa tunakuja na vituo vya mafuta vinavyotembea ambavyo vitatoa huduma vijijini, kwa mfano mtu anakuwa na gari ndogo, unaweka tenki ambalo litakuwa limepimwa halina 'risk' au pikipiki za Guta mtu anabeba lita 50 anapita njia labda ya Mtera (Dodoma- Iringa) anakuuzia pikipiki itasaidia 'gap' (pengo) la kutokuwa na vituo vijijini."

Anaeleza kwamba, Chuo Kikuu cha Dar es salaam (UDSM), hivi sasa kinafanyia utafiti wa suala hilo na lipo katika hatua za juu, hivi karibuni watatoa taarifa ya kuanza kwa biashara hiyo.

"Tuna imani itapunguza 'risk' (hatari) za watu kujenga vituo vikubwa kwenye vijiji.Usafirishaji mafuta kwenye madumu ni 'risk' sana hatuwezi kuruhusu vitu vya aina hii kutokana na uhaba wa vituo,"anasema.

Aidha, Kaguo anasema kuna mfumo wa ujenzi wa vituo vya vijijini, kwa lengo la kumsaidia mtu asiye na uwezo wa kujenga kituo kikubwa, ili aweze kujenga kidogo kinachogharimu si zaidi ya Sh. milioni 50.

"Kujenga kituo ni gharama. Kituo kikubwa kama pale Dar es salaam, unaweza kukuta kati ya Sh. milioni 800 hadi Sh. bilioni moja.

"Ndio maana tumekuja na mfumo unaoendana vijijini, kwa mfano kituo cha pampu moja ambacho kina uwezo wa kuwa na lita za mafuta laki moja. Huwezi kuweka lita milioni mbili wakati wewe unauzia pikipiki ambazo zinatumia lita 12," anasema.

**TAHADHARI MAGARI**

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Ewura, Nzinyangwa Mchany, anatoa tahadhari mbalimbali muhimu kuhusu matumizi ya mafuta, ikiwamo magari ya kubebea mafuta ama kutoegeshwa au kulazwa pasipohusika.

Badala yake anashauri yawekwe sehemu maalumu ilizotengwa, huku akitaja tahadhari nyingine ni kuwa shughuli zote zinazohusu mafuta ya petrol, ni lazima zifanyike kwa umakini na uangalifu mkubwa, kuepuka madhara yanayoweza kutokea.

UCHUMI

# Vanilla inapoongezeka zao la matumaini kwa wakulima

Na Nimi Mweta



Mkulima akihudumia zao la vanilla shambani. Picha ndogo ni baada ya kukaushwa. **PICHA: MTANDAO.**

MATUMAINI yanaongezeka mkoani Kilimanjaro kutokana na zao la vanilla, wakati ambao Tanzania inakuwa mwenyeji wa mkutano wa kimataifa wa kuinua kilimo cha zao hilo.

Washiriki wa mkutano huo wiki hii wanatazamiwa kutoka nchi tofauti duniani, ambako mazingira yanaruhusu kilimo cha zao hilo na Tanzania ni moja ya nchi zinazoinuka katika fani hiyo. Ni moja kati ya mazao mapya ambayo yanaibuka kwa nyakati tofauti, au yamefahamika kuwa na soko zuri.

Wakati kilimo cha vanilla kinaanza kufahamika kwa watu wengi, tayari mikoa ya Kaskazini ilishaanza kuondoa mazao ya zamani kama kahawa na kuingia mazao mapya yenye soko kubwa Ulaya na Marekani zaidi, ingawa nchi za Asia nazo zinakuwa soko la bidhaa za matumizi ya matabaka ya kati kiuchumi.

Vanilla hivi sasa inapigiwa debe na kampuni ya Nestle ya Uswisi, inayofahamika kwa maziwa, chokoleti na uzuri wa aina nyingine wa vyakula kimataifa.

Mazao ya biashara katika maeneo ya baridi nchini ni pamoja na kahawa na chai, ambayo yanalimwa maeneo mengi duniani na soko halikui. Kahawa, kwa mfano imekuwa ikitegemea kupungua uzalishaji Brazil ambayo kwa miongo kadhaa na imekuwa muuzaji mkubwa nje, lakini mbegu mpya na mbinu tofauti zimepunguza utegemezi wa hali ya hewa, licha ya kuwa tatizo kwa kahawa ya Brazil halikuwa mvua ila ukungu ukitanga kwa muda mrefu. Kuna nchi mpya zilizoanza kulima kahawa kwa wingi, kama Vietnam ambazo hazina tatizo la ukungu.

Kutokana na chagamoto hizo za kahawa, limekuwa na bei ya kudorora kila wakati na juhudi za vituo vya utafiti kama TACRI mkoani Kilimanjaro kuboresha ladha ya kahawa kwa mbegu mpya kila wakati zimewezesha ushindani, ila bado katika bei katika soko la kimataifa.

Pamba hasa katika mikoa ya Ziwa, bado kuna matatizo, baadhi ya vyama vya ushirika vinakusanya pamba chafu, hairudishi thamani ya mikopo pembejeo. Kwa kweli wanaiumiza akili serikali, kuwapa usumbufu wananchi wake, wakulima.

'Habari ya mjini' nyingine katika eneo kubwa au lote Kanda ya Ziwa ni kilimo cha katani, ambacho kiliinua mkoa wa Tanga nyakati za uhuru na eneo dogo la Mkoa wa Kilimanjaro, halafu bei yake ikaporomoka.

Eneo jingine la kufurahisha kuhusu kuanza kwa wakulima kuhamia vanilla ni kuwa kampuni kubwa zinazohitaji zao hilo wanaanza mipango ya kilimo cha mkataba, kinachompa mkulima uhakika wa soko la mazao yake.

> **Vanilla hivi sasa inapigiwa debe na kampuni ya Nestle ya Uswisi, inayofahamika kwa maziwa, chokoleti na uzuri wa aina nyingine wa vyakula kimataifa.**

Nestle imepeleka maofisa wa kampuni hiyo kukagua kilimo cha vanilla katika maeneo kadhaa mkoani humo, kuangalia changamoto wanazopata wakulima na njia ya kuzitatua.

Inaweza kuwa mwanzo wa kuweka mipango endelevu kusimamia kilimo cha vanilla kwa njia hiyo, hasa kama sio kujaa mazao kutoka maeneo tofauti duniani. Ni hapo tu ambapo bei itaanza kushuka, zao hilo liwe kama yake ya jadi yaliyochoka kitambo.

Kuinuka kwa zao za vanilla ni sehemu ya mkondo wa mazao mapya yanayoanza kufahamika katika nyakati tofauti miaka ya 2000, unaweza kuita mazao ya utandawazi, ambayo yako katikati ya maua na matunda, yakiitwa kwa jina la jumla la 'horticulture.'

Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha kuna mashamba ya maua, uliokuwa uwekezaji mpya kabisa kuanzia miaka 10 iliyopita, ulioambatana na kilimo cha viungo.

Zamani kidogo ni Zanzibar iliyofahamika kwa kilimo cha viungo hasa karafuu, ikawa ndiyo haiba yake kimataifa, lakini hatua kwa hatua zao hilo likasambazwa kwingine, kama ilivyo kwa alizeti na mawese. Vanilla ni 'fasheni' mpya ya mazao yanayokidhi mahitaji ya masoko maalum ya vyakula au vinywaji soko la dunia.

Waandaaji wa mkutano huo wa kimataifa wanasema kuwa Tanzania na nchi za jirani wanazidi kuwa na umuhimu katika zao la vanilla na vanillin, kiungo kinachoambatana na mbegu za zao hilo kuongeza ladha inayohitajiwa. Wakati katani inaingiza Sh. 2,000 kwa kilo zao la vanilla liko katika kiwango cha sh. 10,000 hadi 15,000 kwa kilo na siyo rahisi kupata zao tofauti lenye kiwango hicho cha mapato.

Hata hivyo, ni wazi kuwa kiwango hicho cha bei hakitadumu kwani wakulima wengi wataacha mazao ya jadi waingie huko na baada ya muda, kutegemea na muda zao linachukua kuanza kupanda hadi kuvuna na kasi ya wakulima wapya kuingia, bei ianze kuporomoka.

Ndiyo maana furaha inayoambatana na kuzuka kwa zao jipya katika soko la kimataifa na kampuni zinazoanzisha kilimo cha mkataba kwa zao kama hilo, ni habari njema lakini siyo mwisho wa changamoto.

Zitaleta faraja kwa kipindi fulani lakini wakulima wanavyozidi kuchangamkia zao hilo na nchi nyingine kupania kilimo chake, ndivyo bei inavyoanza kuingia mashakani, na hali ya wakulima wanaotegemea zao hilo kuanza kuyumba. 'Baada ya faraja, dhiki.'



UCHUMI

UHABA WA SHEHENA

# Bandari Mtwara yajiwekeza kwenye soko saruji, makaa ya mawe Ruvuma

• Meneja atangaza mkakati 'punguzo la bei' • Waachiwa Bagamoyo, bandari ndogo lukuki • Ajisifu usalama miaka 'chembe wizi' haijasikika


Distributed via ippmedia

Gati mpya katika Bandari ya Lindi, ambayo iko chini ya Bandari ya Mtwara, ujenzi wake umekamilika. **PICHA: BLOGU YA MICHUZI.**

**Na Mary Geofrey,** aliyekuwa

MTWARA

***IJUMAA iliyopita katika jarida hili, ilikuwa na sehemu ya kwanza ya makala kuhusu Bandari ya Mtwara, huduma yake na mageuzi ya maendeleo yanayofanyika. Endelea na maelezo yake, mwandishi alipokuwa huko wiki iliyopita.***

BANDARI ya Mtwara ilijengwa kati ya mwaka 1948 na 1954 na uendelezaji wake uliendana na ujenzi wa reli kutoka Mtwara mpaka Nachingwea kwa ajili ya kusafirisha Karanga kwenda Nachingwea. Hadi sasa inasimamiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Mhandisi Juma Kijavara, Meneja wa Bandari ya Mtwara, anasema ina bandari ndogo za Kilwa, Lindi, Pangani na Bagamoyo.

Kijavara anasema, hadi sasa wanatekeleza mradi wa mita ya kupima mafuta uliopo chini ya Ofisi ya Rais unaofanywa na Mkandarasi kutoka nchini Uswisi akishirikiana na kampuni ya kizalendo.

Anasema gharama za mradi huo ni Euro milioni 17 na kwa upande wa bandari ya Mtwara, mradi utahusisha ujenzi wa mitambo miwili na chumba cha usimamizi kwa ajili ya kupima mafuta ya dizeli na petroli.

> **"Mradi huu ukikamilika utaiwezesha bandari kuhifadhi shehena kubwa ya makasha kwa wakati mmoja, pia kuwa na hifadhi ya mizigo kwa usalama katika maghala yake.**

Kijavara anasema mradi ulianza Machi mwaka huu na unatarajiwa kukamilika Mei mwakani. Anafafanua: "Mradi ukikamilika utakuwa umeiwezesha bandari kutekeleza maelekezo ya serikali na itakuwa na uwezo wa kupima mafuta halisi yanayopita katika bandari hii."

Anasema wanatekeleza mradi mwingine wa ujenzi wa sehemu ya kuhifadhi makasha matupu na sehemu ya kupanga mzigo kwa msimu wa korosho, pia ukarabati wa Ghala Namba Tatu.

Kijavara, anasema, nao ulianza Mei mwaka huu na unatarajiwa kukamilika Mei mwakani kwa thamani ya Sh. milioni 3.297.

"Mradi huu ukikamilika utaiwezesha bandari kuhifadhi shehena kubwa ya makasha kwa wakati mmoja, pia kuwa na hifadhi ya mizigo kwa usalama katika maghala yake," anasema Kijavara.

Kwa sasa bandari ya Mtwara inahudumia tani 400,000 na miradi hiyo itakapokamilika itaweza kuhudumia tani milioni moja kwa mwaka.

**BANDARI NDOGO**

Kijavara anasema, TPA inakusudia kufanya uwekezaji mkubwa wa upanuzi wa bandari za Lindi, Kilwa, Rushungi na Kisiwa/Mgawo na ulianza Agosti mwaka huu na unatarajiwa kukamilika baada ya mwaka mmoja na nusu unaogharimu Sh. milioni 732.4.

"Mradi huu ukikamilika utaifanya mamlaka (TPA), kuwa tayari kuhudumia mizigo ambayo inatokana na utekelezaji wa mpango wa serikali wa kujenga Kiwanda cha Mbolea Kilwa, pamoja na usafirishaji mizigo mbalimbali ya uvuvi wa kibiashara, kilimo na viwandani," anasema Kijavara.

Kijavara anasema, katika bandari ya Lindi, TPA imetekeleza mradi wa ukarabati gati la Lindi, uliokamilika mwaka jana.

Anasema mradi ulihusisha ujenzi wa makaravati, ukarabati sehemu za kufungia meli, ujenzi wa kuta ya bahari na kuongezaa kina cha bahari gatini.

Kijavara, anasema mradi huo wa miezi minne ukarabati wake ulianza Mei 10 mwaka jana umekamilika Septemba iliyopita.

"Ukarabati ulihusisha ubadilishaji wa paa, uwekaji wa mageti mapya, ubomoaji na ujenzi wa kuta dhaifu, uwekaji wa sakafu na ukarabati wa ofisi ya ofisa bandari," anasema Kijavara.

Anaeleza, kwa sasa mradi huo katika kipindi cha uangalizi tangu ukaguzi wa mwisho ufanyike Oktoba 25 iliyopita na utakamilika mwishoni mwa mwaka huu.

**UHABA WA SHEHENA**

Kijavara anasema, kwa kipindi kirefu Bandari Mtwara imekuwa ikitegemea shehena ya zao la korosho, hivyo kufanya bandari kuwa ya msimu na kutokana na changamoto hiyo, bandari inafanya juhudi za kupata shehena za saruji.

"Tayari mamlaka imempa punguzo la bei ya usafirishaji, kampuni ya Dangote kwa ajili ya kusafirisha shehena ya saruji kupitia bandari ya Mtwara. Makubaliano hayo kampuni ya Dangote kusafirisha tani 120,000 kwa mwezi," anasema Kijavara.

Anasema, TPA imeingia makubaliano na kampuni nyingine kusafirisha makaa ya mawe kutoka mkoani Ruvuma kupitia bandari ya Mtwara na shehena hiyo inaenda katika masoko ya nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Kijavara, kuna matarajio ya kusafirisha tani 70,000 kwa mwezi za shehena hiyo pindi usafirishaji utakapoanza.

**MAFANIKIO ULINZI**

Kijavara anasema, Bandari Mtwara iliingia katika mfumo wa ulinzi wa meli na bandari ya kimataifa mwaka 2013 na kuanza kufuata kanuni za kiulinzi zinazotambuliwa kimataifa, hivyo kuwezesha ulinzi kuimarika kwa mafanikio.

"Kutokana na mafanikio hayo kiulinzi, bandari ya Mtwara ni moja kati ya bandari zilizo vizuri kiulinzi pamoja na kuwa eneo lenye changamoto zilizo vizuri kiulinzi pamoja na kuwa eneo lenye changamoto ya kiusalama mpakani mwa nchi za msumbuji," anasema Kijavara.

Anaeleza, moja ya mafanikio ni kutokuwa na matukio ya kihalifu bandarini, kwa kudhibiti wizi na hujuma dhidi ya mali za mamlaka.


Kijavara anasema, taarifa zinaonyesha kati ya mwaka 2016 na 2019, hakuna tukio lolote kubwa la kiuhalifu lililotokea ndani ya bandari ikiwa ni juhudi za kiulinzi katika kudhibiti miundombinu ya ndani na nje ya bandari.

"Mafanikio haya kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na matumizi ya mifumo ya kiulinzi pamoja na askari wenye mafunzo sahihi katika ulinzi wa meli na bandari," anasema Kijavara.

Anatumia fursa hiyo, kueleza kuwa wanathamini ushirikianao inaoupata kutoka serikalini na wadau wote wa sekta hiyo.

"Hata hivyo, ushirikiano unahitajika zaidi ili bandari yetu iweze kutekeleza mipango yake kwa ufanisi ili kutoa huduma bora," anaeleza Kijavara.

Anasema, yapo maeneo ambayo yanahitaji msukumo wa serikali kuendelea kuunga mkono jitihada za mamlaka hiyo katika utekelezaji wa miradi ambayo ni mingi na mikubwa, ikiwamo uboreshaji wea miundombinu ya nchi kavu, katika uhusiano na bandari.



## HABARI MBEYA



Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini, Thobias Andengenye, akiwasili katika ofisi za jeshi hilo, mkoani Mbeya jana, alipofanya ziara ya kukagua utendaji kazi wa askari wake, pamoja na kuzungumza nao. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Jela miaka 30 kwa kubaka mwanafunzi

**Na Grace Mwakalinga,**

MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Mbeya imemhukumu Nickson Mungago (23) mkazi wa Usongwe, Mbalizi mkoani Mbeya kutumikia kifungo cha miaka 30 jela, baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mwanafunzi wa kidato cha tatu (jina la shule linahifadhiwa).

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Zawadi Laizer, alisema mahakama iliridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka kwamba mshtakiwa alimbaka mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka 14 Januari, mwaka huu.

Laizer alisema kupitia mashahidi sita wa Jamuhuri, imebainika wazi kuwa mshtakiwa alimbaka mwanafunzi kama ambavyo alikiri mbele ya Polisi kuwa na uhusiano wa kimapenzi, kitu ambacho ni kinyume cha Sheria ya Elimu nchini.

"Ushahidi upande wa mashtaka akiwamo mlalamikaji ambaye ni mwanafunzi aliyebakwa kukiri kwamba na uhusiano na mshtakiwa kwa ahadi kwamba atamuoa, ni shahidi tosha, hivyo mahakama imeamua kutoa adhabu hii," alisema Laizer.

Mshtakiwa Munyango kupitia wakili wake, Felix Kapinga, aliomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa kile anachodai ni kijana mdogo anayetegemewa na ndugu zake na kwamba ni kosa lake la kwanza, hivyo anajutia kosa hilo.

Hata hivyo, mwendesha mashtaka wa serikali, Davice Msanga, aliomba mahakama kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na jamii kwa ujumla kutokana na watu wengi kuendekeza vitendo hivyo.

Baada ya pande zote mbili kuwasilisha maombi hayo, Hakimu Laizer alitoa hukumu miaka 30 kwenda jela na kuelekeza kuwa upande wowote usioridhika na hukumu hiyo kuwa na haki ya kukata rufani.

# Tulia apiga jeki ujenzi kituo cha afya

**Na Grace Mwakalinga,**
CHUNYA

Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kupitia taasisi yake ya Tulia Trust, ametoa msaada wa Sh. milioni tano ili kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya kilichoko kwenye mamlaka ya mji wa Makongorosi, Chunya mkoani Mbeya.

Dk. Tulia alitoa msaada huo juzi wakati wa Tamasha la Kuimarisha Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UCCM), Mkoa wa Mbeya baada ya kupokea maombi kutoka kwa wananchi wa Makongorosi wakihitaji fedha ili kukamilisha ujenzi wa kituo chao cha afya.

Alisema aliguswa kuchangia ujenzi wa kituo cha afya kwa sababu ni suala muhimu linagusa maisha ya watu na kwamba msaada huo utasaidia kufikia kwenye hatua za mwisho kulinganisha na ilivyo sasa ambapo umefikia hatua ya mtamba wa panya.

Naibu Spika aliwasisitiza wananchi kuendelea kujitoa kwa hali na mali kukamilisha ujenzi huo wakati serikali nayo ikijipanga kuwasaidia ili kituo hicho kianze kutoa huduma haraka.

"Nawapongeza wananchi kwa jitihada katika ujenzi huu si suala rahisi kwa sababu kuna baadhi ya maeneo ambayo wananchi hawaonyeshi jitihada zozote za maendeleo.

Endeleeni kujitoa ili mkalimishe jengo hili serikali iko njiani itawashika mkono na kituo chetu kitaanza kutoa huduma," alisema Dk. Tulia.

Kabla ya kutoa msaada huo, Dk. Tulia alisema wananchi walianza jitihada ya ujenzi wa kituo hicho kwa kuchangia nguvu kazi zao na fedha kutoka kila eneo kwa lengo la kuepukana na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya katika hospitali ya wilaya.

Diwani wa Makongolosi, Sailoni Mbalavata, alimwahidi Dk. Tulia fedha alizozitoa zitafanya kazi iliyokusudiwa na kumwomba usaidia kutafuta wadau wengine ili waongeze nguvu katika ujenzi huo.

# Wagomea amri ya kuhama eneo

**Na Grace Mwakalinga,**
ILEJE

WANANCHI wa Kitongoji cha Namangoni, Itumba wilayani Ileje mkoani Songwe, wameiomba serikali kutatua mgogoro wa ardhi baina yao na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) uliodumu kwa zaidi ya miaka miwili.

Wakizungumza na Nipashe jana, wananchi hao walisema wameishi eneo la Namangoni na kufanya shughuli za kilimo kabla nchi kupata uhuru, lakini mwaka jana TFS iliweka alama za mipaka bila kuwashirikisha na wakataka wananchi hao kuyahama maeneo hayo hali iliyozua taharuki.

Mmoja wa wananchi hao, Pelesi Jacob, alisema ili kuondoa hali ya taharuki ambayo itasababisha wananchi kujichukulia sheria mkononi serikali inapaswa kuingilia kati suala hilo.

"Tumeishi hapa kwa miaka mingi tangu uhuru na ardhi hii ya Namangoni tuliirithi kutoka kwa mababu zetu. Tunaona ajabu TFS leo hii kutuambia tuondoke. Msimamo wetu ni kwamba hatuwezi kuondoka," alisema Jacob.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Namangoni, Edward Mlungu, alisema eneo hilo ni mali yao kwa sababu lilitumiwa tangu zama za mababu zao, hivyo wana haki ya kuendelea kutumia ardhi hiyo.

Pia alisema kitongoji hicho ndicho kilikuwa na huduma muhimu za kijamii, hivyo kuondolewa na eneo hilo kutasababisha hasara kubwa na kwamba TFS wanapaswa kulitathmini suala hilo.

Meneja wa TFS katika Wilaya ya Ileje, Omary Abeid, alisema uamuzi huo upo kwa mujibu wa sheria na kanuni za uhifadhi na kwamba taarifa hiyo ilifika Ofisi za Waziri Mkuu ili kuangalia namna ya kushughulikia.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Joseph Mkude, aliwataka wananchi kuendelea kutumia maeneo hayo mpaka taarifa rasmi itakapotolewa na viongozi huku akiwahakikishia wananchi kuwa haki itatendeka.





# Watishia kususia uchaguzi mitaa

**Na Paul Mabeja,** BAHI

ZAIDI ya wakazi 1,000 wa Kijiji cha Bahi Makulu, mkoani Dodoma wamesusia kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu, kutokana na majina ya wagombewa wanaowata kukatwa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, wakazi hao walisema wamefikia hatua hiyo kutokana na viongozi kuwapangia watu wanaowataka wao badala ya wale ambao ni chagua la wananchi.

Mmoja wa wakazi hao, Ludovick Chizugute, alisema amepanga kutoshiriki katika uchaguzi huo ngazi ya kijiji kutokana na mgombea kukatwa.

Alisema kutokana na viongozi kutaka watu wanaowataka wao, ameona hakuna haja ya kwenda kupoteza muda kupiga kura siku ya uchaguzi. "Hizi fitina za uchaguzi zinazofanywa na viongozi wetu hazijaanzia wakati huu wa kuchukua na kurudisha fomu kwani wakati wa uchaguzi wa ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wagombea tunaowataka majina yao yalikatwa kwa maslahi ya mtu mmoja," alisema.

Chizugute aliongeza pia wakati wa kuchukua fomu kwa ajili ya vyama mbalimbali kugombea nafasi hiyo, wagombea wao wa vyama vya upinzani wamekatwa na kubakishwa mmoja wa CCM.

Naye mmoja wa wagombea ambaye jina lake lilikatwa, Daudi Silyaki, alisema wanaiomba serikali kulifanyia kazi suala hilo kabla ya muda wa kupiga kura kufika.

Alisema kutokana na uamuzi wa wananchi kususia uchaguzi, serikali inatakiwa kufika kijijini hapo ili kutafuta suluhu ya haraka.

"Tunachoshangaa hadi hii leo nimepeleka malalamiko yangu ya kukata rufani lakini hakuna aliyenisikiliza. Mchakato mzima wa uchaguzi haukuwa wa haki kabisa viongozi walikuja na majina yao mkononi," alisema Silyaki.

Naye Amina Masawe alisema wanamwomba Rais (John Magufuli) ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Taifa, kuingilia kati malalamiko yao hayo kwa kuwa wanalazimishwa kumchagua kiongozi wasiyemtaka.

Hivi karibuni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, akizungumza na vyombo vya habari, alitoa maagizo kwa kamati zote za rufani kuyashughulikia malalamiko yote ya watu waliokata rufani kabla ya uchaguzi kufanyika.



Distributed via ippmedia

Ofisa masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna (wa pili kulia), akizungumza na wabeba mizigo wa Soko Kuu la Majengo (hawapo pichani), jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kalemani ataka azaki kufanya utafiti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeziagiza asasi za kiraia (Azaki) kutoa taarifa sahihi na zenye utafiti wa kina katika mijadala zinayofanya ili kuepusha migogoro katika jamii.

Aidha, zimeagizwa kutoa elimu ya namna gani matumizi ya rasilimali zilizopo ikiwamo ongezeko la gesi ili jamii ijue nini kinaendelea katika taifa lao.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema juzi wakati akifungua mkutano wa Jukwaa la Tisa la Uzinduaji uliofanyika jijini Dodoma.

Dk. Kalemani alisema ili kuboresha sekta ya uzinduaji ni lazima azaki zijenge utaratibu wa kutoa taarifa sahihi za rasilimali zilizopo nchini zenye takwimu sahihi ambazo zitaleta tija kwa wananchi.

"Kinachotakiwa katika mijadala yenu inayoendelea na ijayo, fanyeni kazi ya kutafuta taarifa zenye takwimu ambazo mkikaa na kuzijadili zitaisaidia serikali kupiga hatua katika maendeleo, lakini zitawajenga wananchi," alisema. "Jukwaa hili ni muhimu sana kuwapo lakini muwajibike kujadili taarifa za wakati sahihi ambazo nitakuwa na manufaa kwa jamii," alisema Dk. Kalemani.

Akitolea mfano wa gesi, alisema nishati hiyo ilianza kupatikana wakati wa mkoloni na ilianza na futi za ujazo tatu, lakini hadi hivi sasa ni ujazo wa gesi ni trilioni 57.5. Kalemani alisema jambo linalostahili ni kupongeza jitihada zinazofanywa na serikali katika usimamizi wa rasilimali zilizoko nchini. "Haya mambo ndio yanatakiwa kujadiliwa na kutolewa taarifa ili wananchi wajue na kutumia fursa zinazopatikana kupitia rasilimali zao," alisema Dk. Kalemani.

Pia alisema serikali inaendelea na jitihada za kutafuta gesi katika maeneo mbalimbali nchini lengo likiwa kuona inapatikana kwa wingi ili wananchi watumie na kuepuka kutumia mkaa ambao unachangia kuharibu mazingira.

"Watu wengi hutumia sana mkaa. Mfano Dar es Salaam pekee magunia 500 ya mkaa hutumika hapo bado mikoa mingine ndiyo maana tunahimiza matumizi ya gesi hadi vijijini ili kuondokana na matumizi ya mkaa," alisema.

# Bandari Mtwara yapigiwa chapuo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeiagiza Bodi ya Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) hadi kufikia Desemba, mwaka huu, ianze kuingiza mafuta kwa ajili ya kusafirisha nchi jirani kupitia Bandari ya Mtwara.

Aidha, serikali imeitaka bodi hiyo kuhakikisha inawachukulia hatua kali ikiwamo kufungia kituo cha mafuta ambacho kitaficha mafuta kwa kutegea upandaji wa bei.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema hayo jana wakati wa kuzindua bodi mpya ya PBPA, jijini hapa.

Dk. Kalemani alisema hatua ya kuanza kutumia Bandari ya Mtwara kuingizia mafuta ya kusafirisha nchi jirani itasaidia kwa kiasi kikubwa katika kuongeza mapato.

"Naomba hakikisheni Bandari ya Mtwara nayo inaanza kuingiza mafuta ya kusafirishwa nchi za nje ili kuongeza mapato ya serikali. Kwa sasa tunapokea mafuta ya petroli na dezeli peke yake, hivyo ni lazima ifikapo Desemba, mwaka huu, tuanze kupokea na mafuta mengine ya kwenda nchi jirani za Malawi, Msumbiji na Zambia na taarifa niipate," alisema.

Waziri Kalemani pia aliiagiza bodi hiyo kuhakikisha uwezo wa kuhifadhi mafuta katika Bandari ya Mtwara unaongezeka kutoka lita milioni 26 za sasa hadi milioni 80 kwa ajili ya mafuta ya mikoa ya Lindi na Mtwara na nchi jirani.

Alisema bodi hiyo inapaswa kuhakikisha inasimamia na kukomesha tabia ya baadhi ya wafanyabiashara wa vituo vya mafuta wanaoficha mafuta wakisubiri kupanda bei, alisema wafanyabiashara watakaobainika kufanya hivyo wachukuliwe hatua kali ikiwamo kufungiwa kituo.

"Wiki iliyopita bei ya mafuta haikupanda, kulikuwa na dalili za wafanyabiashara wengi kuanza kuficha mafuta wakisubiri bei ya mafuta ipande waanze kuuza, suala hilo halikubaliki," alisema Dk. Kalemani.



## NMB yasisitiza miundombinu bora

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Benki ya NMB wameomba uongozi wa serikali ya Mkoa wa Kusini Unguja kuandaa miundombinu rafiki ili kufikia maendeleo ya mkoa huo na taifa kwa ujumla.

Meneja wa NMB Tawi la Zanzibar, Duchi Amour Duchi , alisema hayo jana walipofanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja na viongozi na watendaji kwa lengo la kujadili namna ya kuwasaidia vijana na kinamama wa kutumia fursa mbalimbali ziliko ndani ya mkoa huo hususan ujasiriamali na ushirika.

Alisema mkoa huo una fursa mbalimbali kutokana na mazingira ya kijiografia zikiwamo kilimo, uvuvi na utalii ambazo zinaweza kuwakomboa kiuchumi wananchi huku akiahidi kutoa mafunzo katika sekta hizo.

Alisema mafunzo hayo yatalenga namna ya kuzalisha bidhaa zinazohitajika katika soko ili kupatikana na kuzalishwa kwa wingi na kuulinda mtaji ili uendelee kukua zaidi wakipatiwa mikopo.

"Mkoa huu wa Kusini umebarikiwa kuwa na shughuli nyingi za ujasiriamali ambazo kinamama wakipatiwa mitaji basi watapiga hatua za kimaendeleo, mfano kuna sekta ya kilimo, uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kupitia vikundi vya ushirika, uvuvi, kilimo cha mwani na hata shughuli za ufugaji kwa hiyo ipo haja ya kupatiwa mafunzo ili bidhaa zao zizalishe katika kiwango kinachotakiwa," alisema.

Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema sasa wakati umefika kwa wananchi wa mkoa huo kuwa na mradi wa ufugaji kuku kwa wingi ili kuweza kuwapeleka hotelini na kuachana na kuagiza kutoka soko la mjini.

Alisema kuwapo kwa machinjio ya kisasa ya kuku kila wilaya za mkoa huo zitasaidia zaidi kukuza biashara ya ufugaji wa kuku na kupelekea kufikia soko uhakika na kuongeza kipato cha wananchi.

Mkuu wa Mkoa amewataka wakuu wa wilaya kuweza kutumia fursa hiyo ya ujio wa NMB kuweza kuandaa vikao vya pamoja ambavyo vitaleta tija kwa serekali na wananchi wa mkoa huo.

Nao wakuu wa wilaya mbili za Mkoa huao ambao ni Mkuu wa Wilaya ya Kati na Wilaya ya Kusini wameomba ujumbe huo kuweza kusaidia mabaraza ya vijana na vikundi vya ushirika ili kuweza kuvipeleka mbele kimaendeleo kwani kufanya hivyo kutapanua wigo wa kibiashara kati ya NMB na wananchi wa mkoa huo.

Ujumbe huo wa NMB uliokwenda kwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Ungunja ni Meneja Uhusiano Idara ya biashara za Serikali za kibenki, Mkunde Joseph na Meneja Idara ya Biashara na Kilimo NMB, Makao Makuu, John Machunda.

# Bodi Baraza la Mitihani yapewa somo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, ameitaka bodi mpya ya Baraza la Mitihani Zanzibar kuendeleza ushirikiano kwa kufanya kazi kwa pamoja ili kuleta maendeleo ya elimu.

Aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa bodi hiyo katika ukumbi wa wizara, Mazizini Mjini Unguja.

Juma alisema ushirikiano ni muhimu kwa bodi hiyo kwa kuwa ni chombo nyeti na ndicho pekee kinachoweza kupima ubora wa elimu hapa Zanzibar katika kuleta maendeleo kupitia sekta ya elimu.

Alisema pamoja na kuwa baraza kujitegemea bado liko chini ya Wizara ya Elimu, hivyo masuala yote wanayoyapanga lazima yapitie kwa viongozi wao wa juu ili kuyathibitisha kwa lengo la kuleta mafanikio zaidi. Kwa mujibu wa Waziri, Baraza la Mitihani halionekani umuhimu wake mpaka vifike vipindi vya mitihani na wakati wa matokeo.

Aliwataka wajumbe kuhakikisha wanatunza siri ndani ya baraza na za serikali kwa ujumla na endapo watakwenda kinyume, hatua za kisheria zitachukuliwa kwa atakayehusika.

Pia aliwataka kuwa wazalendo wa kufanya kazi na kujiepusha na masuala ya itikadi za kisiasa kwa kuwa kufanya hivyo kunaweza kuwaparaganyisha na kutofikia malengo ya kuundwa kwa baraza hilo.

Aidha, Juma aliipongeza bodi mpya iliyoteuliwa na ile iliyomaliza muda wake kutokana na juhudi kubwa waliyoifanya kupiga hatua katika malengo waliyojiwekea.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Baraza hilo, Zubeir Juma Khamis, alisema baraza kwa awamu ya pili limepata mafanikio yakiwamo kuimarisha mfumo wa utoaji wa matokeo unaoonyesha ufaulu kwa mwanafunzi, shule husika, wilaya, mkoa na taifa na kutoa tathmini ya matokeo kwa kila ngazi.

Alisema mafanikio mengine ni pamoja na kuanzisha tovuti ya Baraza la Mitihani Zanzibar kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa taarifa za baraza kwa wadau.

Pamoja na mafanikio hayo alisema bado baraza linafanya kazi katika jengo ambalo linatumiwa na ofisi zingine hali inayowapa hofu ya kufanya kazi kutokana na unyeti wa baraza.

Pia alisema baraza halina sehemu sahihi ya kusahihishia mitihani pamoja na mtambo wake wa kuchapishia mitihani ya taifa na nyaraka zingine.



Mwonekano wa jengo la soko jipya la kisasa la Magomeni, litakalokuwa na ghorofa tatu, linaloendelea kujengwa jijini Dar es Salaam jana, ambalo ujenzi wake unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba mwaka huu. **PICHA: JOHN BADI**

# Balozi Iddi abainisha umuhimu uwekezaji

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kuridhia uwapo wa miradi ya uwekezaji ni kuimarisha mapato ya taifa yatakayokwenda sambamba na ongezeko la ajira kwa vijana.

Balozi Iddi alisema hayo jana alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi mkubwa wa ufugaji kuku wa mayai ulioanzishwa katika Kijiji cha Kandwi, Chaani, Wilaya ya Kaskazini "A" Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema wananchi katika baadhi ya maeneo wanaendelea kutoa ushirikiano mkubwa kwa wawekezaji waliokwishaanzisha miradi yao jambo ambalo huleta faraja kwa serikali licha ya maeneo mengine kuibuka malalamiko yanayotokana na masuala ya ulipaji fidia.

Sekta ya uwekezaji katika miradi mbalimbali, alisema imeanza kuleta mafanikio akitolea mfano mradi huo wa ufugaji kuku utakaosaidia pia sekta ya utalii inayohitaji bidhaa hiyo katika utoaji huduma za kila siku kwa wageni wanaofika.

Balozi Iddi aliushauri uongozi wa mradi huo katika malengo yake ya baadaye, kufikiria utoaji wa vifaranga ili kuwasaidia wafugaji wadogo kuondokana na changamoto ya upatikanaji wa vifaranga hivyo.

Alisema mahitaji ya bidhaa zinazotokana na kuku ni mengi nchini yaliyosababisha wananchi wengi kujishughulisha na ufugaji lakini bado kikwazo kikubwa cha upatikanaji wa vifaranga kinawakumba wakati mwingine inalazimika kuagizwa nje ya Zanzibar.

Mradi huo wa ufugaji wa kuku wa mayai, alisema kwa kiasi kikubwa utasaidia sekta ya utalii inayosimamiwa vyema na serikali kwa kumtaka kila mwananchi kuwajibika kutoa mchango wake wakiwamo wawekezaji.

Mapema, Mkuu wa Mradi huo, Mzee Jaffar Hussein, alisema mradi huo ulioanzishwa na wawekezaji wazawa, umeridhiwa na wananchi wa kijiji cha Kandwi na kuanza rasmi ujenzi wake mwaka huu.

Mzee Jaffar alisema wananchi wa Zanzibar wanapaswa kujenga matumaini ya kupata huduma za bidhaa ya mayai kwa bei nafuu ya Sh. 5,000 trei baada ya kukamilika kwa ujenzi ifikapo mwakani.

Alisema taasisi yake tayari imeshawekeza miradi mingi ya kijamii nchini na baadhi ya mataifa duniani na kufikiria azma ya kuwekeza nyumbani Zanzibar wazo ambalo limepokewa na kukubaliwa moja kwa moja na SMZ.

# CUF Mtwara kilio wagombea kuenguliwa

**Na Hamisi Nasiri,**
MASASI

CHAMA cha Wananchi (CUF) mkoani Mtwara, kiimelalamikia wagombea wake kuenguliwa katika uteuzi wa kugombea nafasi mbalimbali uchaguzi wa serikali za mitaa.

Wilayani Masasi CUF imesema imesikitishwa vikali na kinapinga mchakato mzima wa uchaguzi wa serikali za mitaa kutokana na wagombea wake wote wa zaidi ya 50 kuenguliwa bila sababu za msingi.

Tamko hilo lilitolewa wilayani Masasi na Katibu wa CUF wilaya hiyo, Hassan Chariche, alipokuwa akizungumza na viongozi wengine wa chama hicho katika kikao cha dharura, baada ya kuona wagombea takribani 50 ambao waligombea nafasi mbalimbali kuenguliwa kwa madai ya kukosa sifa. Alisema CUF ilisimamisha wagombea wao katika kila mtaa, kitongoji na kijiji, na mchakato mzima wa ujazaji fomu ulikwenda vizuri.

Hata hivyo, alisema chakushangaza ni wagombea wote wameenguliwa katika mchakato huo kwa madai kuwa wameshindwa kutimiza vigezo halisi ikiwamo ujazaji fomu.

Alisema wamepita kila mtàa, kijiji na kitongoji kwa ajili ya kuangalia wagombea wao na walichobaini ni kuona karibu wote wemeenguliwa.

Alisema hadi sasa hawafahamu sababu halisi za wagombea kuenguliwa na hakuna uwazi, hali ambayo inatia shaka uchaguzi huo kama utakuwa wa kuaminika wala kuwa huru na haki kwa vyama vya upinzani.

Chariche alisema tayari wameshamwandikia barua msimamizi wa uchaguzi ya kupinga mchakato mzima wa uchaguzi huo, na kwamba wao hawataweka pingamizi lolote kwa sababu hawajui sababu ya wao kupinga.

Alisema katika Jimbo la Masasi pekee walisimamisha wagombea 50 katika vijiji, kitongoji na mitaa, lakini majimbo la Ndanda na Lulindi pia zaidi ya wagombea 40 wameenguliwa.

"Tunashangazwa kuona wagombea wetu wameenguliwa na hatujui sababu ni nini, hivyo sisi tunapinga uchaguzi huu kwa kuwa haki haitendeki," alisema Chariche.

Naye Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi CUF Taifa, Mneke Jafari, alisema wamesikitishwa na jambo hilo la wagombea wa CUF kuenguliwa. Alisema wamezunguka katika wilaya mbalimbali ikiwamo Liwale, Nachingea, Lindi na Masasi, lakini hali ni moja ya wagombea kuenguliwa bila ya kuwekwa sababu za wazi.

"Tunapinga kwanini wagombea wetu waonekane wamekosa sifa halafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wao wamepita kugombea, hapa haki hakuna," alisema Jafari.

Msimamazi wa Uchaguzi Jimbo la Masasi Halmashauri ya Mji Masasi, Zuwena Ungele, alithibitisha kuwapo na malalamiko hayo, na kueleza kuwa yupo katika kikao na atatolea ufafanuzi akitoka.

Naye Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi yenye majimbo ya Lulindi na Ndanda, Jeremiah Lubeleje, alisema wapo baadhi ya wagombea wa upinzani ambao wameenguliwa.

Alisema baadhi ya vigezo ambavyo vimewaondoa ni kuchanganya maelezo ya ujazaji fomu namba mbili na namba tatu.

Alisema yupo aliyejaza maelezo ambayo yalitakiwa yawepo kwenye fomu namba mbili, lakini mgombea ameyajaza katika fomu namba tatu.

Alisema hadi juzi, katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, wagombea wa CCM katika vijiji 67 na vitongoji zaidi ya 300 wamepita bila kupingwa kutokana na sababu hizo.


Distributed via ippmedia

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kulia), akiagana na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ambaye ni Mbunge wa Kigamboni, Dk. Faustine Ndungulile, baada ya uzinduzi wa huduma ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo inayoitwa Jiwezeshe, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Naibu Waziri wa Tamisemi, Josephat Kandege (katikati), Naibu Gavana wa Benki Kuu, Benard Kibesse (kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Sara Msafiri. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Mgogoro ardhi wananchi, mwekezaji waibuka upya

**INATOKA UK. 9**

kwa kuchukua maeneo ya wananchi wa vitongoji vya Mkanada na Mwashikamile kutokana na maslahi yao.

"Mihtasari iliyopo baada ya kukaa vikao halali iliamuliwa mwekezaji afidiwe huko Kihansi, lakini viongozi wetu wa hapa wilayani nao wakaazimia kumfidia kwa kuchukua maeneo yetu, kwa sababu hata wao wana maslahi ndani ya shamba hilo," alisema Nyoni.

Mohamed Mtupeni alihoji mahali ilipo ardhi yenye ukubwa wa hekta 1,800 ambayo serikali iliamuru irejeshwe kwa wananchi kwani anaona badala ya ardhi hiyo kurejeshwa, wao wanapanua shamba kwa kuchukua ardhi nyingine ya wananchi.

"Rais Magufuli aliagiza turejeshewe ardhi yetu yenye ukubwa wa hekta 1,800, lakini badala ya kuturejeshea ardhi yetu, wao wameamua kupanua shamba kwa kuchukua ardhi yetu kubwa zaidi... hili halikubaliki na tunamwomba Waziri Lukuvi aje atuonyeshe ardhi aliyosema itarejeshwa kwa wananchi," alisema Mtupieni.

Uongozi wa shamba la Kapunga haukutaka kuzungumza lolote kuhusiana na mpaka mpya wa shamba hilo uliowekwa na badala yake wakasema msemaji wa suala hilo ni Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune.

Gazeti hili lilipomfuata Mkuu huyo wa Wilaya, alisema kuwa baada ya serikali kuamuru mwekezaji kurejesha hekta 1,800 kwa wananchi, iliamuliwa kuainisha mpaka halisi wa shamba hilo ili ujulikane.

Alisema wataalamu wa ardhi walipokwenda kuhakiki mipaka ya shamba hilo ndipo wakabaini kuwa mpaka wa kisheria uko katika maeneo hayo ambayo yalikuwa yakitumiwa na wananchi bila kujua.

Alisema kabla ya kuwekwa kwa mpaka huo mpya, alikwenda na kuzungumza na wananchi hao na akawafahamisha kuwa maeneo hayo sio yao bali ni mali ya mwekezaji.

"Mpaka uliowekwa sio mpya, ulikuwapo tangu zamani, sisi tumeufufua tu, wananchi walikuwa wakitumia maeneo yale bila kujua kuwa sio yao lakini sasa kwa vile tumeainisha mpaka halisi wameujua na hatutarajii mgogoro huo uendelee," alisema Mfune.

Alisema baada ya kubaini kuna makazi ya watu ndani ya eneo hilo, anakusudia kwenda kuzungumza nao ndani ya siku tano kuanzia sasa ili kuwaeleza hatima yao.

# NMB yasaidia elimu, afya kwa mil. 900/-

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya Sh. milioni 900 zimetolewa na Benki ya NMB katika kusaidia sekta ya elimu na afya katika kipindi cha mwaka 2019.

Meneja wa benki hiyo Kanda ya Nyanda za Juu, Straton Chilongola, alisema, kwa mwaka 2019, imetenga Sh. bilioni moja ili kurejesha faida inayopatikana kwa jamii kwa kuzilenga sekta hizo katika kuunga mkono pia juhudi za serikali.

Alisema fedha hizo hutumika kutoa misaada ya vifaa vya ujenzi, madawati, meza, viti na kompyuta kwa kupitia Kitengo cha Masuala ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) kutoka NMB.

Chilongolo alisema kuna mambo mengi wamepanga kuifanyia jamii, lakini wameamua kuanza na elimu pamoja na afya kwa sababu ni mambo waliyoyapa kipaumbele cha kwanza kwa jinsi yanavyoigusa jamii moja kwa moja.

Alisema hivi karibuni NMB ilitoa msaada wa madawati 100 kwa shule za msingi za Maduma na Uhambila zilizoko Kata ya Maduma wilayani Mufindi.

"Kwa miaka kadhaa sasa tumekuwa mstari wa mbele kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi kwa lengo la kurejesha sehemu ya faida yetu kwa jamii na kwa zaidi ya miaka saba mfululizo tumechangia asilimia 1 ya faida yetu kama sehemu ya uwajibikaji kwa jamii inayotuzunguka," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Jamhuri William, akiwakilishwa na Katibu Tarafa wa Malangali, Andrew Chunga akipokea msaada huo aliishukuru benki hiyo kwa kusaidia sekta ya elimu na kutoa wito kuendelea kutoa misaada mbalimbali katika sekta nyingine ambazo zinakabiliwa na changamoto kubwa.

Alisema msaada huo umekuja kwa wakati mwafaka kwa kuwa shule hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi zikiwamo miundombinu kama barabara, maabara, dawa kwa ajili ya wanafunzi na kuiomba NMB kuendelea kuisaidia shule hiyo na nyingine zikizo katika Wilaya ya Mafinga.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliishuruku benki hiyo kwa msaada wa meza na viti vyenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa Shule za Sekondari ya Mrisho Gambo iliyopo katika Kata ya Mashono Vijijini.

Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro, alisema msaada huo ni sehemu ya mchango wao kwa jamii na kuunga mkono juhudi za serikali kuleta maendeleo.

Akipokea msaada wa madawati 125 kwa ajili ya Shule za Msingi Minigo na Ryaghati wilayani Rorya, Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Simon Chacha, alisema kuwa benki hiyo imekuwa ni mdau mkubwa wa maendeleo wilayani kwake na kuahidi ushirikiano ili kuendeleza mahusiano yao.

Kaimu Meneja wa Kanda ya Ziwa, Amos Mubusi, alisema benki hiyo ilipokea maombi ya kutoa msaada kwa shule hizo na kuyafanyia maombi hayo kazi kwa haraka.

HABARI KIMATAIFA

# ‘Bwana wa vita’ DRC jela miaka 30

**THE HAQUE,** Uholanzi

KIONGOZI wa zamani wa waasi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Bosco Ntaganda, amehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela katika Mahakama ya Kimataifa ya jinai kwa makosa ya uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu.

Wapiganaji waliomtii Ntaganda walitekeleza mauaji ya ukatili dhidi ya raia, Majaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC), walisema mwezi Julai.

Ntaganda, ambaye alipewa jina la bandia “Terminator”, alipatikana na makosa 18 ikiwamo ubakaji, utumwa wa ngono na kuwatumikisha watoto kama wanajeshi.

Hukumu dhidi yake ni ya muda mrefu kuwahi kutolewa katika historia ya mahakama ya ICC na alikuwa ni mtu wa kwanza kupatikana na hatia ya utumwa wa ngono na mahakama ya ICC na mtu wa nne ambaye mahakama hiyo imempata na hatia tangu ilipoundwa mwaka 2002.

**Ntaganda alikuwa kiongozi muhimu ambaye alitoa amri ya kuwalenga na kuwaua raia, Jaji Robert Fremr alisema katika hukumu yake.**

Ntaganda ambaye alizaliwa nchini Rwanda mwenye umri wa miaka 46 muasi wa zamani amekuwa akihusika na mizozo mbali mbali ya kivita nchini Rwanda na DRC.

Wachambuzi wanasema kujisalimisha kwake katika ubalozi wa Marekani nchini Rwanda kilikuwa ni kitendo cha kujilinda, kutokana na hatari iliyokuwa inamkabili baada ya kupoteza mamlaka ndani ya kikundi chake cha waasi wa M23.

Julai, majaji watatu walimpata Ntaganda na hatia ya makosa yote 18 ya uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu uliofanyika katika jimbo lenye utajiri wa madini lililoko Mashariki mwa DRC la Ituri kati ya mwaka 2002 na 2003. Ntaganda alikuwa kiongozi muhimu ambaye alitoa amri ya kuwalenga na kuwaua raia, Jaji Robert Fremr alisema katika hukumu yake.

Waendesha mashtaka walikuwa wamesema Ntaganda alikuwa mtu muhimu katika kupanga na kuendesha harakati za waasi wa Union of Congolese Patriots (UCP) na tawi lake la kijeshi la Patriotic Forces for the Liberation of Congo (FPLC). Kikundi cha kijeshi kiliendesha mashambulio dhidi ya watu walioaminika kuwa hawatoki katika kabila la Wahema, ICC ilibaini.

Katika shambulio moja, wapiganaji 49 waliwakamata watu katika shamba la migomba nyuma ya kijiji kwa kutumia fimbo, marungu, visu na mapanga.

“Wanaume, wanawake na watoto pamoja na watoto wachanga walipatikana katika shamba hilo. Baadhi ya miili ilipatikana ikiwa uchi, baadhi yake ikiwa imefungwa kwa kamba na baadhi ilikuwa imekatwa kichwa,” alisema Jaji Fremr.

Ghasia katika jimbo hilo ziliwaua watu zaidi ya 60,000 tangu mwaka 1999, huku wanamgambo wakipigania udhibiti wa vyanzo vichache vya madini, yanasema makundi ya haki za binadamu. Majaji waliamua kuwa Ntaganda yeye binafsi alimuua Padri wa Kanisa Katoliki wakati wapiganaji aliowaongoza walipofanya uvamizi jimboni humo.

Uhalifu ulifanyika wakati Ntaganda alipohudumu kama Naibu Mkuu wa Majeshi wa Kiongozi wa Waasi wa UCP, Thomas Lubanga.

Mwaka 2012 Lubanga alikuwa mtu wa kwanza kupatikana na hatia katika Mahakama ya ICC na akahukumiwa kifungo cha miaka 14 jela.

Wote waliopatikana na hatia. **BBC**

## Trump: Mazungumzo na Taliban yamekufa

**NEW YORK,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, alisema mazungumzo na kundi la waasi la Taliban yaliyolenga kumaliza vita vya miaka 18 nchini Afghanistan yamekufa.

“Kulingana na mimi, yamekufa na yamekufa,” Rais Trump aliwaambia waandishi wa habari wa White House Jumatatu.

Wiki iliyopita Rais Trump alifuta mipango yake ya siri ya kuupokea ujumbe wa Taliban nchini Marekani baada ya kikundi hicho kumuua mwanajeshi wa Marekani.

Pande mbili zilionekana kuwa na mkataba wa siri na Taliban, zinasema kuwa Marekani ndiyo itakayopata hasara kubwa zaidi kutokana na kufa kwa mazungumzo hayo.

Rais Trump alikuwa amekaribia kuwapokea viongozi wa Taliban pamoja na Rais wa Afghanstan, Ashraf Ghani katika Ikulu ndogo ya Camp David kabla ya kuyafuta mazungumzo hayo ghafla.

Rais huyo alikosolewa kwa kukubali uwezekano kuwapokea Taliban kwa mkutano siku chache tu kabla ya maadhimisho ya mashambulio ya kigaidi dhidi ya Marekani ya Septemba 11, mwaka 2001, ingawa kiongozi huyo alilitetea wazo lake hilo. Taliban hawakuwahi kukubali kumaliza mashambulio yao dhidi ya Afghanstan na vikosi vya usalama vya serikali ya Afghanistan, huku mazungumzo yakifanyika.

Wanajeshi 16 wa Marekani wamekwishauawa mwaka huu nchini humo.

Mnamo mwaka 2001, vikosi vinavyoongozwa na Marekani viling’oa serikali ya Taliban nchini Afghanistan kwa sababu wanamgambo hao waliupatia mtandao wa al-Qaeda fursa ya kuandaa mpango wa mashambulio dhidi ya Marekani Septemba 11. **BBC**


Distributed via ippmedia

Wanafunzi wa moja ya shule nchini Rwanda. Sensa ya hivi karibuni ya Wizara ya Elimu imebainisha shule nyingi zina idadi kubwa ya wanafunzi nchini humo. **PICHA:BBC**

## Yatakiwa kukabili msongamano madarasani

**KIGALI,** Rwanda

SERIKALI ya Rwanda imeanza kushughulikia suala la msongamano wa wanafunzi katika shule kadhaa za nchi hiyo.

Katika shule nyingi hasa za mikoani, chumba kimoja cha shule kinaweza kuwa na wanafunzi zaidi ya 80, wote wakiwa chini ya usimamizi wa mwalimu mmoja pekee.

Wataalamu wa elimu wanasema kwamba msongamano wa wanafunzi madarasani ni moja wapo ya sababu inayochangia kushuka kwa viwango vya elimu katika shule za Rwanda.

Katika Shule ya Msingi ya Gashora Kusini Mashariki mwa Rwanda na maeneo mengine ya vijijini, suala la idadi kubwa ya wanafunzi isiyolingana na idadi ya madarasa ya shule ni jambo la kawaida.

“Sisi hapa darasani tunakaa sakafuni na kuna wengine wanaokaa kwenye madumu ya maji, lakini yule anayeamka mapema ndiye anayekalia kiti.

Tunapendekeza serikali kutafakari suala hili na kutupatia vifaa,” alisema Mwalimu Beata Mushime.

Sensa ya hivi karibuni ya Wizara ya Elimu imebainisha kwamba shule nyingi zina idadi ya kupindukia ya wanafunzi ambapo katika baadhi ya maeneo chumba kimoja kinaweza kuwa na wanafunzi zaidi ya 100.

“Ukiangalia shule nyingi eneo hili zinakabiliwa na tatizo la msongamano mkubwa wa wanafunzi, iwe shule za sekondari ambako darasa la kwanza lina watoto 90 na katika shule za msingi darasa la kwanza lina watoto 85,” alisema. **BBC**

## Mapya yafichuliwa usalama Boeing

**NEWYORK,** Marekani

MFICHUA siri wa Boeing amedai kuwa abiria katika ndege ya 787 Dreamliner huenda wakaachwa bila hewa ya oksijeni iwapo ndege hiyo ikipata hitilafu ya kiufundi ghafla.

John Barnett anasema uchunguzi umebaini kuwa hadi robo ya mfumo wa oksijeni una hitilafu na kuwa vipuri vya ndege hiyo vilivyo na kasoro vimewekwa wakati ndege hiyo ilipokuwa ikiundwa katika kiwanda cha Boeing. Boeing imepinga madai hayo ikisema kuwa ndege zake zote zinaundwa kwa kuzingatia viwango vya usalama vya hali ya juu.

Kampuni hiyo imejikuta shakani siku za karibuni baada ya ajali mbili mbaya zilizohusisha ndege yake ya 737 Max -iliyokuwa ya Shirika la Ndege la Ethiopia na kupata ajali Machi na ajali ya Lion Air ya Indonesia mwaka jana. Barnett, ni mhandisi wa zamani na mdhibiti wa ubora, aliyefanya kazi na Boeing kwa miaka 32, hadi alipostaafu kwa misingi ya afya yake mwezi Machi mwaka 2017.

Kutoka mwaka 2010 aliajiriwa kama meneja anayesimamamia masuala ya ubora wa viwango vya uundaji ndege katika kiwanda cha Boeing cha North Charleston, Kusini mwa Jimbo la Carolina. **BBC**

# Serikali yawakumbuka wenye ulemavu mikopo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeagiza wakurugenzi wa halmashauri zote nchini pamoja na maofisa maendeleo ya jamii kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vikundi vya watu wenye ulemavu ili waweze kunufaika na mikopo inayotolewa na halmashauri hizo.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Joseph Nyamhanga, katika kongamano la asasi za kiraia (Azaki) linaloendelea jijini Dodoma kwa kuzikutanisha asasi zisizo za kiserikali nchi nzima.

Alisema kumekuwa na changamoto ya watu wenye ulemavu kutotumia fursa ya mikopo inayotolewa na halmashauri kutokana na wengi wao kutokuwa na elimu ya ujasiriamali, hivyo kuwafanya wengi wa jamii hiyo kuishi maisha ya utegemezi na kuomba omba mitaani.

"Ninajua kabisa watu wenye ulemavu hawawezi kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha ikiwamo benki kutokana na hali yao, ndio maana serikali kwa kuliona hilo iliamua kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri zote nchini kwa ajili ya kutoa mikopo kwa makundi maalum yakiwamo ya watu wenye ulemavu," alisema Nyamuhanga.

Nyamuhanga alisema kutokana na hilo, halmashauri zinapaswa kuzingatia utoaji elimu kwa watu hao ili waweze kulipa fedha hizo ambazo hutolewa na serikali kwa ajili ya makundi maalum.

Alisema serikali imeamua kutoa agizo hilo, kwa sababu ni hali ya kusikitisha watu wengi wenye ulemavu bado hawajajitokeza vya kutosha kutumia fursa ya mikopo kwa ajili ya kujiimarisha kiuchumi.

"Nawaagiza wakurugenzi watendaji wa halmashauri kupitia maofisa maendeleo ya jamii kutoa elimu ya ujasiriamali ili watu hawa waweze kujiunga kwenye vikundi, kujisajili na kisha kupata mikopo inayotolewa na halmashauri bila masharti magumu," alisema Nyamhanga.

Alisema mikopo inayotolewa na halmashauri ikiwa ni asilimia 10 ya mapato yake ya ndani ni kwa mujibu wa sheria hivyo kila halmashauri ni lazima itenge fedha hizo kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwani kwa halmashauri ambayo haitafanya hivyo watatakiwa kujieleza.

Alisema katika mwaka wa fedha 2018/2019 halmashauri nchini zilitenga jumla ya Sh. bilioni 54.08 kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu lakini mpaka kufikia Juni 30, mwaka huu kiasi cha fedha kilichokuwa kimetolewa ni Sh. bilioni 42.06 ambapo vikundi vya watu wenye ulemavu walipata kiasi cha Sh. bilioni 3.87 tu kiasi ambacho ni kidogo kulinganisha na makundi mengine ambapo wanawake walipata Sh. bilioni 23.18 na vijana Sh. bilioni 15.01.

Alifafanua zaidi kuwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020, serikali imetenga Sh. bilioni 62.22, ambapo wanawake na vijana wametengewa Sh. bilioni 24.9 na watu wenye ulemavu Sh. bilioni 12.4.

Naye Katibu Mkuu wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Tanzania (Shivyawata), Jonas Lubago, alisema watu wengi wenye ulemavu hawana uelewa wa mikopo inayotolewa na halmashauri na ndiyo maana hawajitokezi kukopa na hata wenye uelewa wanakabiliana na changamoto nyingi ikiwamo ya kujiunga kwenye vikundi kwa kuwa kuna baadhi ya maeneo watu wenye ulemavu siyo wengi, hivyo kuwawia vigumu kujiunga kwenye vikundi vya watu watano.

Aliiomba serikali kuangalia kama kuna uwezekano wa kuwakopesha watu wenye ulemavu wakiwa mtu mmoja mmoja.



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani nchini (FCC), Dk. John Mduma (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Hyundai East Africa Ltd, Mehboob Karmali, alipotembelea banda lao, katika maonyesho ya 22 ya Biashara ya Kimataifa Afrika Mashariki 2019, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Machinga wazua tafrani Mwanza

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAFANYABIASHARA wadogo maarufu machinga waliopo pembezoni mwa Barabara ya Pamba na Mtaa wa Sokoni jijini Mwanza, ambao wanatakiwa kuhamia soko kuu la muda Kata ya Mbugani, wamezua tafrani kubwa, baada ya kutaka kumshambulia Mkurugenzi wa Halmashauri ya jijiiji hilo, Kiomoni Kibamba.

Mkurugenzi huyo alikumbana na kadhia hiyo wakati akitoa maelekezo ya kuwataka kupisha maeneo hayo. Zaidi ya machinga 1,000 wanaofanyia biashara eneo la Barabara ya Pamba na Mtaa wa Sokoni, wamepinga kupisha maeneo hayo ambako soko kuu la kisasa jijini Mwanza linajengwa kwa madai maeneo wanakotakiwa kupelekwa hakuna nafasi ya kufanyia biashara.

Walifunga Barabara ya Pamba kwa madai ya kuchoshwa na manyanyaso.

Akizungumza katika soko hilo wenyekiti wa ulinzi na usalama wa machinga mkoani Mwanza, Mahida Suleiman, amesema maeneo yote yamejaa wafanyabiashara wadogo na kwa mujibu wa maelekezo ya awali waliotakiwa kupisha ni waliokuwa ndani ya soko.

"Tunaziomba Mamlaka kuheshimu maelekezo ya Rais John Magufuli ya kutowabugudhi machinga, sisi, hatukatai kufanya usafi kuweka mazingira salama, lakini tunashindwa kuwaelewa mkurugenzi na timu yake kwanini wanaamua kutunyanyasa hivyo," alisema Mahida.

Mkurugenzi wa Jiji la Kibamba, alisema timu ya wataalamu sita kutoka Jiji itapita kwenye maeneo yao kwa ajili ya kuwasajili ili wapangiwe maeneo ya soko la muda Kata ya Mbugani.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, akizungumza katika kikao cha Bodi ya Barabara cha robo ya kwanza kwa mwaka 2019/2020, alimwagiza Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza pamoja na Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, kuona namna bora ya kuwapanga wafanyabiashara wadogo waliopo pembezoni mwa Barabara Kuu ya Mwanza-Musoma na za mitaa ya katikati ya jiji hilo ili wasiendelee kuzagaa ovyo barabarani.

# Diwani ataka shule ifungwe kunusuru kuponda wanafunzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

DIWANI wa Kata ya Kambarage Manispaa ya Shinyanga, Hassani Mwendapole, ameitaka manispaa hiyo kuifunga kwa muda Shule ya Msingi Jomu kutokana na kukabiliwa na uchakavu wa miondombinu ya majengo ya madarasa, huku mengine yakipasuka nyufa, hali ambayo inatishia maisha ya wanafunzi.

Mwendapole alibainisha hayo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichokuwa na ajenda mbalimbali ikiwamo kuwasilisha taarifa za kila kata, kuwa shule hiyo haifai kuendelea kutoa elimu kutokana na maisha ya wanafunzi wake kuwa hatarini kupondwa na majengo.

Alisema malalamiko hayo walishayatoa siku nyingi ya kufanyiwa ukarabati shule hiyo, lakini hakuna utekelezaji, huku majengo ya madarasa hayo yakiendelea kutishia maisha ya wanafunzi, na kwamba ambapo siku moja yanaweza kuanguka na kuleta maafa.

"Kwenye kata yangu ya Kambarage kuna changamoto kubwa sana ya uchakavu wa majengo ya madarasa katika Shule ya Msingi Jomu, ambapo mengine yana nyufa na yapo hatarini kuanguka na kuponda wanafunzi, hivyo ni vyema shule hii ifungwe kwa muda kwanza mpaka pale itakapofanyiwa ukarabati," alisema Mwendapole.

Naye Mkuu wa shule hiyo, Sara Maloda, akizungumza na Nipashe alikiri shule hiyo kuchakaa miundombinu yake, na ina miaka 55 sasa tangu kujengwa mwaka 1964, na ina madarasa 12, lakini madarasa matano hayatumiki kabisa kutokana na kupasuka nyufa.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Geofley Mwangulumbi, alisema kiasi cha Sh. milioni 14.9 zimeshatengwa kwa ajili ya kukarabati majengo ya madarasa ya shule hiyo, na utekelezaji wake utaanza hivi karibuni.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA 2 ENEO MOJA ZINAUZWA** Zipo Ukonga Mombasa. Ya mbele mjengo wa kisasa vyumba 4 nyingine chumba na sebule 4 kiwanja robo eka. Za kupaua. Bei maelewano. Piga simu: 0719 619444 / 0782 574669.

**VIWANJA VITATU VINAUZWA,** NO.1-1341-1890 SQM NO. 2-1342- 1391 SQM NO.3 1343- 1556 SQM BLOCK A KISUKURU-TABATA. SIMU. 0754 857523/0786 857523

## NAFASI ZA KAZI

**Wanahitajika wanaume wenye umri kuanzia miaka 30 hadi 45** kwa nafasi za udereva (Ikiwemo Class C, C1, C2 na C3). Wanahitajika wanawake wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 35 kwa nafasi za mauzo (sales za bidhaa). Mshahara wa kuvutia utatolewa. Mawasiliano piga 0714 634 046. Piga simu kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni tu.

## MCHANGANYIKO

**KISIMA CHA BEI NAFUU KILICHOKAMILIKA:** Tutakuchimbia kisima na kukuwekea pampu, tutaacha maji yanatoka kisimani kwako. tupigie Simu:0714 564 651 / 0692 006 546.

**Tunasafifisha visima virefu na vifupi** kwa kumia mashineza kisasa na tunapima ubora wa maji.Gharama zetu nafuu!! Simu:0623 528 465 / 0657 746 365.

**Kuchimba kisima Dar na Pwani** kwa gharama nafuu!! Mita 1 Sh.60,000/= tu! Tunaweka bomba (UPVC), kokoto (Gravels) na pampu bure! Piga:0623 528 465 / 0657 746 365.

## 2 ACRE YARD FOR RENT

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HEADLIGHT ERASTO KWEKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3736-0017-2016** kilichotolewa na DESTINY SEKONDARI DAR ES SALAM mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **WBU/RB/9276/2019.**

115506002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Magret M. Sanga** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari SCANIA LORI yenye namba za usajili **T289 ABX** Lori hilo liliibwa likiwa kwenye maegesho katika barabara ya Njombe Songea na baadae kadi yake iliungua ndani ya nyumba yake Taarifa imetolewa polisi na kupewa RB. NO; **NJ/TR/RB/722/2019**

215507802

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**WUZHOU INVESTMENT** wa nyakato Kahama, anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC.825 CBX.** Yeyote atakaiona atoe taarifa katika kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya Polisi. **KAH/RB/TR/843/2019.**

215506402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;224/2019**

**Ombi la REHEMA PETER JINGU Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu PETER KINYALI JINGU**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 28/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/11/2019.

215506502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;216/2019**


**Ombi la SIMON FRANCIS MUHEBU Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu FRANCIS HERMAN MUHEBU**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 12/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 24/10/2019

215506602

## KUPOTEA KWA CHETI



**REUBEN ELIAS NGILI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0439-0067** kilichotolewa na **BUPANDAGILA SEKONDARI** mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MSI/RB/448792/2019.**

115505902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;216/2019**

**Ombi la FAUSTINA WANGAELI URONU Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu FLORA WANGAELI URONU**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/11/2019

215507602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Samwel Donald Kiwanga** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili **T329 AYN.** Yenye chases namba **LH.1190016057** Injini namba **3L 2815320.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

215507902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. YA 2019 BAINA YA**

**GLORY LEONARD SHIRIMA....................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**KASSIM PASPHILY NKARA**
**FRANK MACHUMU**
**FINI FINANCIALS & REAL ESTATE AGENCY**
**SERVICES COMPANY LIMITED MBOGO AUCTION MART........WADAI-WA**
**DENNIS KIOBA**
**DEVID HESAU MWAKITWANGE**

**KWA:**
**KASSIM PASPHILY NKARA**
**FRANK MACHUMU**
**FINI FINANCIALS & REAL ESTATE AGENCY**
**SERVUCES COMPANY LIMITED MBOGO AUCTION MART........WADAIWA**
**DENNIS KIOBA**
**DEVID HESAU MWAKITWANGE**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yao ambayo maelezo yao yameelezwa katiak nakala ya maombi ambayo inapatikana katika baraza hili. Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika baraza hii wewe binfsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tareh 02/12/2019 saa 3:00 asubuhi kwa mujibu wa maombi hayo mntakiwa kuleta uetetzi wenu kwa maandishi.
**Anglizo:** kama hamkuhudhua taehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa mmepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yenu.
Hati hii imetolewa kwa am yangu na lakiri/muhuri wa Baraza hili leo 04/10/2019.

215506302

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**MATRIMONIAL CAUSE NO. 11/2019**

**ADELA EVARIST LYIMO....PETITIONER**

**VS**

**EVARIST ADOLPH URIO....RESPONDENT**

**NOTICE OF PETITION**

Whereas petition, a copy of wish has been presented to this court by the above named petitioner, will be mentioned before the magistrate on the 13 November 2019 at 08:30 o'clock in the afternoon.

Take notice that all parties to the petition are hereby required attending before the magistrate on the said day at the said time and that in the event of default by any party to enter appearance, the petition shall be proceeded within in accidence with the provisions of the law of Marriage (Matrimonial proceedings) Rules.
Dated at Dodoma, this 18/10/2019

215506802

## KUPOTEA KWA CHETI



**ZAINABU BAKARI SEIF** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2731/0024** kilichotolewa na KITEO SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/329314/2019.**

115506102

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa**

**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0767 223311**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Distributed via ippmedia

# EDERSON HATIHATI KUIVAA LIVERPOOL

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola hajui kama atakuwa na golikipa, Ederson wakati Manchester City itakapoivaa Liverpool katika mchezo wa Ligi Kuu England utakaochezwa Jumapili.

Ederson alitolewa nje kipindi cha pili kwa matatizo ya kuumia misuli ya nyama za paja wakati City ikitoka sare ya bao 1-1 na Atalanta kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumatano.

Akiwa hajaokoa hatari yoyote kipindi cha kwanza, Ederson nafasi yake ilichukuliwa na Claudio Bravo, ambaye kazi yake ya kwanza ilikuwa ni kuuokota mpira kwenye nyavu zake baada ya Mario Pasalic kufunga kwa kichwa akisawazisha goli la Raheem Sterling.

Mambo yakawa magumu zaidi kwa City baada ya Bravo kuonyeshwa kadi nyekundu baada ya kumchezea vibaya Josip Ilicic, hali iliyosababisha beki wa kulia, Kyle Walker, kuitwa kutoka benchi na kuvaa glovu za kukaa golini.

City sasa mchezo uliopo mbele yake ni ule wa pale kwenye dimba la Anfield, ambapo watawavaa vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool na Guardiola anajua kwamba Ederson pengine huenda asicheze.

"Sijui chochote kwa sasa. Ni tatizo la misuli ya nyama za paja. Haikuwa kubwa sana, lakini alitakiwa kutolewa nje ili kuepuka kuumia zaidi," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari wakati alipoulizwa kuhusu hali ya Ederson.

"Hakujisikia vizuri katika dakika ya mwisho ya kipindi cha kwanza. Ndio maana tukaamua kumbadilisha. Lakini kwa sasa hatujui."

# Onana aitamani Ligi Kuu England

**AMSTERDAM,** Uholanzi

GOLIKIPA wa klabu ya Ajax, Andre Onana, amesema anatamani kuhamia katika Ligi Kuu England, ili kutimiza ndoto zake, kwa mujibu wa ESPN.

Kipa huyo wa kimataifa wa Cameroon mwenye umri wa miaka 23, aliyasema hayo baada ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Chelsea, uliomalizika kwa sare ya 4-4, Jumanne.

Licha ya kusaini mkataba wa muda mrefu wa kuendelea kuitumikia Ajax, Onana, amedhihirisha suala hilo mbele ya waandishi wa habari ambao walitaka kufahamu nini malengo yake, baada ya kuendelea kuonyesha uwezo mkubwa anapokua langoni.

Mkataba mpya wa Onana na Ajax unatarajiwa kufikia kikomo Juni mwaka 2022.

"Hapa England kuna soka la ushindani, kila mchezaji anatamani kucheza katika ligi ya nchi hii, ninatumai ipo siku ndoto zangu za kuja hapa, zitatimia."

"Ligi ya England imekua na mvuto wa aina yake, kila wiki nimekua naifuatilia. Ninaamini hakuna litakaloshindikana kwa mimi kuwa hapa katika siku za maisha yangu ya kucheza soka, kwa sasa ninaendelea kuheshimu mkataba wangu na Ajax, ninafurahia maisha nikiwa na klabu yangu tangu nilipokua chaguo la kwanza," alisema Onana.

Onana amekua akifuatiliwa kwa ukaribu na baadhi ya klabu za Ulaya, huku vyombo vya habari vya England vikizitaja Tottenham Hotspur na Manchester United kuwa katika mawindo makali ya kuisaka saini yake.

Onana alijiunga na Ajax mwaka 2015 akitokea Barcelona, baada ya kukuzwa kutoka kwenye kituo cha kulea vipaji cha La Masia.

Msimu uliopita aliisaidia Ajax ilifika nusu fainali kwa mara ya kwanza kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu mwaka 1997, na alikuwa sehemu ya kikosi cha Cameroon kilichoshiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2019) zilizopigwa nchini Misri.





# *Allegri apigiwa debe kumrithi Solskjaer*

**ROME,** Italia

KOCHA mkongwe wa Italia, Marcello Lippi, amesema atafurahi kuona Massimiliano Allegri, akipata nafasi ya kuinoa Manchester United siku moja.

Kocha wa sasa wa United, Ole Gunnar Solskjaer, ambaye ni mchezaji wa zamani wa timu hiyo, anaonekana kuwa kwenye kuti kavu kutokana na matokeo mabaya ya timu hiyo.

Baada ya kuachana na Juventus majira wa joto, Allegri kwa sasa yuko katika mchakato wa kutafuta kibarua kipya. Mtaliano huyo amependekezwa kama mtu anayeweza kuleta mafanikio Old Trafford licha ya hivi karibuni kuhusishwa na kutakiwa Bayern Munich iliyomtimua kocha wake Niko Kovac.

Lippi aliyebeba Kombe la Dunia akiwa na Italia mwaka 2006, anaamini Allegri ni mtu sahihi zaidi kutua United.

"Manchester United ni klabu yenye historia kubwa katika soka la Kiingereza. Wamekuwa katika kipindi kigumu miaka ya hivi karibuni, lakini ni klabu ya kipekee," alisema.

Lippi aliongeza: "Kwanza kabisa Allegri ninamwona kama mtaalamu wa mfano ambaye ana mtindo wa Juventus katika damu yake.

"Urafiki wangu mkubwa na (Sir Alex) Ferguson unaniruhusu kusema kwamba anaweza kuwa chaguo bora kwa United."

# Pochettino: Ushindi wa Spurs ni hatua ndogo

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino amewaonya wachezaji wake wa Tottenham kuwa wamefikia "hatua ndogo" baada ya kikosi chake kupata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Red Star Belgrade kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Tottenham walipata pointi zote tatu juzi Jumatano, shukrani kwa mabao ya Son Heung-min aliyefunga mawili na mengine kutoka kwa Giovani Lo Celso na Christian Eriksen.

Ushindi huo wa Tottenham ulikuwa wa kwanza ugenini tangu Mei 8, mwaka huu, ikiwa imecheza mechi tisa kwenye mashindano yote, na Pochettino anaitaka timu yake kujijenga zaidi kwa ajili ya ushindi wa pointi tatu katika kila mchezo.

"Nafikiri yalikuwa matokeo mazuri zaidi nje ya nyumbani," alisema wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Tulihitaji kuwa na mchezo kama ule kwa ajili ya kurudisha ubora wetu na kuweza kujiamini zaidi kwa kikosi chetu.

"Kiwango kilikuwa kizuri sana katika nafasi ngumu kwelikweli. Nina furaha kubwa, lakini tunahitaji kuendelea kupambana. Hii ni hatua ndogo tu kwa sasa."

Tottenham imekuwa timu ya kwanza ya Uingereza kushinda mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye uwanja wa Rajko Mitic, mwaka mmoja tangu Liverpool ipokutana na kichapo pale, na kuufanya ushindi huo kuwa muhimu zaidi kwa macho ya Pochettino.





# LEONARDO AMBWATUKIA ZIDANE KUHUSU MBAPPE

**PARIS,** Ufaransa

MKURUGENZI wa Michezo wa Paris Saint-Germain, Leonardo amemjia juu, Zinedine Zidane, akibainisha kwamba, alikasirishwa na kocha huyo wa Real Madrid kumzungumzia Kylian Mbappe.

Mbappe mwenye umri wa miaka 20 amekuwa akihusishwa kwa muda mrefu na kuondoka PSG, ambako alianza kung'ara tangu alipowasili mwaka 2017.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa ameripotiwa kwamba anawaniwa na Madrid na Zidane alisema Jumanne kwamba, ni ndoto yake kuona Mbappe akiwachezea miamba hao wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

Leonardo alimbwatukia Zidane baada ya PSG kuibuka na ushindi wa bao 1-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Club Brugge juzi Jumatano, akisema nyota huyo anatakiwa kuachwa.

"Inanikasirisha na inanikera. Huu sio muda wa kuzungumzia hili. Bado ana miaka miwili na nusu kwenye mkataba wake na sisi. Ni muda wa kuacha kuzungumzia jambo hili," amesema akinukuliwa na RMC Sport.

"Yeye ni mchezaji muhimu zaidi kwetu. Ni mchezaji kijana wa Ufaransa ambaye Ufaransa wanaye kwa sasa. Ni bingwa wa dunia na hata mchezaji bora wa duniani.

"Hakuna muda sasa wa kulizungumzia hili au kuanza kumwangaza kwa tochi."

Mbappe amefunga mabao tisa katika mechi 11 alizocheza hadi sasa msimu huu na ana mkataba na miamba hao wa jijini Paris hadi mwaka 2022.

# Simeone ataka vitendo tu kwa wachezaji

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone amekubali lawama baada ya Atletico Madrid kufungwa mabao 2-1 na Bayer Leverkusen, lakini akasisitiza klabu yake "inahitaji kujibu kwa vitendo na sio maneno."

Atletico ilikosa nafasi ya kufuzu kwenye hatua ya mtoano wa timu 16 kwenye ligi ya juzi Jumatano baada ya bao la kujifunga la Thomas Partey na lile la Kevin Volland kumaliza 'umwambafai' wao wa kucheza mechi 11 bila kufungwa. Atletico awali walionekana walikuwa na presha kubwa kwenye mchezo huo uliopigwa dimba la BayArena hadi walipojikuta wakiwa nyuma kwa 2-0, huku Alvaro Morata akifunga bao la kufutia machozi dakika za majeruhi baada ya Nadiem Amiri kutolewa nje kwa kadi nyekundu.

Atletico sasa wamecheza michezo mitatu bila ushindi kwenye Ligi ya nyumbani na mashindano hayo ya Ulaya na walionekana walikuwa na tatizo kwenye safu yao ya ushambuliaji, huku Diego Costa akionyesha kiwango kizuri kabla ya kutolewa nje.

Na Simeone sasa amesema lawama zote anazipokea, lakini amewataka wachezaji sasa kujibu kwa vitendo.

"Sio sawa kwangu mimi kumlaumu mchezaji mmoja," alisema baada ya mchezo huo.

"Mtu ambaye anapaswa kulaumiwa kwa timu kufanya vibaya ni mimi kwa sababu sikuwapa hamasa wakati wa kuanza mchezo, kitu ambacho walikifanya kipindi cha pili.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




Distributed via ippmedia

# BENZEMA: MIMI SIO GWIJI HAPA MADRID

●●● Mshambuliaji huyo afunguka baada ya kufikisha mabao 50 Uefa, aipiku rekodi ya mkongwe De Stefano...

**MADRID,** Hispania

KARIM Benzema amesisitiza kuwa "yeye sio gwiji" baada ya kufikisha mabao 50 kwa Real Madrid katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumatano.

**Benzema alifunga mabao mawili wakati Madrid ikiwafumua Galatasaray 6-0 kwenye mechi ambayo Rodrygo Goes ndiye alikuwa nyota wa mchezo kwa kufunga mabao matatu 'hat-trick' hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu.**

Akiwa mara kwa mara akishutumiwa, Benzema sasa amepitwa na Cristiano Ronaldo (105) na Raul (66) ambao wameifungia mabao mengi zaidi Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mfaransa huyo aliipiku rekodi ya mkongwe Alfredo Di Stefano aliyefunga mabao 49, lakini alikataa kuzungumzia kwamba yeye ni gwiji wa Madrid.

"Tulifunga mabao, tulicheza vizuri na hatukuruhusu kufungwa bao. Hakika ilikuwa ni sherehe kubwa kwa mashabiki," alisema Benzema akinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo.

"Mimi sio gwiji. Wakati niliposajiliwa na klabu hii kamwe sikufikiria kama nitafikia hatua hii, nina furaha kubwa.

"Nitajaribu kuisaidia timu na kuwa kwenye ubora wangu, nataka kuendelea kuisaidia. Najisikia jasiri, kama ninaweza kuwasaidia wachezaji wenzangu kwa kuzungumza pale, nitafanya hivyo, hii ni sehemu ya uzoefu wangu kwenye klabu."

Rodrygo alikuwa nyota kwa kufunga kwake 'hat-trick', huku Sergio Ramos pia akifunga penalti kwenye ushindi huo mnono wa Madrid.

Benzema alimzungumzia pia Rodrygo na Eden Hazard, akimtaka kuimarika zaidi baada ya uhamisho wake kutoka Chelsea wakati wa dirisha la kipindi cha majira ya joto kilichopita.

"Rodrygo alionekana yupo vizuri zaidi, haogopi. Anacheza mpira na napenda hicho wakati nikimuona mchezaji kijana akicheza vizuri kama vile," alisema.

"Kwa Hazard, yeye ni mchezaji mkubwa na muunganiko wetu ni mzuri tu. Kidogo kidogo utaona jinsi atakavyojipambanua kuwa mchezaji mkubwa kwa kiasi gani.

"Naamini ni suala la muda tu, kwani yeye ubora wake ni wa hali ya juu na ana uwezo mkubwa wa kuimarika."

## ZISIKUPITE

### BARCA YAMBEBA VELVEDE

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde, bado anapewa ushirikiano na bodi ya klabu hiyo, licha ya kuwapo kwa hoja mbalimbali kuhusiana na mwenendo wa timu hiyo inavyocheza. ***(ESPN)***

### WENGER KUTUA ARSENAL

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, anajiandaa kutua katika klabu ya Bayern Munich ifikapo mwishoni mwa msimu huu. ***(Sun)***

### HAVERTZ ANUKIA UNITED

KIUNGO wa Bayern Leverkusen, Kai Havertz, yuko huru kuanza mchakato wa kuondoka katika Ligi ya Bundesliga. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 20 anawindwa na Manchester United. ***(Marca, via Metro)***

### SOLSKJAER KUSAJILI WAWILI

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema kuwa anaweza kusajili nyota "wawili wapya" katika kipindi cha dirisha la Januari, lakini mchakato mkubwa wa usajili utafanyika kwenye kipindi cha majira ya joto mwakani. ***(Evening Standard)***

### GIROUD, PEDRO SOKONI

CHELSEA inajiandaa kupokea ofa ya kumuuza straika Mfaransa Olivier Giroud (33), winga Mhispania Pedro, wakati beki wake wa kushoto Mhispania Marcos Alonso (28), akiwa anapambana kuhakikisha anapata muda mzuri wa kuendelea kubakia hapo Stamford Bridge. ***(Telegraph)***

### PEDRO ANUKIA FENERBAHCE

KLABU ya Fenerbahce imesema kuwa inataka kumsajili winga Mhispania Pedro, akiwa mchezaji huru katika kipindi cha majira ya joto mwakani. ***(Takvim, via Mail)***

### HUSILLOS MATATANI

HATIMA ya Mkurugenzi wa Soka wa West Ham, Mario Husillos, iko katika wakati mbaya kutokana na timu hiyo kufanya vibaya. ***(Guardian)***

### HUGHTON AIKATAA CITY

KOCHA wa zamani wa Brighton, Chris Hughton, ameweka wazi kwamba hataki kukubali ofa ya kutua Stoke City, kutokana na kuwa na matumaini ya kupata klabu nyingine inayoshiriki Ligi Kuu England. ***(Sun)***

### MATIC SAFARI IMEIVA

KIUNGO wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Serbia, Nemanja Matic, ambaye ana umri wa miaka 31, yuko huru kuondoka katika klabu hiyo ifikapo Januari mwakani. ***(Manchester Evening News)***

### RANGNICK, UNITED WATETA

MKURUGENZI wa Michezo wa zamani wa Red Bull Salzburg na RB Leipzig, Ralf Rangnick, ameanza mazungumzo na maofisa wa Manchester United kwa ajili ya kuajiriwa katika klabu hiyo. ***(Athletic, via Mirror)***

### LAMPARD: HATUSAJILI JANUARI

CHELSEA haina mpango wa kusajili mchezaji yoyote katika kipindi cha dirisha dogo la Januari hata kama adhabu yao ya kufungiwa usajili itakuwa imemalizika, kocha Frank Lampard, amesema. ***(Talksport)***

# HABARI MICHEZO

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 8 | 7 | 0 | 1 | 16 | 3 | 21 |
| 2. Lipuli | 10 | 5 | 3 | 2 | 18 | 10 | 18 |
| 3. Tanzania Prisons | 10 | 4 | 6 | 0 | 13 | 8 | 18 |
| 4. Kagera Sugar | 9 | 5 | 2 | 2 | 12 | 7 | 17 |
| 5. Ruvu Shooting | 10 | 4 | 3 | 3 | 8 | 8 | 15 |
| 6. JKT Tanzania | 10 | 4 | 3 | 3 | 7 | 7 | 15 |
| 7. Alliance | 10 | 3 | 5 | 2 | 8 | 7 | 14 |
| 8. Polisi Tanzania | 8 | 4 | 1 | 3 | 9 | 9 | 13 |
| 9. Namungo | 9 | 4 | 1 | 4 | 7 | 7 | 13 |
| 10. Mtibwa Sugar | 10 | 3 | 3 | 4 | 9 | 11 | 12 |
| 11. Coastal Union | 10 | 3 | 2 | 5 | 8 | 9 | 11 |
| 12. Mbao | 10 | 2 | 5 | 3 | 8 | 10 | 11 |
| 13. Mwadui | 10 | 2 | 5 | 3 | 7 | 9 | 11 |
| 14. Azam | 6 | 3 | 1 | 2 | 5 | 3 | 10 |
| 15. Kinondoni MC | 7 | 2 | 2 | 3 | 4 | 6 | 8 |
| 16. Biashara United | 9 | 2 | 2 | 5 | 5 | 9 | 8 |
| 17. Mbeya City | 9 | 1 | 5 | 3 | 7 | 15 | 8 |
| 18. Young Africans | 4 | 2 | 1 | 1 | 5 | 4 | 7 |
| 19. Ndanda | 8 | 1 | 4 | 3 | 6 | 8 | 7 |
| 20. Singida United | 10 | 0 | 4 | 6 | 4 | 15 | 4 |

## SBL YAJIPANGA KUWAPA FURAHA MASHABIKI STARS

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA mechi dhidi ya Equatorial Guinea, Mdhamini Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), kupitia kinywaji chake cha Serengeti, imesema kuwa itaendelea kuwapa raha mashabiki wa soka hapa nchini.

Taifa Stars inatarajia kucheza mechi ya kuwania tiketi ya kufuzu mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2021), dhidi ya Equatorial Guinea itakayochezwa Novemba 15, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Meneja Masoko wa SBL, Anitha Msangi, alisema SBL kupitia bia yake ya Serengeti, ipo bega kwa bega na Taifa Stars pamoja na mashabiki wa soka hapa nchini.

**Anitha alisema, ili kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wanafurahia mechi hiyo, SBL, imejipanga kuweka "screen" kubwa katika maeneo mbalimbali nchini, kwa lengo la kuonyesha mchezo huo bure huku nafasi ya kufurahia bia ya Serengeti ikitolewa pia.**

"SBL kupitia bia yetu ya Serengeti tutaendelea kuwapa burudani mashabiki wa soka kwa kuhakikisha tunaiwezesha timu yetu ya Taifa inafanya vizuri, lakini kupitia bia ya Serengeti kuwafanya mashabiki wafurahie mechi pamoja na bia yao pendwa, tujitokeze kwa wingi kuishangilia timu yetu huku tukifurahia bia yetu ya Serengeti ambayo ni fahari yetu," alisema Anitha.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Kidao Wilfred, alisema timu itaingia kambini mapema wiki ijayo ili kujiandaa na mchezo huo.

Kidao alifafanua kuwa, baada ya mchezo huo, kikosi cha timu hiyo kitasafiri kuwafuata Libya katika mchezo wa pili ambayo utachezwa Novemba 19, mwaka huu, ikiwa ni siku nne tu baada ya kucheza mchezo wa kwanza.

"Tunawaomba Watanzania kwa pamoja tuungane kwa ajili ya timu yetu ya Taifa. Tujitokeze kwa wingi siku ya mechi na kuishangilia kwa nguvu zetu zote ili kuwapa hamasa wachezaji wetu waweze kufanya vizuri," alisema Kidao.


Distributed via ippmedia

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao (kulia), akizungumza kuhusu maandalizi ya mechi kati ya Taifa Stars dhidi ya Equatorial Guinea, itakayochezwa Novemba 15, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam. Katikati ni Meneja Masoko wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Anitha Rwehumbiza na Mwenyekiti wa Kamati ya Hamasa, Haji Manara. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Pasha ajipanga kuiteka Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Pasha anatarajia kutoa burudani katika onyesho maalumu litakalofanyika Jumapili kwenye ukumbi wa Msangazi uliopo wilayani hapa, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Baa ya Msangazi, Jeniffer Simwasi, alisema kuwa lengo la kuandaa onyesho hilo ni kuwapa burudani wakazi wa Muheza na hakutakuwa na kiingilio cha aina yoyote.

"Tunawaomba wakazi wa Muheza wajiandae kupata burudani nii, onyesho litafanyika Jumapili na litaanza saa 1:00 usiku, wakae mkao wa kula kutokana na msanii huyu alivyojiandaa, watarajie kushuhudia kazi ya kiwango cha juu," alisema Simwasi.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha wakazi wa Muheza wanapata muda wa kupumzika, wameahidi kuwaandalia burudani ya kila Jumamosi kwa kuwaalika wasanii wanaotamba na hii itawasaidia kuimarisha mahusiano baada ya kumaliza kazi.

Pasha (pichani chini), alisema kuwa amefurahi kupata nafasi hiyo ya kutoa burudani kwa wakazi wa Muheza, na anaahidi atafanya kazi kwa kiwango cha kimataifa.

"Kwangu ni heshima kubwa kupata nafasi hii, ninatarajia kuwapa burudani nzuri mashabiki wangu wa Muheza, ninawaomba wajiandae kushuhudia burudani ya kiwango cha juu," alisema msanii huyo.



## *Mwakyembe, Kiwale kupanga mikakati*

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Sunday Kiwale, anatarajia kukutana na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, kwa malengo la kujadili maandalizi ya safari yake ya kuelekea nchini Uingereza, imefahamika.

Kiwale anatarajia kuondoka nchini ifikapo Novemba 24, mwaka huu kwa ajili ya kwenda kupigana na Tommy Frank, katika pambano la kuwania ubingwa wa IBO, raundi 12, ambalo litakalofanyika Novemba 29, mwaka huu, nchini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, baada ya kumaliza mazoezi yake ya asubuhi kwenye viwanja vya Shule ya Uhuru, Kiwale alisema kuwa anaamini kikao chake na Mwakyembe kitamsaidia kumjenga zaidi.

"Mwakyembe aliniambia anataka kukutana na kuzungumza na mimi kabla ya kusafiri kwenda Uingereza kwa ajili ya pambano langu, naamini nikikutana naye atanipa mbinu nyingi ambazo zitanisaidia katika pambano hilo," alisema Kiwale.

Bondia huyo aliongeza kuwa anaendelea vema na programu za maandalizi kwa ajili ya pambano hilo na anajiamini atakwenda kufanya vizuri, lakini akihitaji Watanzania wazidi kumwombea dua ili aweze kuipeperusha vema bendera ya taifa.

"Naomba Watanzania wenzangu wazidi kuniombea na kunisapoti ili niweze kuiwakilisha vema bendera ya Tanzania, nimejipanga vizuri, sina hofu na mpinzani wangu, japo kuwa ninakwenda kupigana kwao," alisema Kiwale.

Bondia huyo ananolewa na kocha, Rajabu Mhamila maarufu Super D, ambaye aliliambia gazeti hili kuwa Kiwale atarejea nyumbani na mkanda wa pambano hilo.

Michezo
Ijumaa Novemba 8, 2019
Nipashe



Benzema: Mimi sio gwiji Madrid UKURASA 30



Beki wa Simba, Shomari Kapombe (kulia), akimiliki mpira huku akizongwa na wachezaji wa Tanzania Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. Mechi hiyo iliisha kwa suluhu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Distributed via ippmedia

# SIMBA, PRISONS HAKUNA MBABE

## Maafande hao waendelea kushikilia rekodi ya kutopoteza mchezo msimu huu...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara Simba wamelazimishwa sare ya bila kufungana dhidi ya "Maafande" wa Tanzania Prisons kutoka Mbeya, katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**Ulikuwa ni mchezo uliotimua akili na nguvu hasa kwa Prisons ambao walikuwa wakitumia njia zote kuhakikisha haifungwi, na inamaliza kwa kushinda mechi au kutoka sare, jambo ambalo walifanikiwa.**

Matokeo ya mechi hiyo yameifanya Simba, kupata sare yake ya kwanza kwenye katika Ligi Kuu Bara msimu huu, ikicheza mechi tisa, kushinda saba, kupoteza moja na sare moja wakati Prisons imeendeleza rekodi yake safi ya kutopoteza mechi yoyote mpaka sasa, ikiwa imecheza mechi 11, ikishinda mechi nne na sare saba.

Simba bado inaendelea kuongoza ikiwa na pointi 22, huku Prisons inayofundishwa Adolph Rishard na ikishika nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo baada ya kufikisha pointi 19.

Kipindi cha kwanza Prisons iliishinda Simba kwa kufanya mashambulizi ya hatari zaidi kwenye lango la mabingwa hao watetezi. Ilianza kulitia msukosuko lango la Simba dakika ya 11 tu, wakati Salum Kimenya alipopata krosi safi akiwa hajakabwa na beki yoyote wa timu pinzani, akaachia shuti lililotoka pembeni kidogo mwa lango la wapinzani wao.

Dakika ya 31, lango la Simba lilikuwa kwenye majaribu wakati straika wa Prisons, Jeremiah Juma, aliingia ndani ya eneo la hatari, lakini alichelewa kupiga mpira na kukutana na kipa, Aishi Manula ambaye katika harakati za kuudaka ulimponyoka na kuambaambaa kama unaeelekea wavuni, lakini ghafla mpira ulibadili uelekeo na kwenda pembeni mwa lango, kabla ya mabeki kuuokoa na kuwa kona tasa.

Jaribio pekee la hatari la Simba lilifanywa dakika ya 39, wakati Meddie Kagere alipoambaa na mpira winga ya kushoto na kupiga krosi iliyokatika na kutaka kujaa wavuni, lakini ukaokolewa kwa ustadi na kipa, Jeremiah Kisubi.

Kipindi cha pili karibuni chote, Prisons waliamua 'kupaki basi', na kushambulia kwa kushtukiza kitu kilichoifanya Simba kushambulia mfululizo, lakini wachezaji wake walishindwa kuipenya ngome ya wapinzani wao ikiongozwa na Nurdin Chona.

Ilifanya majaribio dakika ya 56, Deo Kanda, alipopiga mpira juu akitazamana na kipa, Kagere naye aliukosa mpira wa krosi ambao ungeweza kuipa timu yake goli, huku kinda, Rashid Juma, alipoikosesha timu yake bao, baada ya kupiga shuti kali akiwa nje ya eneo la hatari lililotoka kidogo pembeni mwa lango.

Dakika ya 72 nusura Prisons iandike bao, baada ya Samson Mbangula kubaki na kipa Manula, lakini kipa huyo aliokoa kwa ustadi na dakika ya 87 pia walikosa bao la wazi kupitia kwa Lambart Subianka.

Ligi hiyo ya juu nchini inatarajia kuendelea tena leo kwa Ndanda FC kuwakaribisha Yanga kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara wakati Azam FC itawaalika Biashara United kutoka Musoma huku Kagera Sugar wakiwa wageni wa KMC FC kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

# Yanga, Ndanda hapatoshi Bara

**Na Somoe Ng'itu**

IKIWA chini ya kocha mpya wa muda, Boniface Mkwasa "Master", Yanga inatarajia kuteremka ugenini kuwakabili Ndanda FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, ulioko mkoani Mtwara.

Kuelekea mchezo huo, Mkwasa, alisema kuwa wanatarajia mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani kutokana na wapinzani wao kuwapa changamoto kila wanapokutana.

Mkwasa alisema kuwa anaamini wachezaji wake watakuwa makini kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo huo, ambao kwa Yanga ni wa tano, tangu kuanza kwa msimu huu.

Alisema kuwa katika mechi hiyo, atawakosa wachezaji wake nane ambao ni pamoja na Juma Balinya, Lamine Moro, Abdul-Aziz Makame, Ali Ali, Maybin Kalengo, Paul Godfrey, Cleofas Sospeter na Feisal Salum "Fei Toto".

Mechi nyingine za ligi hiyo zinazotarajiwa kuchezwa leo ni kati ya Azam FC dhidi ya Biashara United kwenye Uwanja wa Azam Complex wakati KMC FC yenyewe itawakaribisha Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

# Samatta anukia Newcastle, West

**LONDON, England**

KLABU za Newcastle na West Ham zimeweka wazi nia yake ya kuwania saini ya straika wa KRC Genk na Timu ya Taifa ya Tanzania, Mbwana Samatta.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 26, alifunga bao moja katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa Jumanne wiki hii, ambayo ilimalizika kwa Liverpool kupata ushindi wa mabao 2-1.

Taarifa zinasema kuwa thamani ya Samatta, mchezaji huyo wa zamani wa Simba ya Tanzania na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ni pauni milioni 10.

Samatta ndiye Mfungaji Bora wa Ligi Kuu Ubelgiji, msimu uliopita aliifungia Genk mabao 25 na kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

Mtanzania huyo tayari ameshafunga mabao sita katika mechi 13 za Ligi Kuu Ubelgiji, ambazo amecheza msimu huu.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042